

UISLAMU SAFI

**KATIKA MANENO NA UJUMBE
WA IMAM KHOMEINI (R.A)**

BISMILLAHIR RAHMANIR RAHIIM

الإسلام الصافي

في كلام و خطاب الإمام الخميني

**Mtarjum:
Hazrat Zahra Foundation (a.s) of Tanzania.**

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION**

ISBN: 978 - 9987 -17 - 007 - 4

Kimeandikwa na:
Imam Khomeini (R.A.)

Kimetarjumiwa na:
Hazrat Zahra (a.s.) Foundation of Tanzania

Kimehaririwa na:
Alhaji Ramadhani S. K. Shemahimbo
Na
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

Kimepitwa na:
Shuaib Ayoub Nyello
Na
Mubarak A. Tila

Toleo la kwanza: Juni, 2011

Nakala: 1000

Toleo la pili: Januari, 2016

Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv.com
Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

Dibaji	1
Neno la Mchapishaji	2
Utangulizi.....	4
Sehemu ya Kwanza:.....	7
Sura ya Kwanza:	7
Uwezo wa Uislamu katika Jamii.....	7
Sura ya Pili:.....	18
Sababu za Waislam Kubakia Nyuma	18
Sura ya Tatu:	21
Uislam Safi na Uislam wa Marekani	21
Sehemu ya Pili:	23
Sura ya Kwanza:	23
Uislam ni Dini ya Siasa.....	27
Sura ya Pili:.....	33
Sharti la kuutambua Uislamu Safi.....	33
Sura ya Tatu:	49
Uislamu ni Dini ya Mapambano	49
Sehemu ya Tatu:.....	77
Uislam wa Mustadhaafin na Wanaoonewa	77
Sehemu ya Nne:	85
Uislam na maisha ya kawaida.....	85
Sehemu ya Tano:	88
Sura ya Kwanza:	88
Sifa za Uislam wa Kimarekani	88
Sura ya Pili:.....	94
Uislamu Umeleta Uongofu na Fursa.....	94
Sehemu ya Sita:.....	100

Kuulinda Uislam Safi dhidi ya Uislam wa Kimarekani.....	107
Sura ya Kwanza:	107
Watetezi wa Uislamu Safi	107
Sura ya Pili:.....	107
Kuutetea na kuuhami Uislamu wa Kimarekani	107
Sehemu ya Saba:	115
Uadui dhidi ya Uislamu Safi	115
Sura ya Kwanza:	115
Sababu ya Mapambano na Uadui	115
Sura ya Pili:.....	119
Mbinu za Mapambano na Uadui.....	119
Sehemu ya Nane:	123
Utaratibu wa Kutoa Utawala kwa Uislam wa Kimarekani.....	123
Sura ya Kwanza:	123
Maadui Wakuu wa Uislam Safi.....	123
Sura ya Pili:.....	125
Pigo kwa Uislam kwa Kutumia Jina la Uislam	125
Sura ya Tatu:	127
Kuleta mgawanyiko katika mataifa na kuzua tofauti baina ya Waislam.....	127
Sehemu ya Tisa:	128
Wadhifa wa watu kuutambua Uislam Safi	128
Sura ya Kwanza:	128
Jukumu la mataifa na watu	128
Sura ya Pili:.....	131
Nafasi ya Hawza na Vyuvo Vikuu	131

DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenyewe kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

SMS: +255 778 300 140

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kifarsi kiitwacho, *Islam-e-Naab dar Kalaam wa Payaam-e-Imam Khomeini (Pure Islam – Selected from the Speeches and Messages of Imam Khomeini)* kilichochapishwa na Taasisi ya Majumui ya Uchapishaji wa Athari za Imam Khomeini (r.a.). Sisi tumekiita, Uislamu Safi.

Kitabu hiki kinalezea harakati za Imam Khomeini (r.a.) katika kuihudumia dini, na jinsi ambavyo aliipa uhai dini hii baada ya kukanyangwa na maadui wa Uislamu wa ndani na wa nje. Katika kitabu hiki, utaona mbinu alizotumia mwanachuoni mchamungu huyu mpaka kufanikisha Mapinduzi Makubwa ya Kiislamu, si nchini Iran tu bali ulimwenguni kote athari ya Mapinduzi haya imeenea.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu ambapo maadui wa Uislamu wameungana ili kuuangamiza. Lakini kama ailivyosema Allah ('Azza wa Jalla) katika Qur'ani Tukufu:

"Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia." (9:32) Allah anasema kweli, kwa hakika hawatafani-kiwa katika njama yao hii.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwashudumia Waislamu, hususan wa-zungumzaji wa Kiswahili.

Tunaishukuru taasisi ya Hazrat Zahra Foundation of Tanzania kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tun-

washukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa na changamoto kubwa kwa wasomaji wetu.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation

UTANGULIZI

Siku zote, Imam Khomeini (r.a) alikuwa ana fikra kuipa uhai dini na kuwatafutia maslahi wanajamii. Alikuwa mwanazuoni wa dini, si kwa maana ya uanazuoni tu peke yake, bali pia ni kiongozi na mlinzi wa dini.

Allah (s.w.t) aliileta dini kwa wanadamu ambao maisha yao ni ya ardhini, kwa muda maalum, katika mazingira maalum ya jamii, kwa kutumia akili, fikra na utukufu waliokuwa nao unaowaletea athari kiroho na kimwili pia.

Mwanadamu ameumbwa akiwa mwenye khiyari kwa kiasi kikubwa kulingana na mahusiano yake ya asili ambayo kamwe hawezu kuwa na subira. Kila mwanadamu ana sifa maalum ambayo siku zote huuona ukweli, kwamba yeze anapitia katika njia iliyo sahihi ili asipotee.

Dini ya Allah (s.w.t) ilikuja kumkomboa mwanadamu aweze kujitambua, kuzifanya kazi fikra alizotunukiwa na Mola wake na kukabiliana na kila aina ya mashaka yatakayojiteza mbele yake.

Hapa ni lazima tufahamu kwamba, laiti kama kusingelikuwa na mashaka ya kidunia, basi kusingelikuwa na njia ya kumfikisha mwanadamu huyo kwenye ukamilifu wa kibinadamu. Hali hii ndiyo inayomfanya mwanadamu azidishe juhud ya kutafuta elimu kwa bidii aweze kuufikia ukamilifu uliokusudiwa.

Imam Khomeini (r.a) ni mmoja kati ya wanafalsafa wachamungu na mwenye kiwango cha uwelewa wa hali ya juu, mwanazuoni na faqihimkubwa katika masuala ya dini. Hii ndiyo sababu iliyomfan-ya awe mlinzi mkuu wa dini na kuiwezesha ioneckane hai, na yenye thamani. Alihakikisha kwamba anapambana na kila hali, vikwazo, na matatizo mbalimbali ili kuitetea dini ya Allah (s.w.t).

Kuipa dini uhai ni moja kati ya njia aliyoichagua Imam Khomeini (r.a). Akaonekana ana muonekano pekee katika kukabiliana na ugumu na vikwazo ili kuitetea dini. Ndiyo maana alijitokeza, akajitoa muhanga maisha yake yote kwa kutetea na kuihudumia dini kwa moyo wake wote.

Dini ya Allah (s.w.t) ni amri iendayo na wakati ambayo ni wajibu kwa kila mwanadamu wa kila zama na ni mojawapo ya matendo yatakayohesabiwa.

Katika kukabiliana na yote haya, yaani, imani katika dini, iliyokuwa baina ya ukweli na ushujaa, itakuwa ni chachu na changamoto ya kutetea dini na kuipa uhai kwa maslahi ya utukufu wa dini.

Imam Khomeini (r.a) alikuwa mujahid aliyetoea mwanga kwa wanadamu wote. Ni kiongozi shupavu aliyeuangusha uongozi dhalimu na kuibadili Iran kutoka kwenye udhalimu huo, sambamba na kuipa uhuru na ukamilifu kwa ajili ya kila Muislam.

Bila ya kuwa na fikra za uhuisho, maslahi ya Uislamu na mapinduzi ya Kiislam, basi Imam Khomeini (r.a) asingeweza kulifkia daraja hilo ambalo lilikuwa na wito maalum wa kuihuisha dini na maslahi ya jamii. Mapinduzi ya Kiislam yalichukua sura mpya na yalipatikana katika kipindi kilichokuwa na muingiliano wa tamaduni na mila za kimagharibi, lakini dini iliwaita watu katika uadilifu, ukombozi na uhuru ambao taifa lilikuwa likihitajia.

Uislam wa Imam Khomeini (r.a) ulikuwa katika kipindi ambacho binadamu wote walikuwa wakihitaji uongozi bora na wa haki. Imam Khomeini (r.a) alibainisha kwamba ni Uislam tu ambao ndiyo una haki ya kuongoza jamii na ubora wake ndiyo mwongozo wa dunia uletao manufaa kwa watu wote.

Fatwa zake zilikuwa mwongozo wa jamii iliyo huru ambayo ndiyo inayoongoza umma wa sasa na ni kielelezo cha juhudi ita-

kayofanikisha kufaulu kwenye mashaka ya dunia. Ulimwengu wa Kiislam unahitaji mwongozo bora na ulio na kanuni zinazokabiliana na fikra huru.

Kiongozi mkuu wa mapinduzi ya Kiislam hakuwa tofauti na Uislam na maumbile, na hii ndiyo maana halisi ya **Uislam Safi**. Uislam huu ndiyo ambao Imam Khomeini (r.a) aliyutangaza, akausimamia kidete ili kuhakikisha kuwa juhud zake za kutafuta elimu na uchunguzi wa hali ya juu ulikuwa ndiyo faraja na njia sahihi ya kukamili-sha jukumu lake alilokuwa nalo katika dini.

Alipoanza kutoa maelezo yake, ujumbe wake na hotuba zake, Imam Khomeini (r.a) alihakikisha kwamba anaulingania Uislam ulio sahihi na kupambana na fikra potofu zilizokuwamo ndani ya Uislam.

Katika miaka ya mwisho ya uhai wake, alitumia fikra na busara zake juu ya aina hizo mbili za Uislam, yaani; **Uislam Safi** na **Uislam wa Kimarekani**, ambao ndiyo ulikuwa kwenye nyoyo za Waislam.

Hivyo, kwa kutumia maneno aliyotuachia Imam Khomeini (r.a), tunaweza kupata fursa ya kuzifanyia uchunguzi na kuzihakiki fikra zake ili tuweze kubainisha na kutambua mahusiano yetu na Uislam.

Tuna matumaini kwamba, fikra hizi zitakuwa ni njia na mwongozo wa kuufikia **Uislam Safi** na sahihi na kuutambua Uislam ulionasibishwa na Umarekani,

**Taasisi ya mipango na uchapishaji athari za
Imam Khomeini (r.a)**

SEHEMU YA KWANZA

MUHTASARI SURA YA KWANZA UWEZO WA UISLAM KATIKA JAMII

Jamii na Uislam

Uislam ni dini iliyolewa kwa ajili ya watu wote ulimwenguni ili iwaongoze kwenye ukweli na kuachana na batili sambamba na kuifuata njia hiyo ambayo itawasaidia hapa duniani na katika akhera yao pia.

Uislam una huruma kwa wote. Uislam unawahurumia watu wote, si kwa ajili ya kukuhurumia wewe tu, bali, Uislam ni kwa ajili ya kuwaliwaza wote na si wewe tu.

Uislam umekuja kuwaondolea watu machungu na kuwakomboa waweze kuondokana na mabaya. Uislam umekuja kuyakomboa matalifa yote.

Ukisema Uislam ni kama dini nyinginezo, yaani ni dini ambayo hivi sasa dhahiri yake imetufikia, laa! si hivyo. Kila kinachofanya wa na mwanadamu kinafanya kwa masharti ya akili, akhlaq, kwa mwonekano wa dhahiri na pia adabu katika matendo yote ambayo mwanadamu anayafanya yana umuhimu na ni yenye kuingiliana na Uislam. Mfano si uongozi tu, bali hata katika masuala ya kijamii na kisiasa, ni lazima Uislam uhitajike.

Uislam ni mali ya wote na si mali ya mtu binafsi, bali ni kwa ajili ya watu wote na si mali ya Waislam tu, Uislam umekuja ili kuwaon-

doa watu watoke kwenye njia waliyopotea na kuwaongoza wafuate njia iliyonyooka. Uislam si kama dini nyinginezo zilizokuja kuongoza umma mmoja maalum kimaada na kidunia tu.

Qur’ani tukufu na Sunna ndiyo mwongozo na hakimu wa watu wote ama vizito hivi viwili vinawaongoza watu kuwafikisha kwenye ukamilifu. Hilo ndilo tegemeo kuu. Mitume pia walikuja kwa kila kitu, yaani kuongoza kiroho kama walivyotubainishia na ambavyo pia Qur’ani imebainisha.

Uislam ni dini iliyo tofauti na dini nyingine ambazo si za *tawhid* (za kumwamini Mungu mmoja tu), bali ilikuwa ni dini iliyoshamiri na kujihusisha katika mawanda yote, yaani, masuala ya mtu binafsi, jamii, *kimaada* (kidunia), *kimaanawiya* (kiroho), kiutamaduni, kisiasa, mipango na uchumi.

Uislam una utamaduni wa kumjenga mwanadamu bila ya kujali rangi yake, lugha yake na sehemu atokayo. Bali, unamjenga mwanadamu katika mawanda yote ya uchumi, *akhlaq* (tabia), kumwongoza aondokane na ujinga, kumfikisha kwenye elimu na tahakiki – uchambuzi.

Uislam unapinga uadui, ujisadi na unapambana vikali na ujisadi katika uongozi. Madhumuni ya Uislam ni kumfikisha mwanadamu **mahali** ambapo ataweza kuifuata njia sahihi katika maisha ya kijamii, kibinafsi, kisiasa na kumfanya mwanadamu huyo awe na moyo wa kutosheka maishani mwake.

Kanuni zilizomo ndani ya Uislam ndizo hitajio la kila mwanadamu. Kanuni hizi ni nyepesi na ni za wazi. Uislam ni njia na mwenendo wa kufuatwa na kila mtu katika jamii na una kanuni maalum zenye nidhamu ya hali ya juu. Kwa kubainisha ni kwamba, kanuni hizo za Kiislam ni za Uislam sahihi ambao mwanadamu anatakiwa kwenda nazo sanjari katika maisha yake yote.

Mtazamo wa Kiislam ni wa *ki-maanawiya* (kiroho). Malezi ya kidini ni ya nafsi ambayo pia humjenga mwanadamu awe na mtazamo wa *ki-maada* (kidunia) na kumwezesha aweze kujua namna gani anaweza kutambua na kuyatumia maisha ya *ki-maada* katika ulimwengu huu.

Uislam katika maisha ya *ki-maada* una mtazamo wa *ki-Mungu*, na katika Uungu kuna mtazamo wa *ki-maada*. Uislam umejumui-sha kila hali ambapo wewe mwenyewe pia unatakiwa ushiriki kikamilifu katika suala zima la uongozi na kujiongoza wenyewe kama ambavyo Allah (s.w.t) alivyoamrisha tunatakiwa tuende nao sanjari. Uongozi wa *ki-maada* pia ni moja ya uongozi katika Uislam na uongozi huu ni moja ya uongozi wa kiuadilifu na viongozi wake wanatakiwa lazima kuwaongoza na kuwafanya watu kazi.

Hakuna tofauti yoyote baina ya watu katika Uislam. Uislam unatii na kutekeleza haki ya kila taifa na haki ya kila dini, awe Mkristo, ama awe Myahudi. Watu wote katika ulimwengu huu wana haki sawa. Ulimwengu wote unahitaji mapenzi, kutafuta ukombozi wa *mustadhaafina* - wanaodhulumiwa - na unataka kila mmoja afikie daraja la utukufu.

Haijawahi kudhaniwa kwamba Uislam ni kama dini nyingine ambazo mahusiano ya *ki-maanawiya* ni baina ya mtu na Allah Mtukufu tu, basi. Uislam unayo ratiba maalum ya maisha na uongozi. Uislam umeongoza kwa takriban miaka 500 na zaidi na pia upo katika ratiba maalumu ya kumwongoza mwanadamu tofauti na zilivyo dini nyingine.

Hukumu zilizopo zilizokuja katika Uislam, ziwe za kisiasa, au ziwe zinahusiana na uongozi, ama ziwe hukumu zinazohusiana na mambo ya binafsi, jamii, utamaduni, yote haya, zipo kwa mahitaji ya mwanadamu.

Uislam unamwangalia mwanadamu tangu kabla hajazaliwa. Anapozaliwa tu, basi, anakuwa tayari ameshakadiriwa kila kitu kuhusiana na maisha yake na *taklifu* - wajibu - wake unakuwa tayari umeshaainishwa. Hata anapokuwa bado yu masomoni, anapoingia na kuwa sehemu ya jamii, mahusiano yake - yote hayo - yamo kwenye ratiba maalum inayohitaji kufanyiwa kazi. Wala si katika dua na ziyara tu, si katika swala tu, bali, ni moja kati ya hukumu za Kiislam. Dua na ziyara ni kati ya mambo muhimu ya Kiislam. Lakini, ndani ya Uislam pia kuna siasa na utawala. Uislam ni mamlaka makubwa yanayoongoza.

Siku zile ambazo hakukuwa na habari zozote juu ya nchi za Magharibi, wakazi wa nchi hizo za Magharibi na sehemu ya Marekani wanayoishi Wamarekani wenyewe ngozi nyekundu, huko watu walikuwa wakichinjwa na walikuwa katika maisha ya hali ya kutisha. Nchi kubwa mbili; Uajemi na Roma, ziliingia katika hatia ya uchokozi, umwinyi, ubaguzi na kutawaliwa na wakoloni na ndipo hapo ambapo Allah (s.w.t) kwa kupitia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alileta sheria zilizomtoa mwanadamu kutoka kwenye udhalili na kumfikisha kwenye utukufu.

Uwezo wa kuongoza Jamii

Katika karne nydingi zilizopita, mamlaka makubwa ya Kiislam - kufanyia kazi nusu tu ya kanuni za Kiislam - zilifanikiwa kuanzisha nchi zilizokuwa bora zenye utamaduni wa hali ya juu.

Kutokana na fitna zilizojitokeza katika karne ya mwisho, hususan kwenye (mzunguko) mwaka wa kumi baada ya ushindi wa mapinduzi ya Kiislam, kulienea propaganda zenye ikhtilafu za kudhoofisha taifa chapakazi la Iran kutoka katika Uislam.

Ndani ya Qur'an Tukufu zipo aya za kuwaongoza watu wote ambazo ni hukumu za Kiislam. Baadhi ya aya hizo ni kama zifutazo:

1. *Suurat Fuswilat*: Aya ya 42.

لَا يَأْتِيهِ الْبَاطِلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِّنْ
حَكِيمٍ حَمِيدٍ

“Hautakifika upotofu mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na Mwenye Hekima, Msifiwa.”

2. *Surat Al Maidah*: Aya ya 48 - 50:

وَأَنْزَلَنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ
الْكِتَابِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا
تَشْتَبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَأَنِ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا
تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ..... أَفَحُكْمُ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ
مِنَ اللَّهِ حَكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ.

“Na tumekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu na kuyalinda, basi hukumu baina yao kwa yale aliyoyeremsha Mwenyezi Mungu, na kila (Umma) katika nyinyi, tumeujalia sharia yake na njia yake.”

“Na hukumu baina yao kwa yale aliyoyeremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate mapenzi yao, nawe jihadhari nao wasije wakakutia kwenye fitna ukaacha badhi ya yale aliyokeremshia Mwenyezi Mungu...”

“Je, wanataka hukumu za kijahiliya? Na ni nani aliye mzuri zaidi kwa hukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini.”

3. Suuratul Aali Imran: Aya ya 85.

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ
مِنَ الْخَاسِرِينَ

“Na mwenye kutaka dini isiyokuwa Uislam haitakubaliwa kwake,
naye katika akhera ni mionganoni mwa wenyewe kupara hasara.”

Suuratul Al furqaan: Aya ya 1.

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ
لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا

“Mwenye baraka ni yule aliyeteremsha Qur’ani kwa mja wake ili iwe
muonyaji kwa walimwengu.”

4. Suurat Al An’am: Aya ya 90:

أَوْلَائِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبِهُدَاهُمْ أَفْتَدِهِ قُلْ لَا
أَسْتَلِكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ

“Hao ndio ambao Allah amewaongoza, basi fuata muongozo wao,
sema: sikuombeni malipo juu ya haya, hayakuwa haya ila ni
mawaiidha kwa walimwengu wote.”

5. Suuratul al Ambiyaa: Aya ya 107:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ

“Nasi hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu”

Hukumu zilizotafsiriwa hazina nafasi katika hukumu za Kiislam

Hapa ni lazima turejee katika sheria za Allah (s.w.t) na tupime kwa kulinganisha na zile zilizotafsiriwa. Je, zinaendana na hukumu za Kiislam? Je, ipo njia ya kuweza kuzitafsiri kwa makini na usahihi? Au tayari zipo kamili? na Je, zinakwenda na wakati maalum? Na kama ni hivyo, basi hamna haja ya kuzifanyia tafsiri na tafsiri zake hizo ndizo zitakazojitoa zitumike katika hukumu.

Je, ni sheria zipi zaweza kutafsiriwa?

Kwa kawaida zipo aya zisizojitosheleza zinazoweza kutafsiriwa ziweze kuwaongoza watu katika maisha ya kiroho na kimaada. Aidha, zipo aya bora zinazoweza kuongoza maisha ya kiroho na kimaada na zisizohitaji tafsiri. Kutohana na rai ya kifalsafa, ipo kauli ya mwanzo kabisa inayohusiana na sheria isemayo ya kwamba: "... **mliona kuwa mwanadamu ana maisha mawili ...**"

Ya Kwanza: Ni sheria kwa kuongoza maisha ya kimaada, yaani, maisha ya duniani ambayo ni maisha yasiyomtosheleza mwanadamu.

Ya Pili: Ni sheria bora. Kutohana na sheria hizi, mwanadamu anaweza kuishi maisha ya kiroho, yaani, maisha ya mwisho ambayo hayo ni kwa ajili ya ulimwengu wa akhera.

Kila moja kati ya maisha haya mawili hujengeka kwa jitihada na juhudzi za mwanadamu mwenyewe ambaye ndiye mtayarishaji mkuu wa maisha yake. Falsafa iliyotumika ndani ya Qur'ani tukufu ni kwamba, sheria zote zimethibitishwa na Mitume wote. Mitume wamethibitisha kwamba, maisha haya mawili kujengeka kwake kuhahitaji maandalizi ya lazima. Ili kuthibiti hili, maada na sheria za kiroho walizokuja nazo Mitume zinatosheleza na kila mmoja lazima arejee Qur'ani, humo atapata maelezo mazuri.

Hivyo, kama tulivyotangulia kusema hapo mwanzo kwamba, kuna sheria ambazo zipo kwa kuongoza maisha ya *ki-maada* peke yake, au maisha ya kiroho peke yake. Basi, sisi hatuzitambui sheria kama hizo katika dini na hatukubaliani nazo.

Sheria za Kimaada na za Kiroho Katika Uislam

Sheria zote zilizopo katika Uislam zina sehemu mbili na zote zina mtazamo wa maisha ya kimaada na wa kiroho pia.

Mfano: *kulingania* katika *tawhid* (Umoja wa Allah) na *taqwa* (kumcha Allah) ambalo ni *linganio* lililokuwa bora katika *malinganio* yote katika Uislam na kujengeka kwake kunasaidiana na maisha ya kiroho.

Katika maisha ya kimaada ni kusaidia nidhamu ya nchi, maisha ya kijamii, na masuala ya kiutamaduni. Iwapo pia ikaingizwa na suala la *tawhid* na *taqwa*, hapa wananchi roho zao zitakuwa kubwa na kamilifu na pia utukufu utapatikana katika maisha ya kijamii na kisiaza.

Kanuni Mali

Mfano uliopo katika Uislam ambao ni kwa ajili ya kuongoza nchi na inayohitajia maisha ya kimaada ambayo chimbuko lake ni maisha ya

kiroho, mtazamo wake ni kusaidia kazi za maisha ya kiroho ambayo pia itaweza kumweka karibu zaidi na Allah (s.w.t).

Kanuni na Kusimamia Sheria

Moja kati ya sheria kuu za umma zilizokuja katika Uislam ni sheria ya kuzishika sheria nyingine za Allah (s.w.t). Mfano; sheria za makosa, kupoteza, dharura, shinikizo na mfano wa hizi. Sheria hizi ni za kuzisimamia sheria nyingine.

Kwa kupitisha sheria hizi, Uislam unakwenda sanjari na mahitaji ya wakati, nchi, watu na zinatosheleza. Hivyo basi, mahitajio ya kila kitu huja kabla ya kuleta sheria hizi katika baadhi ya nchi au watu kulingana na mabadiliko katika sheria za kwanza.

Sheria zinazokwenda na wakati na zinazohitajika katika nchi hazina tofauti na kanuni za kisheria zinazoingiliana na nidhamu za nchi. Aina hii ya sheria katika dola ya Kiislam inaweza ikathibitishwa kupitia kwa wasomi wa dini - maulamaa - ambao pia watalinganisha kwa pamoja na sheria za Kiislam.

Mfano: Ili kulinda nchi au miji, kunahitajika masharti au sheria ambazo hazitakuwa kinyume na Uislam na wasomi wa dini watalithibitisha hilo kuwa kamwe halitaweza kujitokeza jambo lolote kuhusiana na hilo.

Katika mfano mwengine utaona kuwa katika baadhi ya nchi za Kiislam kulikuwa hakuna mahitaji ya kuwepo kwa benki au kumi-liki akaunti au mali na mfano wa hayo, au kuunda jeshi katika kipindi hicho ukilinganisha na kipindi hiki ilikuwa ni kinyume kabisa. Kulikuwa hakuna idara ya posta na telegrafu kama ilivyo sasa, lakini kanuni za Kiislam zilikuwa hazizuii chochote kuwepo na kuanzishwa kwa taasisi kama hizi.

Hivi sasa, wanadini ambao ni maulamaa wa Kiislam lazima wawe macho na fikra zozote ambazo zitakuwa kinyume na kanuni za Kiislam na kuanzishwa asasi zozote ambazo zinahitajika na zina manufaa kwa nchi.

Maendeleo na Demokrasia katika Uislam

Uislam ni dini ambayo imekuja ikiwa tayari na mipango ya shughuli za *kimaada* ili kuweza kumfikisha mwanadamu katika njia ya *kimaanawiya*.

Asili ya kuutambua Uislam inakuja pale pindi jamii itakapokuwa ni yenye kufuata mfumo wa *taqwa* na uadilifu.

Uislam unaweza kulinda uhuru wetu, kutokana na Uislam tunapata mwongozo, Uislam unaweza kulinda pia uchumi wetu. Uislam unakubali sanaa na miongozo, lakini uko kinyume na kila kitu ambacho ni cha ovyo, mamlaka yetu haikubaliani kabisa na vitu kama hivyo, lakini inaafikiana na kila ambacho ni mwongozo na tamaduni zenyе kufungamana na Uislam.

Uislam unapambana na maovu, kama tunavyobainishiwa kuwa sanaa zetu ni zile zinazofungamana na Uislam, na kusiwe na madhara kwetu, kwenye idara zetu zifungamane na Uislam na uchumi na tamaduni zetu zisiende tofauti na Uislam. Sisi wenyewe ndio tuijideshe na kujiongoza na kamwe wala tusikubali kufanyiwa kila kitu na Wamarekani. Wakati tunapouzungumzia Uislam hatuna maana ya kwenda kinyume na mwongozo na maendeleo, bali kufanya hivyo ni kinyume na akida zetu ambazo ndio msingi katika Uislam ambao ni asasi ya wapenda maendeleo.

Uislam ni Dhamana ya Furaha na Uhuru wa Mwanadamu

Uislam na serikali ya Kiislam ni safari ya kimungu ambayo kazi yake ni kutoa furaha kwa watoto wake katika dunia na akhera, ku-

wapandisha daraja la tumaini na kupambana na dhulma na ufisadi ili kuwafikisha katika ukamilifu.

Kivuli cha Uislam ni uhuru kwa maana ya ukombozi wa kweli, na wenyе uhakika, kama tunahitaji uhuru katika nchi yetu, kama tunahitaji nchi iwe mali yetu, ni lazima sote kwa pamoja tuwe chini ya bendera ya Uislam:

“Na tushikamane sote kwa pamoja na wala tusifarakane”

Hii ni amri ya Allah (s.w.t) ni wajibu wetu kuitii, na kuacha kila ambacho ametukataza. Pia, kwamba sote tushikamane na kamba ya Allah (s.w.t). Kamba hapa ni Uislam, njia iliyonyoka ni Uislam.

Ili tufikie baina ya haki na uumbaji, ni Uislam, hivyo ni lazima “tushikamane na Uislam”, tusifarakane na kuwa katika vikundi. Ili nchi yenu iweze kujitegemea yenyeewe ni lazima muwe huru, mtambue thamani ya Uislam wenu ambao umewatoa katika shimo.

Hivyo basi, Uislam kwa ajili yetu ni uhuru, uhuru uliokamilika na sahihi. Uislam ndio utakaotufanya sisi tuweze kujitegemea wenyeewe, Uislam ndio utakaoweza kufanya nyoyo zetu ziwe na nguvu na msimamo na hivyo ndivyo tutakuwa ni wakakamavu.

SURA YA PILI

SABABU ZA WAISLAM KUBAKIA NYUMA

Uislam ni moja katika dini zilizoteremshwa na Allah (s.w.t) kwa ajili ya kuongoza umma na kuondoa ikhtilafu baina yao, kuwaongoza ili kufikia katika ukamilifu, na kuondoa dhulma na pia umekuja ili kuwaamsha waliolala.

Lakini, Waislam karibu wote, na hususan waliokuwamo katika dola za Kiislam, bado hawajajua ile siri ya kuja kwa Uislam kwa ajili yao. Ama walikuwa wameghafirika au wameghafirishwa na matatizo yaliyokuwa yamejitokeza katika historia nzima. Na ndiyo yaliyosababisha wawe mbali katika kujifunza elimu ya Uislam, hivyo, hawakuweza kutumia hidaya iliyokuja kwa ajili yao au kuondokana na athari hiyo waliyokuwa nayo na ndiyo sababu hawakuweza kuitumia.

Tatizo sugu la Uislam ni kuwa mbali na Uislam na Qur’ani. Laiti Waislam wangefuata sawa sawa amri za Allah (s.w.t) kama alivyosema:

”وَاعْصُمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَ لَا تُفْرِقُوا“

"Na shikamaneni pamoja na kamba ya Allah wala msifarakane"

Kama tungekuwa tukifuata amri hii na kukatazana mabaya, basi matatizo hayo yote, ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi yangeweza

kuondoka na tungeweza kukabiliana na nguvu ya aina yoyote ile, lakini kwa kuwa tupo katikati ya dimbwi la kughafirika na baadhi yetu kughafirishwa, tumeweza kubaki katika mambo yaliyo Haramishwa, na kama hatutaweza kuitafuta njia ya haki na kufuata amri za Allah (s.w.t) basi tutaendelea kubaki hivyo na tusubiri matatizo zaidi.

Ni lazima tuone kwamba, hadi pale watu wa mashariki wenyewe watakapotambua kuwa wao pia ni viumbe, wao pia ni taifa, mashariki pia ni sehemu, kamwe hawataweza kujikomboa wao wenyewe kwa mikono yao, ni lazima wakabiliane na wamagharibi ambao ndio upotovu mkuu wa Uislam, hivyo kama hatutafanya hivi basi tutakuwa tukijipoteza sisi wenyewe.

Ni lazima tutambue kuwa Uislam ndiyo dini kuu kuliko dini zote duniani, ambayo ipo mashariki na wao ndio wenyewe kuipoteza, kama hawataifuata dini hii au kutojua ni nini, na wao ni kina nani na kujua kuwa nchi yao ni kama nchi nydingine basi hawataweza kukabiliana na wamagharibi na ni lazima wajitahidi kukabiliana nao.

Wenyewe mtafakari fikra hii kwamba hii ni nchi yenu, na kila mmoja wenu kila mahali alipo lazima aamke. Mlifahamu taifa lenu kwamba na ninyi mpo, mna dini yenu, mna akiba zenu na mna kila kitu ambacho vyote hivi wamevichukua kutoka katika mikono yenu.

Kufungamana kwetu na asiyekuwa sisi, hii haikuwa ni akida yetu kwamba hakuna mwengine isipokuwa asiyekuwa Mmagharibi, hapa si mahala pake na kamwe haiwezi kuwa hivyo.

Sisi ni lazima tufungamane na mashariki, watu wetu wazuri wanatuambia kuwa fungamaneni na wamagharibi pia, si kwa kuwa hakukuwa na mitazamo yao, hapana! Sisi tunaweza tukasimama wenyewe na kufanya kazi, sisi wenyewe tunaweza tukajisimamia we-

nyewe na tutoe ahadi kuwa tukikata mkono na utamaduni ambao ni wa kifisadi, basi tutafikia katika maisha yenyе ubinadamu.

Hivyo suala hili la kubaki nyuma ni sisi wenyewe kupenda dunia na kuendelea kubaki katika tamaduni za sasa za ulaya na kufuata akida za viongozi wao, na kuacha dini na utamaduni wake.

SURA YA TATU

MAELEZO YA JUMLA

Uislam Safi na Uislam wa Marekani

Watoto wangu wapenzi *mujahidina!* Kitu kimoja tu ambacho mnatakiwa mkitafakari ni; kuhuisha na kusimamisha **Uislam Safi wa Muhammad** (s.a.w.w). Uislam ambao washika bendera wake ni wale walio pamoja na wanaodhulumiwa pamoja na mafakiri duniani na adui zao ni wale makafiri na wenye kulimbikiza mali na kuwijazia mapesa katika mifuko yao.

Uislam ambao wafuasi wake wa kweli ni wale ambao siku zote hawathamini mali wala utajiri, na adui wao mkubwa ni udanganyifu na wapenda madaraka na kamwe hawapendi utukufu. Uislam ni dini ya watu *mujahidina* na wanaofuata haki na uadilifu, ni dini ya watu ipendayo waliohuru na waliokombolewa, ni maktaba yenye kupambana na wasiopenda ustaarabu.

Tangu pale Uislam ulipoasisiwa hadi sasa, kuna njia mbili, kuna mistari miwili: mstari wa kwanza ni kwa wale watu wapendao wepesi, kwamba lengo lao lote ni kutafuta tonge moja la chakula wakala kisha wakalala, kisha wakamuabudu Allah (s.w.t), hawa ni Waislam. Lakini, mwanzo wa kila kitu katika mtazamo wao ni kutafuta wepesi.

Mfano wa mnyama ambaye hushibisha tumbo lake, matamanio yake, hukamilisha kwa kila kitu, asili, hufunga na kufanya ibada zote za kisheria lakini si kukaa na kutafakari kwani binaadamu hapaswi kuijingiza mwenyewe katika makosa, au kufikiria ni jinsi gani taifa hili tukufu la Kiislam lilifanya kazi kubwa kwa ajili yake, au kwa

upande mwingine Manabii (a.s) na Mawalii wakubwa, hawa pia walikuwa ni moja katika maktaba na mstari mmoja kwa kutumia umri wao wote ili kuindosha dhulma na yote yaliyokuwa yamejaa katika ulimwengu huu waliyasafisha na kukabiliana nayo.

Mtu ambaye ataiangalia historia ya manabii na historia ya Uislam kwa ujumla na historia ya maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w), Maimam watoharifu (a.s), na masahaba wake ataona ya kwamba, hawa ndio watu wa kwanza kuingia katika uwanja, na Mtume (s.a.w.w), alikuwa wa kwanza toka pale alipokabidhiwa kazi ya kufikisha ujumbe wake mpaka wakati akiwa yupo kitandani amelala alipofikwa na umauti. Lakini, baina ya umauti wake na kupewa kwake utume alikuwa ana harakati nyingi ambazo ni vita, kulinda umma na kadhalika.

Hali kadhalika, ukiyaangalia maisha ya Amirul Muuminin Ali Bin Abi Twalib (a.s), yalikuwa ni vivyo hivyo tu, kujitolea katika njia ya Allah (s.w.t), kujitolea katika hukumu za Allah (s.w.t) na Maimam wote walikuwa ni katika hali hiyo hiyo.

Leo hii tupo katika vita vya haki na dhulma, vita vya ufakiri na kukinai (*ghanaa*), vita vya udhoofishaji na *istikbar*.

Mimi nawaunga mkono nyote wapendwa duniani ambao kwamba mnapambana na kujitolea katika njia ya Allah (s.w.t) na Waislam wote ni watukufu mbele yangu, nawabusu na kuwatumia salamu zilizojaa *ikhlaas*, na kwa taifa tukufu la Iran, napenda kubainisha kuwa; kwa baraka za Allah (s.w.t) athari za kiroho zishamiri duniani kote, nyoyo na macho yenu yaweze kujizuia na yaliyoharamishwa.

SEHEMU YA PILI

SIFA ZA UISLAM SAFI

SURA YA KWANZA

UISLAM NI DINI YA SIASA

Uislam ni mchanganyiko na siasa

Uislam si kwa ibada tu, au kujifunza ibada tu na mengi yanayofanana na hayo, bali Uislam ni siasa pia. Uislam haupo mbali na siasa. Uislam ndiyo muasisi mkuu wa uongozi na ndiyo uliokuja kuyaweka vizuri masuala yote yanayohusu mamlaka. Uislam ni mfumo wa utawala na mfumo wa kisiasa, lakini, kivuli cha mifumo hii tuliyonayo imekithiri zaidi kwa kughafilika wakati Uislam haujaghafilika na kitu chohote kile, yaani, Uislam umekuja ili kumlea mwanadamu kwenye kila nyanja.

Tokea mwanzo wa Uislam siasa ilikuwepo. Siasa ilikuwa ni kwa ajili ya maisha ya duniani. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alinyoosha mikono kuelekea ulimwenguni na ulimwengu ukalingania Uislam na Uislam ukalingania siasa na hatimaye ukaanzishwa uongozi na ukhalifa ambao ulikuwepo tangu mwanzo wa Uislam. Tangu zama za Mtume wa Allah (s.w.t) hadi wakati Uislam ulipokuwa bado haujapotoshwa, dini na siasa vilikuwa sanjari.

Siasa si upotofu, ni ukweli. Siasa ni kitu chenye kuongoza nchi na si cha kupotosha na kudanganya nchi, kuyafanya haya yote ni makosa makubwa, Uislam asili yake ni siasa, na wala si upotofu wala udanganyifu kama wanavyofikiria.

Ni lazima tubainishe kuwa siasa ni kwa ajili ya wanazuoni na ni haki kwa ajili ya Mitume na Mawalii wa Allah (s.w.t).

Iwapo itatokea kwamba mtu mmoja ataanzisha siasa iliyo sahihi (chama), na si ya kishetani, halafu ikaongoza nchi kwa dola ya ki-siasa iliyo sahihi, chama chenyeye kuongozwa na rais wa Jamhuri kwa kheri na usalama na kwa kupatikana taifa salama, basi siasa kama hii ni siasa iliyokuwepo kwa ajili ya Mitume, Mawalii na sasa kwa ajili ya maulamaa wa Kiislam.

Siasa kama hii ndiyo anayohitaji mwanadamu na jamii kwa ujumla, ndiyo yenye kuongoza taifa kwenye njia sahihi, hii ndiyo siasa iliyomo ndani ya Uislam na ndiyo iliyothibiti kwa ajili ya Mitume na Mawalii wa Allah (s.w.t).

Siasa iliyomo Ndani ya Qur'ani na Hadithi

Wito wa Qur'ani ulikuja katika mji wa Makka na pia katika mji mtukufu wa Madina. Wito huu haukumhusu mtu maalum au baina ya mtu na Allah (s.w.t) tu, haikuwa hivyo, bali, wito huu ulihu hata katika mambo ya mtu binafsi, mahusiano ya watu na Allah (s.w.t), jamii na siasa.

Katika Uislam, Qur'ani imehifadhiwa na hakuna hata neno moja lililobadilishwa. Qur'ani ni mjumuiko wa kila kitu; mambo ya kiroho, kimaada (kidunia), ya dhahiri na ya kificho.

Qur'ani pia imekuja ili kumjenga mwanadamu kwenye mawanda yote na kwa kila atakalolihitaji kwa maisha yake binafsi, ya jamii, mahusiano yake na Muumba wake (Tawhid), sifa Zake zinazomstahiki, mambo yanayohusu kiyama, siasa na jamii kwa ujumla.

Viongozi wa dini na siasa

Mtume Mtukufu (s.a.w.w), alikuwa ni mhimili mkuu wa siasa na dini. Mtume (s.a.w.w) ndiye muasisi wa mambo ya uongozi, alianzisha vituo vya siasa na ukhalifa (uongozi) katika Uislam.

Suala la uongozi lilikuwepo tangu wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w.w) na siasa ilikuwepo. Pia, katika zama za Amirul Muuminin (a.s), uongozi ulikuwepo na siasa pia ilikuwepo. Kama ambavyo lilinakiliwa tukio kubwa lilitokea katika siku ya *Ghadiir Khum*, ili-kuwa ni kutufahamisha na kutuelimisha kwamba nasi ni lazima tutilie mkazo suala zima la uongozi,

Iwapo mtakaa na kutafakari dhana ya dini katika utamaduni wa Kiislam, mtaona kwamba hakuna utata wowote uliopo baina ya kiongozi wa kidini na wa kisiasa. Mtaona pia kwamba, harakati, mapambano, wadhifa na wajibu uliopo katika dini hali kadhalika ni hivyo hivyo katika siasa. Kuongoza ni moja katika nyadhifa na majukumu yaliyokuwapo katika dini na saisa.

Hata ukiangalia maisha ya kiongozi mkubwa wa Kiislam, Mtume (s.a.w.w) na maisha ya Imam Ali (a.s), utaona kwamba walikuwa ni viongozi wetu wa dini na wa siasa pia. Jambo hili lipo wazi kwenye utamaduni wa *Shia Ithna'ashariyyah*, ni mambo yaliyo wazi na muhimu kwa kila Muislam mwenye kuyafuata madhehebu haya na ni wadhifa wa kila kiongozi wa kidini afahamu suala hili kwamba mwisho wa yote ni lazima siasa na jamii iingizwe moja kwa moja katika masuala yote ya uongozi, na kuongoza ni jukumu lake na ni lazima alitekeleze.

Uhusiano wa hukumu na ibada pamoja na siasa

Uislam ni dini ya *Tawhiid*, ni dini iliyovunja ushirikina, ukafiri, ibada ya masanamu, na pia ubinafsi. Dini ni *fitra* na sehemu ya kupambana

na vikwazo mbalimbali, kati ya mja, wasiwasi wa shetani, jinni, na watu kwa dhahiri na kwa kificho.

Siasa ya dini ni kuongoza katika njia iliyonyooka, njia isiyofungamana na mashariki wala magharibi. Ni dini ambayo yenyekulingga na siasa, na siasa yake ni ibada. Uislam si dini ambayo yenyekuwa upande wa jambo moja tu, Uislam upo katika kila kitu. Katika Uislam kuna hukumu, kuna masuala yanayohusiana na dunia na namna ya kuishi, kuna siasa, kuna masuala yanayohusu jamii, na uchumi kwa ujumla.

Qur'ani tukufu ambayo ipo mikononi mwa Waislam, tangu ili vyoshuka kwa mara ya kwanza hadi hivi sasa, hakuna neno hata moja, wala herufi moja iliyozidi wala kupungua. Pindi unapoishuhudia Qur'ani, utaona ya kwamba, hakukuwa na masuala ya wito tu kwa ajili ya watu ili wakae tu nyumbani na wamtaje Allah wao tu, bali, ilikuja na wito kwa ajili ya masuala ya kijamii, kisiasa, uongozi na ukayaangalia haya yote kuwa ni moja katika ibada, na kumuabudu Allah (s.w.t) inatokana na siasa na maslahi ya kijamii.

Katika Uislam shughuli zote ambazo zinakwenda sambamba na Dini hiyo ni moja katika vipengele vya ibada. Hata kufanya kazi katika kiwanda, kulima, kufundisha na kulea, yote hayo ni nishani na maslahi ya Uislam.

Ni tumaini letu kwamba Waislam wote watakuja kufanya kama ambavyo Allah (s.w.t) alivyowaamuru na kufanya kazi masuala yote yanayohusiana na siasa na ibada kama ipasavyo na sio kukaa tu na kusubiri swala, ingawa ibada ya swala ndilo jambo la kumweka mja karibu na mola wake zaidi na hakuna kilicho bora zaidi ya jambo hili, lakini kinachotakiwa hapa ni kwamba, mja baada ya kuswali, baada ya mikutano ya ibada, basi pia ni muhimu aende akautumikie Uislam, na ibada ya Hijja katika kipindi hicho ndicho kinadhihirisha zaidi masuala ya kijamii na kisiasa.

Katika kumwelekea Allah (s.w.t), sio lazima mtu akae kwenye kipembe cha ukuta na aseme kuwa; “Mimi nilikuwa namwelekea Allah (s.w.t)”. Hapana, kumwelekea Allah (s.w.t), ndio maisha ya Manabii hasa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Maimamu wetu Maa-sumiin (a.s) ambao walikuwa katika mwenendo huu. Lakini, pindi wanapohitajika kwenda katika vita basi walitoka na kupambana kisawasawa, na pia waliongoza. Kila kitu ukifanyacho ni kumwelekea Allah (s.w.t). Haikuwa hivyo, kwani hata Imam Mtukufu alikuwa akijishughulisha mchana kutwa na kisha alifanya ibada zake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema:

**“Dhoruba ya Ali siku ya Khandaq ni bora kuliko ibada...
Thaqlaini” (Kitabu: *Munaaqib*, Juz. 3, uk. 163)**

Kuna baadhi ya hukumu za kiibada zilizopo katika Uislam, asili yake ni kuitumikia jamii na siasa, zinahamasisha shughuli za kijamii na kisiasa. Mfano, swala za jamaa, swala za Ijumaa, kujumuika katika ibada ya Hijja, zote hizi ni msingi wa kiroho na zenye kuathiri *akhalaq* na *aqida* na pia huathiri mno masuala ya kisiasa.

Uislam umeleta mijumuiko kama hii ili iweze kutumika katika dini katika kukuza udugu na ushirikiano, kubadilishana mawazo, kutatua matatizo ya kisiasa na kijamii yanayozikabili jamii zetu kwa ujumla.

HIJA NA SIASA

Ukweli kuhusu Hijja

Ni uchungu mkubwa ulioje unaokabili jamii za Kiislamu kuwa hadi sasa falsafa halisi kutokana na hukumu hii ya Allah (s.w.t) kuhusiana na ibada hii kuu ya Hijja na fadhila iliyopo katika ibada hii bado hai-

jaeleweka! Hadi sasa imebaki kuwa ni ibada iliyokauka, isiyopiga hatua na isiyoleta matunda yoyote.

Moja katika nyadhifa kubwa ambazo Waislamu tunatakiwa kujua ni ukweli kwamba je, Hijja ni kitu gani, kwa nini siku zote huwa tunajiandalia uwezo wa kimada na kiroho kwa ajili ya kuanzisha safari kuelekea huko?

Hijja ni kwa ajili ya kujiweka karibu kwa Mwenyezi Mungu, na Hijja si kufunga safari na kufanya amali zinazotakiwa kule tu, au kufanya safari iliyokauka (isiyokuwa na faida) kwa maneno na kutumia muda tu, safari kama hii haitomfikisha mtu kwa Allah (s.w.t). Hijja ni kituo cha kumjua Allah Mtukufu ambapo ndani yake kuanapatikana siasa ya Uislam na maisha kwa ujumla.

Katika faradhi za Hijja ambazo ni kwamba, kusema *Labaik!* kwa haki, yaani nimekuitika na kufanya Hijra kuelekea kwa Allah wa haki na kwa baraka za Ibrahim (a.s) na Mtume Muhammad (s.a.w.w) ambao ndio waliovunja masanamu na mashetani wote. Na ni yupi katika mashetani wakubwa kama Marekani aliyeumeza ulimwengu na Urusi ambaye ni mwillingiaji mkubwa na ni yupi shetani katika mashetani wakuu wa zama hizi?

Pindi Waislam wanapokwenda Hijja, basi iwe ni Hijja iliyokuwa hai, iwe ni Hijja yenye kulaani uhalifu wa Urusi na Marekani, iwe ni Hijja yenye kukubalika. Iwapo tutaenda kule bila ya kufikiria maslahi ya Waislam wengine kutohana na uhalifu unaofanywa dhidi ya Waislam, basi Hijja hii haitokuwa na maana yoyote ile.

Kwanini serikali za Kiislam ambazo zina idadi ya watu takriban mamilioni na wana hazina za mafuta katika ardhi zao ambayo ndio uti wa mgongo wa maisha yao, badala ya kutumia mafunzo yato-kanayo na Qur'ani Tukufu na amri tukufu ya Mtume wetu (s.a.w.w) ambayo inatuita kushikamana pamoja na kamba ya Allah (s.w.t) na

tuache mifarakano na ikhitilafu tulizokuwa nazo, kwani Haram hizi Tukufu (Makka na Madina) ni agizo la Mtume wa Allah (s.w.t), na ilikuwa ni kituo cha ibada na siasa za Kiislam, na iliendelea kuwa hivyo hata baada ya kufariki kwake ambapo sasa mchakato na mipango ya kisiasa na kiibada inaanza kuporomoka, zenyewe zime-nyamaza kimya? Na yeote atakayeonekana anajaribu kuingilia kati masuala ya kisiasa na kijamii ambayo ni masuala muhimu kwa Waislam basi ataonekana amefanya dhambi kubwa mno katika Haram tukufu na atauwawa.

Mimi sielewi maimamu na viongozi wa swala za jamaa katika Haram hizi tukufu wamejifunza nini katika Uislam na kuhiji katika nyumba ya Allah (s.w.t)! wanalichukulia kuwa ni jambo lililokuja kichwa kichwa tu, na wanajidanganya kuwa watu kusimama dhi-di ya kutokomeza dhulma na ukandamizaji ni masuala ya kisiasa, wanafahamu nini kwamba mahujaji wanaokuja kuzuru Haram hizo tukufu wanakuja kwa jina la Uislam, ambamo ndani yake ni mwigilio na masuala ya kisiasa na wito wa kimataifa ni kuwa dhidi ya Israel na Marekani ambao ndio maadui wakubwa wa Uislam na wako kinyume na sira ya Bwana Mtume (s.a.w.w).

Wito wa kujitoa

Kutangaza kujitoa katika ushirikina ni moja ya nguzo ya *tawhid* na ni wajibu wa kisiasa katika ibada ya Hijja. Ni lazima siku za Hijja kufanya maandamano kwa heshima na utukufu, na kwa kadri tut-akavyokuwa wengi ndiyo bora zaidi. Maandamano yafanyike kwa ushirikiano wa mahujaji wa Kiiran na wasio Wairan, na wapaze juu sauti zao ili kujitoa kabisa kutoka kwa washirikina na wote wafanyakao dhulma ulimwenguni humu ambao kiongozi wao mkuu ni Marekani!

Leo hii, kujitoa kwetu huko na kupiga mayowe yetu dhidi ya makafiri ni kwa ajili ya dhuulma na uonevu unaofanyika katika nchi za mashariki na maangamizi yanayofanywa na Marekani kwa ku-vamia nyumba zao, kuchukua rasilimali zao, kuwatoa katika ardhi yao na kupora rasilimali walizokuwa nazo. Hiki ndicho kilio chetu, na kilio kwa taifa linalodhulumiwa la Afghanistan.

Kilio chetu pia ni kwa ajili ya ndugu zetu Waislam Waafrika kwa uhalifu na ubaguzi wanaofanyiwa.

Kilio chetu vile vile ni kwa ajili ya watu wa Lebanon na Palestina na mataifa yote yanayokaliwa kwa mabavu na Marekani na Israili.

Kilio chetu ni kulinda na kutetea heshima na utukufu tuliokuwa nao, kulinda utajiri na rasilimali tulizokuwa nazo. Kilio chetu ni juu ya machungu wayapatayo ndugu zetu wa mataifa mengine ambayo yapo katika adhabu ya ufakiri na njaa ambayo imesababishwa na uvamizi waliofanyiwa ndugu zetu wa Iraq, kwa taabu wazipatazo na umwagaji damu wa asubuhi na jioni. Hii ni dhamana iliyochukuliwa na Umoja wa Mataifa kwa kutetea haki za watu duniani! (Lakini waapi!)

Jukumu la kisiasa la misikiti

Mwanzoni mwa Uislam msikiti na *mimbar* ilikuwa ikitumika kwa ajili ya harakati za kisiasa na maandalizi; na shughuli mbalimbali katika Uislam zilikuwa zikipangwa katika msikiti.

Msikiti ulikuwa ni kituo na sehemu maalum kwa ajili ya kuanzia shughuli zote za tabligh na harakati zote za Uislam na mapambano ya kuukandamiza ukafiri. Ninyi ambaeo ni watu wa msikiti na maulamaa wa misikiti, ni lazima muwe wafauasi wa Mtume wa Uislam na maswahaba zake. Na misikiti iwe ni kwa kuulingania Uislam na harakati zake na kwa ajili ya kukataza aina zote za

shirki na ukafiri na kuungana na wanaoonewa ili kukabiliana na madhalimu.

Wakristo msifikiri kwamba msikiti katika Uislamu ni kama kanisa. Wanapomaliza kuswali, Waislam hupata fursa ya kugawiana majukumu. Vita vyote vilivyopiganwa katika enzi hizo msingi wake mkuu ulipangwa msikitini.

Mambo ya uongozi katika dini ya Kiislamu yalifanyikia msikitini, na kwa msingi huo tangu zama za Mtume wa Allah (s.a.w.w) hadi kipindi cha makhalifa, msikiti ulikuwa ni kituo cha kisiasa na Uislam. Hata katika swala za Ijumaa, khutba itolewayo ilikuwa ni hutba inayohusiana na masuala ya kisiasa na Uislam kwa ujumla.

Huzuni na siasa

Tukio la Karbala pekee ni suala la kisiasa, hivyo ni lazima lihuishwe na kamwe halitobadilika. Msiba uliotokea Karbala ni lazima ubainishwe kwa watu wote.

Bwana wa Mashahidi kwa mtazamo wa riwaya na wa akida yetu ni kwamba tangu pale alipoanza harakati akitokea Madina, alijua kuwa yeye ni shahidi. Kabla ya kuzaliwa kwake ilishatolewa habari. Wakati alipokuwa akitoka Makka na namna alivyotoka ilionyesha sura ya harakati ya kisiasa na kila hatua moja aliyoipitia ilionyesha kuwa ni ya kisiasa iliyokuwa na mtazamo wa Kiislam.

Hadi sasa ambapo katika mwezi wa Muharram bado wahanga wa Karbala na jeshi la Kiislam hukumbukwa. Mashekhe wakubwa, wahadhiri wa masaibu ya Karbala na wafuasi wa Sayyidush Shuhadaa (a.s) bado wanatumia fursa walivyopewa na Allah (s.w.t) kuhakikisha kuwa wanakata miti na kuing'oa mizizi yote ya dhulma ili kuuangusha utawala wa kishetani wa Yazidi bin Muawiyah bin Abu Sufiyani na hila zake.

Majilisi (vikao) hizi kubwa zitumike kuhamasisha uhuru, kulishinda jeshi linalopambana baina ya akili dhidi ya ujinga, uadili-fu dhidi ya dhulma, amana dhidi ya usaliti (khiyana), na serikali ya Kiislamu dhidi ya utawala wa kishetani. **Majilisi hizi zihuishwe kwa utukufu wote na kuinua juu bendera ya damu ya Ashura iwe ni alama ya kulipiza kisasi kwa siku ya anayedhulumiwa na dhalimu.**

Wahadhiri wa masaibu ya Karbala na taifa lote kwa ujumla ni wajibu wao kuilinda na kuihuisha shahada ya Imam Husein (a.s) na waifanye iwe ni moja ya mila za Uislam kwani kuilinda kwake ni kuulinda Uislam kama alivyosema Mtume (s.a.w.w) kuwa:

“..... من حسين”

“..... Mimi natokana na Husein” (Rejea: Arshaad uk. 249, Kashfu al-Ghammah, Juz. 2, uk. 175)

Hii ina maana kwamba Husein anatokana na mimi na mimi pia nimekuwa hai kutokana na Husein. Na hizi zote ni baraka za shahada yake Imam Husein (a.s) kwani maadui walitaka kuuondoa Uislam na athari zake. Walikuwa wanataka ukoo wa Bani Hashim usiwepo kabisa, kuiangamiza kabisa asili ya Uislam na kuanzisha utawala wa Kiarabu. Na hii ilikuwa ni kazi yao ambayo ni sababu iliyowafanya Waarabu, Waajemi na Waislam wote wazingatie kwamba kadhia hii si kadhia ya Waarabu, Waajemi na Wafursi tu bali ni kadhia inayomhusu Allah (s.w.t) na Uislam kwa ujumla. Hivyo, hifadhini majilisi hizi na majilisi zote ambazo zitaleta urafiki wa kidini na umoja wa Kiislam, zote hizi tuzihifadhi na tuzihuishe katika nyoyo zetu.

SURA YA PILI

UTAWALA WA KIISLAMU

SHARTI LA KUUTAMBUA UISLAMU SAFI

Umuhimu wa utawala wa Kiislamu

Utawala adilifu ni siasa, ni utawala uliojaa maana ya kisiasa. Hii ni siasa ambayo Allah (s.w.t) amemwamrisha Mtume wake (s.a.w.w) **kumwainisha** Amirul Muumimiin (a.s). Hivyo, utaona kwamba Mtume (s.a.w.w) **alikuwa na siasa**. Utawala bila ya siasa ni kitu kisichowezekana na hili lilithibitika katika siku ya *Ghadiir Khum*.

Mtume wa Allah (s.a.w.w) kwa miaka mingi alipata nafasi ya kuendeleza utawala wa kisiasa, kusimamisha uadilifu kwa kila mtu na kila kitu kilisimama kwenye misingi ya uadilifu, katika kipindi ambacho wanaokasirika hawakuweza kukasirika tena, katika mazingira ambayo hayawezi kuwakasirisha watu wa kisufi (irfanî) kuueneza usufi wao, wanafalsafa kwa falsafa yao na mafaqihî kwa fiqhî yao.

Lakini, wakati uliposimamishwa utawala wa Allah (s.w.t) tu ambaao ni uadilifu, na ulipoenea, ndipo wafuasi na wapenda haki waliopata fursa ya kuyafikia malengo yao yalipopatikana mazingira tulivu kwa kila kitu. Hivyo, hapakutangazwa tangazo lolote la mfano kama huo wa kuwatangazia watu kwende kwenye utawala ambaao si mwingine zaidi ya ule wa siasa.

Lazima uanzishwe utawala unaofuata sira ya Mitume na Mawali

Kwa utukufu wa akili na dharura ya kuwepo dini, malengo ya kuja Mitume (amani za Allah ziwe juu yao), kazi zao na kubainisha hukumu zao si masuala pekee ya kuzungumzia tu, si hivyo, bali ni masuala yaliyokuja kutokana na wahyi kupitia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) nao ukaendelea kwa Mtukufu Amirul Muuminin Ali Bin Abi Twalib (a.s) hadi kwa Maimamu (a.s), ambao Allah (s.w.t) amewateua ili waweze kufikisha na kubainisha hukumu za Allah (s.w.t) kwa watu wote bila ya kufanya khiyana, nao pia amana hiyo wakakabidhi kwa mafuqaha (maulamaa) ili wawafikishie watu ujumbe wa Manabii.

”الفَقَاءُ امْنَاءُ الرَّسُولِ“

”Mafuqaha (maulamaa) ni wawakilishi (warithi) wa Mitume.“

Maulamaa ni lazima wasimamie amani. Ukweli huu ni wadhifa muhimu sana kwa Mitume waliokabidhiwa ili waweze kuanzisha mfumo wa haki, wenye uadilifu katika jamii na ndiyo njia ya kusimamisha kanuni na hukumu za Allah (s.w.t), kubainisha, kueneza mafundisho na akida (imani) ya Allah (s.w.t) kama ilivyobainishaaya tukufu isemayo:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا إِلَيْنَا وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ
وَالْمِيزَانَ لِيَقُوْمَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ.....

”Kwa hakika tuliwapelekea mitume kwa dalili waziwazi na tukakiteremsha Kitabu na mizani pamoja nao ili watu wasimame kwa uadilifu“. (*Suuratul Hadid*, aya ya 25)

Hivyo, sababu ya kuletwa Mitume kwa ujumla ni kwamba waw-aongoze watu kwa haki, kwa uadilifu, na kutoa mafunzo yatakay-owafikisha katika ukamilifu kwa kuanzisha utawala na kueneza hu-kumu za Allah (s.w.t)

Allah (s.w.t) amemfanya Mtume Muhammad (s.a.w.w) awe ki-ongozi wa watu na pia ameamrisha utiifu wetu kwake kuwa wajibu kwa kila mmoja wetu, kama alivyosema kuwa:

أطِيعُ اللَّهَ وَأطِيعُوا أَسْوَلَ وَأَوْلَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ

“Mtiini Allah na mtiini Mtume wake na wenyе mamlaka katika nyinyi....” (Sura ya An Nisaa, aya ya 59)

Si suala la kusema kwamba jambo hili limesemwa na Mtume (s.a.w.w) basi ukalikubali bali ulifanyie kazi, ulifanye kwa hukumu na kumtii Allah (s.w.t). Ibada na isiyokuwa ibada inayohusiana na hukumu basi huko ni kumtii Allah (s.w.t)

Kumfuata Mtume (s.a.w.w) si kutenda kwa kufuata hukumu tu, hili ni jambo jingine kabisa, bali kumtii Mtume ni kumtii Allah (s.w.t) kwa sababu Allah (s.w.t) ndiye aliyeamrisha kumtii Mtume wake.

Kama tulivyosema hapo awali, Mitume wamekuja kufanya kazi za kiroho na kuwaongoza katika mambo ya kidunia. Iwapo Mi-tume, Mawalii na viongozi wakuu wa kidini wakiyakana hayo, basi watakuwa wamejikusanya uovu ambao natija yake ni kuupeleka umma wa Kiislam katika njia ya ovyo, kufungua mlango kwa ajili ya ukoloni na umwagaji damu.

Hivyo, hata ukiangalia maisha ya Mitume wote kuanzia Mtume Adamu (a.s) hadi kwa Mtume wetu wa mwisho Mtukufu Mtume

(s.a.w.w) na Maimamu Watukufu utaona kuwa kila mmoja aliweza kuonesha njia hii ya uadilifu na kutufahamisha maana ya utawala uliokuwa bora.

Sisi pia tuna wadhifa kwa ajili ya taifa letu. Kama tunataka taifa liwe dhaifu basi twendeni msikitini tuswali tu, na tusome dua tu. Je huu ndio wadhifa wetu, twende msikitini tuswali na tusome dua tu, au tuamke? Hivyo basi jukumu letu sisi sote ni kufanya yale yote ambayo yatatushnikiza katika njia ya Uislam na hivi ndivyo walivyofanya viongozi wetu.

Ni lazima tuwaambie wajinga jinsi Qur'an tukufu na Sunna za Mtume ilivyoelezea masuala ya utawala, hukumu, na siasa ambapo hajjaweza kupatikana popote pale, bali hukumu nyingi za Kiislam ni za kiibada na za kisiasa, kughafirika nazo ni msiba mkubwa. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alianzisha utawala kama ambavyo watawala wen-gine wanatawala ulimwengu, lakini ye ye alifungamana na jamii yenye uadilifu, na hivi ndivyo alivyotawala Imam Ali bin Abu Twalib (a.s).

Umuhimu wa kuanzisha utawala kwa mtazamo wa habari na hukumu

Kulingana na dharura iliyopo akilini, hukumu za Kiislam, faragha ya Mtume (s.a.w.w), Imam Ali (a.s), vifungu vyaya na hadithi utaona kwamba kuanzisha serikali na utawala ni jambo la lazima katika Uislam.

Pamoja na kifungu hicho utaona kwamba ni moja ya sababu na dalili za kuwapo kwa kiongozi ili kusimamisha nidhamu na kanuni (sheria), na kama hukuweza kuchagua mtumishi mwaminifu, mlinzi na mtunza amana basi dini itaangukia katika mateso makali, kanuni zote zitaangamia, mapokeo na hukumu za Kiislam zitapinduliwa na kurejea kama mwanzo ilivyokuwa.

Uhalisi na ubora wa kuwapo kwa sheria za Kiislam

Dalili nyingine ya kuwapo kwa ulazima wa kuanzisha utawala ni, “**Uhalisi na ubora wa kuwapo kwa sheria za Kiislam**,” hukumu na hakimu (jaji).

Uhalisi na ubora wa sheria hizi katika kuanzisha serikali kwa ajili ya kuongoza kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii ni:

Mosi

Ni sheria yenye kanuni na utaratibu mbalimbali ulio na nidhamu moja ya kijamii. Nidhamu hii ni haki ambayo kila mtu anaihitaji; namna ya kuishi na jirani, watoto, jamaa zako wa karibu, raia wen-zako, maisha yako binafsi, ya mke na mume, hata taratibu na kanuni za kupigana vita, suluhi, umoja wa mataifa, wahalifu, biashara, sa-naa na kilimo.

Uislam umeweka nidhamu hata kwa maisha ya mtu binafsi. Namna mtu atakavyoishi katika jamii inayomzunguka na kutoa miongozo yake kama namna ya kufunga ndoa, kanuni zake, kula kwake, kuvaan kwake, kipindi cha mama anavyotakiwa awe anaponyesha mtoto na wadhifa gani, namna ya mama kulea mtoto, na mahusiano kati ya mke na mume.

Hivyo, Uislam haukumwacha mwanadamu aishi tu ili mradi ameishi, bali imemwekea miongozo maalum ya kumfikisha katika ukamilifu wa kibinaadamu. Ni wazi kwamba, Uislam ni utawala wenyewe mahusiano ya karibu kabisa na siasa katika jamii, inayofanya juhudji katika mafunzo hatimaye kufikia katika masharti ya utoaji huduma kwa binaadamu ili awe mtu mwema.

Qur’ani tukufu na Sunna imejumuisha sheria na hukumu zote ambazo zinatoa mwongozo, furaha na ukamilifu ambao kila mwanadamu anauhitaji. Mahitaji yote ya mwanadamu yamebainishwa

ndani ya kitabu, yaani Qur'ani na Sunna. Wala hakikuachwa kitu chochote na kila mwanadamu ataishi kulingana na riwaya hizo.

Pili

Kwa kuzingatia kwa makini maumbile na ubora wa kuwa na sheria, tutaona kwamba, kuyasimamisha haya na kuyafanyia kazi italazimika kuwa na utawala na uongozi. Bila ya kuanzishwa chombo kimoja kikubwa, kamwe hatutaweza kuzifanyia kazi fursa ambazo Allah ametuamrisha tuzifanye.

Tubainishe baadhi ya masuala ambayo ni lazima kuyafahamu:

1. Hukumu za Mali

Mali na bajeti iliyokadiriwa katika Uislam siyo tu itumike kwa ajili ya maskini na msaada kwa mafukara, bali ni kwa ajili ya kuanzisha utawala na itumike kwa matumizi muhimu na ya dharura ya Taifa.

Mfano: *Khums* (1/5) ni moja ya pato kubwa linaloingia kwenye *Baytul maal*, yaani mali ya Waislam, na ni moja ya rasilimali inayowingia kwenye bajeti ya taifa.

Kulingana na madhehebu yetu (*Shia Ithna'ashariyyah*), faida zote zinazopatikana kwenye kilimo, biashara, rasilimali za ardhini, za juu ya ardhni, mapato na maslahi yote yanayopatikana kwa uadili-fu kama uuzaaji wa majani, shughuli za meli, au uchimbaji madini, kimoja kimoja kinaingia katika *khums*. Yaani, kile kibakiacho baada ya kutoa gharama zote alizozitumia, kwa hukumu ya Kiislam, kuna pesa kidogo ambazo zitaingia katika mfuko wa *baitul maal*.

Ni wazi kwamba, pato hili ni kubwa sana kwa kuongoza nchi ya Kiislam na linatatua mahitaji yote yanayohusiana na mali. Ikiwa pato la *khums* linalopatikana katika nchi za Kiislam, au dunia nzima

na zikawa katika nidhamu ya Kiislam basi ni dhahiri kwamba pesa hizo hazitakuwa ni kwa ajili ya kutatua mahitaji ya *masharifu* na *mashekhe* tu bali ni kwa kila jambo ambalo ni muhimu katika nchi.

Iwapo utawala wa Kiislam utafanya utafiti katika mali hizi hizi tulizokuwa nazo, yaani *khums* na zaka na zile zipatikanazo kutokana na fidia, na kodi, basi zitatumika kwa ajili ya kusaidia nchi na taifa kwa ujumla.

2. Hukumu za ulinzi wa Taifa

Kwa upande mwingine, kuhusiana na hukumu ni kuhifadhi nidhamu ya Kiislam na kulinda ardhi na uhuru wa nchi na Uislam kwa ujumla. Ni lazima kuwe na uongozi. Mfano wa hukumu hiyo ni hii katika aya tukufu isemayo:

وَأَعِدُّوا لَكُم مَا اسْتَطَعْتُم مِنْ قُوَّةٍ وَ مِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ

“Na waandalieni nguvu muwezavyo, na kwa farasi waliofungwa (kwa maandalizi)” (*Anfaal*, Aya ya 60.)

Laiti Waislam wangeliifanyia kazi hukumu hii kwa kuanzisha utawala wa Kiislam, kamwe Mayahudi na washirika wake wasinge-likuwa na nguvu ya kuanzisha vita na kufanya uharibifu katika ardhi za Waislamu wala *Masjidul Aqsa* kufanyiwa uharibifu.

3. Hukumu ya haki na hukumu ya kihalifu

Hukumu ni nyingi sana kama vile kulipa fedha za damu iliyomwagika (*diye*) ambayo ni lazima ichukuliwe na irejeshwe kwa wamiliki wake, au visasi ambavyo ni lazima zitekelezwe kwa hukumu za Kiislam, bila ya kuanzisha serikali ya Kiislam, kamwe hatutoweza kufikia katika haki. Kanuni zote hizi bila ya kuwapo kwa nguvu ya serikali kamwe hatutaweza kuyafikia masuala haya muhimu.

Sunna na desturi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w)

Sunna na desturi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ni hoja muhimu katika kuanzisha serikali, kwa sababu mbili:

Moja

Kuanzisha serikali kama ambavyo historia inavyothibitisha kwamba alianzisha serikali na kutekeleza mfumo wa Kiislam na kuiongoza jamii. Alitumwa kwa ajili ya ulimwengu wote, kuhukumu na kutuma mabalozi kwa ajili ya kuonana na viongozi wa makabila mbalimbali na wafalme ili kuwalingania, kufunga nao mikataba, kuongoza vita na kusimamia hukumu alizokuja nazo.

Pili

Kwa ajili ya kuanzisha utawala baada yake kwa amri ya Allah (s.w.t), kwa ajili ya kuongoza umma **mara baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w)** na kuchagua kiongozi ina maana kwamba, uongozi baada ya Mtume (s.a.w.w) pia ni muhimu, ndiyo maana Mtume (s.a.w.w) aliacha wosia wake kwa amri ya Allah, Allah (s.w.t), akatangaza kuwa uongozi ni jambo la msingi na la lazima.

Desturi ya Amirul Muuminiina Ali bin Abi Twalib (a.s)

Baada ya kifo cha Mtume Mtukufu (s.a.w.w) hakukuwa na Muislam hata mmoja aliyekuwa na shaka juu ya ulazima wa kuwapo kwa uongozi baada ya Mtume. Hakuna hata mmoja aliyesema kuwa hatuhitajii uongozi, kwa sababu, hakuna hata mmoja aliyesikika akisema lolote juu ya hilo. Watu wote walikuwa wakifahamu umuhimu wa kuwapo kwa uongozi, bali tofauti iliyokuwapo ni ile ya nani ambaye amepewa jukumu hilo la kuongoza dola hiyo ya Kiislam.

Hivyo, baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na katika kipindi cha ukhalifa Amirul Muuminiin Ali bin Abi Twalib (a.s) pia kulikuwa na uongozi, kulikuwa na vyombo vyaa serikali ambavyo vilichukua nafasi ya uongozi.

Umuhimu wa mwendelezo wa hukumu

Ni wazi kwamba umuhimu wa kuendesha hukumu na kuasisi masuala ya uongozi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ni ulazima wa kipekee, wenye muda na haukuwa kwa ajili ya wakati wa Mtume pekee tu, bali uliendelea hadi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

Kulingana na aya tukufu, hukumu za Kiislam kwa uchache haziangalii muda na sehemu, bali zitaendelea kubaki milele. Hukumu za Kiislam lazima zitekelezwe, hazikuja kwa ajili ya kipindi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w) tu bali hadi watakaozaliwa baada yake pia wataendeleza kanuni hizo hizo na Uislam utaendelea kulinda ardhi na umma wa Kiislam.

Hivyo, umuhimu wa sheria na hukumu kama ilivyokuwa katika kipindi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w), kipindi cha Amirul Muuminiin (a.s) na hata baada yao utaendelea kubaki hadi kufikia zama zetu na kuendelea. Yaani, ni lazima uwepo uongozi na namna ya kuongoza idara zake.

SIFA ZA HUKUMU ZA KIISLAM

Haki (uadilifu) ya kijamii

Mitume wa Allah (amani za Allah ziwe juu yao) wametumwa kwa ajili ya kuwahudumia viumbe wa Allah (s.w.t) kiroho, kuwaongoza

kutoka katika dhulma (giza), kuwapeleka katika nuru na kusimamisha uadilifu wa mtu mmoja mmoja na wa kijamii.

Kulingana na utaratibu wa Kiislam, Uislam una maana mbili na njia mbili ambazo ni; kulinda na kukuza roho (*maanawiyah*) za watu na kusimanisha uadilifu na kuwaokoa kutoka katika mikono ya dhulma. Hivyo, Uislam umekuja kwa sababu hizo kuu mbili na wanaoufuata Uislam lazima wazilinde sababu hizo na kanuni zake kwa ujumla.

Kazi moja ya Jamhuri ya Kiislam ni kulinda na kusambaza uhuru wa nchi na watu wake, kupambana na ufisadi, ukahaba, kutunga na kurekebisha sheria, kuleta maendeleo katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni kwa kuzingatia misingi ya Kiislam, kwa maslahi ya kimsingi ya watu wote.

Hukumu za Kiislam ni zile zilizokuwapo tangu mwanzo mwa Uislam na ndizo ambazo leo hii sisi tunatakiwa kuzitumia katika utawala wetu. Uislam kamwe hautokuwa radhi hata kwa kumkosea mwanamke wa Kiyahudi ambaye yupo katika ulinzi wa Uislam.

Katika Uislam hakuna ubora baina ya tajiri na asiye tajiri, mweusi na mweupe, Sunni na Shia, Mwarabu na Mwajemi, Mturuki na asiye Mturuki na watu mbalimbali, wote hawa hakuna hata mbora baina yao. Qur'ani Tukufu imebainisha kwamba ubora upo katika uadilifu na *taqwa* (yaani ucha Mungu). Mtu mwenye *taqwa*, mwenye roho safi ndiye mbora, lakini si katika mali wala kwa mwenye nacho, ni lazima ubora baina ya watu tuuweke kando na tuone kwamba watu wote ni sawa na kila mmoja amepewa haki sawa.

Kutawala kwa sheria za Allah (s.w.t)

Utawala wa Kiislam ni utawala wa sheria na kanuni. Katika aina hii ya utawala, utawala wa sheria na utaratibu wa kipekee ni wa Allah

(s.w.t). Sheria za Kiislam pamoja na amri ni za Allah (s.w.t) juu ya kila mtu, kila utawala na dola zote za Kiislam. Watu wote wanafuata sheria na kanuni alizokuja nazo Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na viongozi waliofuatia baada yake. Sheria zote zimetoka kwa Allah Mtukufu (s.w.t) kama zilivyoshuka na kubainishwa katika Qur'ani Tukufu na kusikika kupitia katika ulimi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

Hivyo basi, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alihukumu kwa sheria na aliifuata na sheria ndio iliyomchagua Amirul Muuminin Ali bin Abi Twalib (a.s) kuwa khalifa baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w), sio eti kwa sababu alikuwa mkwe wake bali alikuwa amechaguliwa kwa amri ya Allah (s.w.t).

Utarwala wa Kiislam si kama aina nyingine zozote za tawala zilizopo, si uongozi wa dikteta aliyechaguliwa kwa kura zenu, kuchezza, kuvamia mapato, mali na uhai wa watu, kila mmoja kujichukulia madaraka na mali, kuua anavyotaka, kutaka malipo na kutoa na kutumia mali ya taifa atakavyo. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Amirul Muuminiin (a.s) na makhalifa wengine hawakuwa na mammaka kama haya. Uislam ni dini ya sheria. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) hakuweza kwenda kinyume cha sheria wala hakufanya kitu kama hicho. Allah (s.w.t) alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwamba iwapo utasema neno lolote kinyume nitaikata shingo yako.

Hukumu ni sheria, kinyume na sheria za Allah (s.w.t) basi mtu hawezি kuongoza, na hakuna uongozi wa mtu yeoyote, si faqih na wala asiyé fakihi, wote hawa wapo chini ya sheria na wazifanyie kazi.

Sifa za msimamizi (kiongozi) wa mfumo wa Kiislam

Elimu na uadilifu

Masharti ambayo kwamba ni lazima kwa mtawala kupaswa kuwa nayo ni asili ya moja kwa moja katika uongozi wa Kiislam. Baada ya

sharti la umma kama akili na hekima basi kuna masharti ya msingi mawili, nayo ni:

1. Ujuzi wa sheria.

2. Uadilifu.

1. Kwa kuwa uongozi wa Kiislam ni sheria basi ujuzi wa sheria hizo ni lazima na muhimu kwa kila mtawala. Kama ilivyokuja katika hadithi, na hii si kwa ajili ya kiongozi tu, bali hata kwa watu wengine, kila shughuli au wadhifa au cheo fulani ni lazima lipatikane sharti hili la ujuzi wa sheria. Maimam wetu wame-lithibitisha hili kwa ajili ya Uimam wao kuwa Imam ni lazima awe ni neema kwa ajili ya wengine. Kwa mtazamo wa Waislam, sheria na uadilifu ni sharti na nguzo ya msingi katika Uislam.
2. Kiongozi lazima afungamane na imani, akhlaq, uadilifu na ajitenge na kila aina ya uchafu. Mtu anay- etaka kuwa kiongozi lazima atekeleze kanuni na sheria za Kiislam, asimamie mali za Waislam kwa kila kitakachoingia na kutoka na Allah (s.w.t) amempa jukumu la kusimamia na kuongoza waja wake, hivyo, lazima asiwe mfanya madhambi. Allah (s.w.t) amesema kuwa:

قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ

“Ahadi yangu haitowafikia madhalimu”
(Suuratul-Baqarah, Aya ya 124)

Kuheshimu haki za watu

Viongozi popote walipo, katika kila nchi, dola na serikali ya kila nchi lazima watambue kwamba kukififikia cheo kama hiki ni mtihani wa Allah na ni mtihani ulio mzito sana kwao. Lazima wafikirie kwamba kabla ya kupata cheo hiki hapo mwanzo walikuwa vipi na baada ya cheo wapo vipi, hali zao zikoje, je kuna tofauti yoyote?

Katika Jamhuri ya Kiislam, watawala hawapaswi kutumia vyeo walivyo navyo kwa mtu kujilimbikizia utajiri kwa ajili yake binafsi au maisha yake ya kila siku yawe ya hali ya juu na bora zaidi kwa ajili yake. Ni lazima vigezo vya Kiislam katika kila jamii na kuwa makini na heshima katika kila ngazi vifuatwe.

Ukiyaangalia maisha ya Bwana Mtume (s.a.w.w) utaona ya kwamba hadi pale anafariki hakuwa na chochote alichojoivekea kwa ajili yake, na hivi ndivyo alivyotuusia. Pia, ukimsoma Amirul Muuminin Ali bin Abi Twalib (a.s) na Bibi Fatma (s.a) binti wa Mtume (s.a.w.w) utaona walikuwa wanamiliki ngozi moja tu ambayo usiku walikuwa wakiitumia kulalia, mchana waliitumia ngozi hiyo hiyo kuwekea nyasi za ngamia wao ili wale majani. Hiki ni kitanda na pia sehemu ya kulishia ya mtu kama kiongozi aliyekuwa akichapa kazi kutwa na si kwa ajili ya kulimbikiza mali bali alikuwa akitoa wakfu kwa ajili ya Waislam.

Serikali ya Kiislam si kama ya kifalme. Uislam ni tofauti na utawala wa kifalme, kisultani na wa ki-Kaisari (*imparaturi*), ambao athari yake ipo katika mahekulu makubwa, amali (vitendo) yenye kuonekana, ofisi maalum, na mengine mengi yaliyo muhimu kwa mfalme. Lakini maisha ya Bwana Mtume (s.a.w.w) aliyekuwa ndiyе rais wa dola ya Kiislam, jinsi alivyokuwa akitawala kila mmoja alishuhudia. Utawala huo uliendelea hata baada yake na kabla ya utawala wa bani Umaiyyah.

Sisi tunataka tuwe na serikali moja ya uadilifu, yenyewe uwiano na inayopenda watu, iliyio na imani kwamba iwapo mimi nitakula mkate mkavu isije ikawa kuna mtu mmoja katika utawala wangu akabakia ngozi tu kwa njaa.

Katika utawala wa Kiislam, mtu wa kwanza ni khalifa wa Waislam ambaye maisha yake yatakuwa ya kawaida baina ya watu walio mafukara na wenye maisha ya chini kabisa.

Mtu wa kwanza katika Uislam ni yule ambaye utawala wake si wa kujionyesha, usioonesha tofauti, bali katika kutumia mali za kidunia, yeeye awe chini kabisa

Mafuqaha ni viongozi wa jamii

Maimamu na mafuqaha wana wajibu mkubwa wa kuanzisha na kuedeleza mfumo wa utawala mzuri wa Kiislam kwa kusimamia sheria za Allah (s.w.t) na uadilifu utakaowanufaisha watu kwa huduma yao. Matumizi ya serikali yasiwe kwa ajili yao, mateso na taabu si chochote kwao bali ni kutekeleza majukumu yao. Wafahamu kuwa madhumuni ya *wilayat faqih* (uongozi wa wanazuoni - mafaqihu) ni kutekeleza majukumu ya Utume.

Hadithi zote zinazopatikana katika elimu ya maarifa ni fadhila ya ulimwengu huu, zipo mikononi mwa mwanazuoni mwadilifu na bora zaidi ni juu ya kuwaongoza na kuwaonya watu. Yote haya ni moja ya mchakato unaojionyesha katika Uislam kwa ajili ya kuanzisha utawala wa Kiislam, kwa watu walio katika mikono ya ukandamizaji, kuharibu nyumba ya dhlulma, kufungua milango katika nyumba za wanazuoni kwa ajili ya watu - wanazuoni ambao ni waadilifu, hodari, mujahidina, wanaosimamisha nidhamu na sheria ya Kiislam katika jamii.

Khalifa na mtawala kwanza kabisa lazima azitambue sheria za Kiislam, yaani awe mjuzi wa sheria, awe mwadilifu - kuanzia uka-

milifu wa imani na maadili mema - na akili pia ina ulazima wake - kwa sababu uongozi katika Uislam ni uongozi wa sheria, si kichwa chako wala si uongozi wa mtu binafsi kwa watu. Iwapo mtawala hajui mambo ya sheria basi ni wazi kuwa hakuna uongozi.

Haki ya kuchagua kiongozi Mwanazuoni

Ikiwa mtu ana uwezo na ana tabia hizi mbili, yaani kusimamisha na kuadhimisha utawala ambao ndiyo aliopewa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) katika masuala ya kuongoza jamii basi ni dira muhimu na ni lazima watu wote kumtii.

Maono yaliyokabidhiwa kwa uongozi wa Mtume (s.a.w.w) ni zaidi ya aliyokuwa nayo Amirul Muuniniin Ali Bin Abi Twalib (a.s). Bila ya kuwa mwanazuoni, basi itakuwa ni batili na kosa. Lakini fadhila za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ni nyingi zaidi ya viumbwe wote ulimwenguni. Aliyefuatia baada yake kwa fadhila zaidi ya wengine ni Amirul Muuniniin Ali Bin Abi Twalib (a.s). Lakini, wingi wa fadhila za kiroho hautaongezeka katika uchaguzi wa kiongozi.

Uchaguzi huo huo na uongozi ambao Mtume (s.a.w.w) na Maimam wengine (amani ya Allah ziwe juu yao) katika utoaji na uhamasishaji wa jeshi, kuchagua kiongozi, magavana, kuchukua mali na kuzitumia kwa maslahi ya Waislam, hivyo ndivyo Allah (s.w.t) alivyochagua uongozi.

Umuhimu wa kuingia kwenye siasa

Ile kusema kwamba dini imetengana na siasa ni maneno yasiyokuwa na nafasi katika Uislam. Shughuli za kisiasa ni moja ya wadhifa wa Waislam katika dini.

Kauli yetu ni hii kwamba, si shekhe peke yake, bali watu wote ni lazima waingie katika siasa. Siasa si kitu cha urithi kama ambavyo

ilivyo mali ya nchi, mali ya bunge au mali ya mtu fulani bali siasa maana yake ni hali na kila kitu ambacho kinapita katika nchi, hes-hima ya uongozi, watu wote kuwa haki katika nchi hiyo.

SURA YA TATU

UISLAMU NI DINI YA MAPAMBANO

MAPAMBANO NA MSUGUANO DHIDI YA UKOLONI

Uislam ni dini, njia na chanzo cha kuifikia haki. Hakuna dini am-bayo imejisalimisha na kuwa chini ya walioathirika na nguvu yoyote isiyo ya kweli, ambayo haikupoteza motisha wowote wala faida kwa ajili ya nchi yake, kulinda uhuru wake na watumishi wen-gine wa Mungu kutokana na khofu na uchoyo wowote, kuepukana na ubinafsi wenye fikra fupi ambazo ndizo chanzo cha taabu na matatizo isipokuwa Uislam.

Taifa la Iran ni Waislam na wanautaka Uislam. Uislam ni kim-bilio na kivuli cha uhuru na ukombozi, unatokomeza walowezi, una-ondoa misingi ya ukandamizaji, rushwa (ufisadi), unaokata mikono ya usaliti na vitendo vya jinai.

Mimi nasema kwa kujamini kwamba Uislam hautakaa katika ardhi za mabeberu. Uislam ni kikwazo kikubwa ndani na nje ya maeneo yake, moja baada ya jingine, huondosha kila aina ya ugumu na hatimaye Uislam utashinda duniani.

Ni lazima kwa nguvu zote tusonge mbele na kwa juhud zote. Tupambane na wale wote ambao wanautaka kutunyanyasa na kutuin-gilia. Tutambue kuwa kuishi maisha ya udhalili, chini ya mabawa, ni bora binadamu akubali kufa mara elfu na hiyo itakuwa ni heshima kwake.

Mimi kwa ujasiri ninautangazia ulimwengu kuwa, iwapo wa koloni wanataka kusimama dhidi ya dini yetu na sisi pia tutasimama tukabiliane na dunia nzima hadi pale tutakapo wasambaratisha wote na kamwe hatutakuwa chini ya miguu yao.

Na kamwe hatutawaacha katika ardhii. Hatutakuwa na sulhu yoyote kwa kupambana na udhalimu, kiburi na wanyanyasaji. Watan-gazieni kauli mbiu hii kuwa:

“Kuweni rafiki pamoja na marafiki wa Allah (s.w.t) na kuweni adui na maadui wa Allah (s.w.t).”

- Nafasi ya mapambano (mwamko) katika Uislam.

Msimamo kwa ajili ya Allah (s.w.t) ili kuikomesha dhulma

Allah (s.w.t) amesema kumwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kuwa:

قُلْ إِنَّمَا أَعِظُّكُمْ بِوَاحِدَةٍ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مَتَّنِي وَ
فُرَدَاءِ

“Sema, Mimi nakunasihi tu kwa jambo kuwa; msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili wawili na mmoja mmoja”

Huu ni ufumbuzi na mawaihda ambayo Allah (s.w.t) **akimuadhi** Mjumbe wake Mtukufu ambapo nami pia ninawaambia kwamba kuweni na msimamo na simameni kwa ajili ya Allah (s.w.t), hata kama uko peke yako, mkiwa wengi, simameni kwa ajili ya Allah (s.w.t) kwa kukabiliana na *twaghuti* (shetani), dhulma na dhaalim kama ambavyo ametuamrisha Allah (s.w.t) kwa kusema kuwa:

قِيَامُ اللَّهِ

“Kisimamo cha Allah”.

Ukirejea historia za Mitume utaona kwamba zimetusimulia waziwazi jinsi ambavyo Mitume walivyokabiliana na nguvu mbali mbali. Mtume Ibrahim (a.s) alisimama akiwa peke yake bila hata ya kuwa na woga kwa kukabiliana na wanaoabudu masanamu, akafanikiwa kuvunja masanamu yote isipokuwa moja kubwa aliloliacha kama ushahidi, alipoulizwa akasema aulizwe yule aliyebacki.

Mwamko na kusimama kwa mara ya pili ilikuwa kwa Nabii Musa (a.s) alipokabiliana na Firauni na wachawi wake akiwa na fimbo tu.

Mtukufu Mtume wetu (s.a.w.w) kwanza aliamrishwa asimame peke yake. Aliamrishwa kuwa:

فَمَنْ فَانَذِرَ

“Simama na kisha waite watu”

Mwaliko (wito) wa kwanza ulianzia kwa Mtume mwenyewe, siku hiyo ndiyo alitangaza Unabii. Walikuwa ni kijana mmoja na mwanamke mmoja ndiyo waliomkubali na kuamini, lakini alikuwa na *istiqama* (msimamo) ambayo kila kiongozi (nabii) anatakiwa kuwa nayo.

فَاسْتَقِمْ كَمَا أُمِرْتُ

“Simama na kuwa na msimamo”

Hivyo sifa hizi mbili zenyé malengo makubwa ndizo alizokuwa nazo Mtume wa Waislam, alizitanguliza ili kuuendeleza Uislamu.

Msimamo kwa walioonewa ni njia pekee ya haki kwa ajili yao

Maisha tunayoishi katika zama zetu ni maisha yaliyotekwa na mataifa ya kidhalimu, yaliyofungamana na mikono ya uhalifu ambapo wengi wao wapo karibu na desturi za zama za tawala zilizokuwepo hapo nyuma, isipokuwa tu katika zama hizo kulikuwa na sheria za misituni na hakukuwa na utawala.

Sisi tupo katika zama ambazo wahalifu badala ya kuwa ni watifufu na wanaokubali, sifa na wenye kuwa na kibali, tupo katika zama za mauaji, ambapo mashirika ya kimataifa kama ambavyo yanajulikana kuwa ni ya haki za binaadamu, yapo kwa ajili ya manufaa ya madhalimu, mahaini na wameshikamana na wanaowatetea waovu.

Wote mnaodhoofishwa na mnaoonewa simameni! Lazima mchukue haki zenu kwa nguvu zote, miji na nchi zote, wala msisubiri wao wawape haki zenu, kwani wao hawako tayari kutoa haki ya mtu.

Mataifa yote lazima yainuke. Iwapo mtakaa tu na mkisubiri mtu mwingine aje kwa ajili yenu, iwe kwa masuala ya kidunia au kiroho haya ni makosa makubwa. Hii ndiyo itayosababisha msiweze kufanya lolote, hali itaendelea kubaki hivyo hivyo hadi kufikia watoto wenu pia wakajenga tabia hiyo. Kama mtakuwa makini juu ya Allah (s.w.t) na juu ya Uislam, basi Allah Mtukufu (s.w.t) atawafungulia njia.

Wito wa kuwa katika Mapambano

Wito kwa Waislamu kupambana na ubeberu duniani

Enyi mliodhoofishwa duniani! Simameni, jiokoeni kutokana na makucha ya mateso. Enyi Waislam! Amkeni toka kwenye usingizi wa kughafilika, simameni muutetee Uislam na nchi za Kiislam kutoka kwenye mikono ya wakoloni na walowezi.

Kaka zangu na dada zangu wapendwa kutoka katika kila nchi na popote mlipo! Lindeni hadhi ya Uislam na taifa lenu kwa ujumla. Msiwe na khofu kwenye kukabiliana na maadui zenu, yaani Marekani, Mazayuni wa kimataifa na walowezi wa mashariki na magharibi. Bila ya kupoteza muda wowote, teteeni mataifa yenu na nchi za Kiislam, watokomezeni maadui na madhalimu wa Uislam.

Leo hii, kibla cha kwanza cha Waislam kipo mikononi mwa Israili, na hii ni saratani iliyoenea katika eneo hili. Leo ndugu zetu wapenzi wa Palestina na Lebanon, kwa nguvu zote wanakatwa katwa na kugaragazwa kwenye damu na udongo. Leo hii Israeli wana-fanya uovu kwa njia yoyote ile.

Leo hii, Waislam waliopo katika nchi za Afrika wanapaza sauti ya vilio vyao juu kwa kadri ya uwezo wao juu ya uonevu wanay-ofanyiwa. Falsafa ya Hijja yapaswa kukidhi haja ya kilio hiki cha wanaoonewa. Mzunguko wote katika Nyumba ya Allah (s.w.t) uonyeshe kuwa hakuna mwingine isipokuwa Allah (s.w.t), kwa kuweka ahadi na Allah (s.w.t) hadi pale mtakaporushia mawe urafiki wa mashetani na mabepari ili waweze kukimbia katika nchi tukufu za Kiislam.

Leo, ulimwengu wa Kiislam umeangukia katika mikono na tabu za Marekani. Nyinyi mtoke na kuzunguka katika mabara yote duniani kuwafikishia Waislamu wa huko ujumbe wa Allah (s.w.t) ambao utamfanya mtu asiwe mtumwa kwa mwingine isipokuwa Allah (s.w.t) na mtumishi wa mtu yoyote yule.

Matumaini ni kwamba, mataifa yote yanayodhoofishwa duniani, hususan mataifa ya Kiislam kwa kuungana pamoja kwenye mapambano ni dira. Baada ya uamuzi huu, utakuwa ni mwongozo na umoja kamili wa kutatua migogoro na tofauti zao katika kukabiliana na kufru, shirki, mamlaka ya kikoloni, kupambana dhidi ya mfalme wao

hasa beberu la Kimarekani na kukata mizizi yake ili kujifungulia milango ya ukombozi sahihi kwa ajili ya nchi zao.

Wito kwa Waislam Kusimama ili kurejesha Utukufu wa Uislam

Enyi Waislam duniani! Ilikuaje pale mwanzo wa Uislam kwa idadi ndogo mliweza kushinda nguvu kubwa ya maadui na mkawea kutengeneza umma mkubwa wa Kiislam, lakini sasa kwa jamii il-
iyo na idadi inayofikia watu bilioni moja, iliyo na jeshi kubwa kwa
kukabiliana na adui, lakini, ni jinsi gani mlivyo dhaifu? Je, mna-
jua kwamba masikitiko yote na huzuni mliyo nayo ipo kwenye
mgawanyiko na khitilafu baina ya wakuu wa nchi zenu na nyinyi
wenyewe? Amkeni, shikeni Qur'ani Tukufu mikononi mwenu, re-
jeeni maamrisho ya Allah (s.w.t) na rejesheni utukufu wa dini tukufu
ya Kiislam.

Wito kwa mapambano dhidi ya Israili

Baada ya kukamilisha hukumu tukufu za Kiislam hakuna amri yoy-
ote nyingine iliyokuwa ya wajibu kwa Waislam ambayo, sijui vipi,
mtu anatakiwa aulinde Uislam, iwe kwa kujitolea maisha na mali
yake katika njia tukufu ya hazina yake kwa kuutetea Uislam wake.

Wakati mnapoona damu zisizokuwa na hatia yoyote zikim-
wagika, za ndugu zetu waliopo kwenye ardhi tukufu ya Palestina,
wakati mnaposhuhudia ardhi zetu zikifanyiwa uhalifu na kuharibiwa
kwa jinai za Mazayuni, kwa mtazamo huu, hakuna njia yoyote ile
isipokuwa ni kuendeleza jihadi tukufu. Jihadi tukufu ni wajibu kwa
kila Muislam kwa kutoa misaada ya hali na mali na Allah (s.w.t)
atakuwa nyuma na mlinzi katika njia hii.

Mimi nina mpango wa kusisitiza kupatikana uhuru kutoka kwa
Israel, kutambuliwa kwake na Waislam ni janga kwa serikali za Kiis-

lam, mnajua kwamba ni mlipuko kufanya upinzani dhidi yake, na ni moja ya faradhi kubwa kwa Uislam. Namuomba Allah (s.w.t) aliye Mkuu, kwamba majukumu haya yaliyopo mikononi mwa Waislam ayaonyeshe kwa Uislam

Siku ya Quds ni ya Uislam na ni ya uhuru kwa Palestina

Siku ya Quds ni moja ya siku ulimwenguni, siyo tu kwa kuwa ni siku maalum kwa ajili ya kuwapo kwake Quds, bali ni siku ya wanaoone-wa katika kukabiliana na walowezi, ni siku ya mataifa ambayo yapo kwenye shinikizo la dhulma za Marekani, washirika wake, ni siku ya kukabiliana na wakoloni, siku ambayo wanaodhoofishwa wote pamoja na kudai na kukabiliana na walowezi hao ni lazima kuwaangamiza.

Siku ya Quds si siku ya Palestina tu bali pia ni siku ya Uislam. Ni siku ya utawala wa Kiislam. Siku ambayo Jamhuri ya Kiislam duniani lazima ipandishe bendera juu kutangaza kushindwa kwa wakoloni, kamwe hawataweza kuutawala Uislam.

Siku ya Quds ni siku inayokaribiana na usiku wa Qadri ambapo Waislam lazima wakeshe. Iwe ni chanzo cha kuamka, kuwatangazia wote walioghofirika katika giza la ukoloni, unafiki duniani na Waislam wote ulimwenguni waunge nguvu ya pamoja na kwa msingi imara. Katika usiku huo wa Qadr Waislam wakeshe kwa dua na maombi kutokana na vikwazo vya utumwa, kutoabudiwa asiyekuwa Allah na kuwa huru kwa kumwabudu Allah (s.w.t). Kwamba, siku hiyo ya Quds huenda sanjari na siku za mwezi mtukufu wa Allah (s.w.t).

Ni vyema Waislam wote duniani wajinasue kutokana na vikwazo na kifungo cha utumwa, shetani mkubwa, na kujikomboa kutokana na ukoloni na kuwa na uwezo na nguvu ya kumwomba Allah (s.w.t)

asiwajaalie kuwa mikononi mwa wahalifu na kukata mizizi ya uonevuu kwenye nchi za waliodhoofishwa.

Wito kwa Maulamaa wa Kiislam kujiunga kwenye Mapambano

Ni jukumu la maulamaa waliopo kwenye nchi za Kiislam kujihusisha kutatua matatizo ya Waislam kwa nguvu ya pamoja. Wajadili, washauriane na wabadilishane mawazo ili wahifadhi manufaa ya Waislam kwa kukabiliana katika kuzuia uvamizi wa tamaduni za mashariki na magharibi. Wahakikishe wanaangamiza kizazi na mataifa yanayosababisha hatari kwa watu na Uislam kwa ujumla. Wakabiliane na mapambo yatokayo nchi za mashariki na magharibi yanayoleta athari mbaya kwa watu, wauelezee ukoloni mpya na ushetani wake, kwamba hivi ni vita vya kuchora katika ulimwengu wa Kiislam .

Je kuna ugumu wowote kwa maulamaa wa nchi za Kiislam kulifanya hilo hali ya kuwa kuna Qur'ani tukufu, sheria za Kiislam, Sunna ya Mtume (s.a.w.w) na mafundisho sahihi ya Maimamu Watukufu (a.s)?

Wito kwa Maulamaa wa kikristo kujiunga kwenye Mapambano

Mwenyeezi Mungu Mtukufu anasema kuwa:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُنُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ
وَ لَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَءُ أُنَقْئٍ عَلَى أَلَا تَعْدِلُوا اَعْدِلُوا
هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ وَ اتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا
تَعْمَلُونَ

“Enyi mlionamini! Kuweni wasimamizi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtoe ushahidi kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanya uadilifu, fanyeni uadilifu, huko ndiko kunakomkurubisha mtu na ucha Mungu, na mcheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda.” (Surat Maidah: 8)

“Kheri yao ambao wenyenjaa na kiu lakini ni waadilifu...”

(Injili Mathayo, sura ya 5, kifungu cha 6.)

“Kheri yao ambaoni wenyenjolea (*quotient*) katika uadilifu, ambayo ndio sababu ya kuwawekea mamlaka ya mbinguni.” (Injili Mathayo, sura ya 5, kifungu cha 10.)

Enyi makasisi wa makanisa na wafuasi wa Hazrat Isa (a.s)! Amkeni! wateteeni, waokoeni wote wanaodhulumiwa na wanaoonewa duniani waondokane na makucha ya shida, makucha ya uonevu na kwa ridhaa ya Allah (s.w.t), fuateni sheria na desturi za Hazrat Isa (a.s). Mahekalu yenu yawe ni moja ya idara kwa manufaa ya wanaodhulumiwa, inueni sauti moja na kumtuhumu dhalimu.

Kheri yao wale walio na njaa na kiu ya haki na wenyenjolea zahama au kuuawa kwa ajili ya kusimamisha haki. Na ole wao wanaokwenda kinyume na sheria na desturi za Isa Masihi (Yesu) na za Mitume wote, ambao hutaabika kwa manufaa ya wanaodhulumu, majasusi na wanaokanyaga haki za mataifa.

Ewe taifa la Masihi na wafuasi wa Isa *Ruhullah!* Amkeni, lindeni utukufu wa Isa Masihi na taifa lake. Msiruhusu maadui kuchafua mafundisho ya kiungu, kuleta upinzani katika maamrisha ya Allah (s.w.t), na kumtangaza vibaya Isa Masihi kuwa ni taifa lenye kudhulumiwa duniani.

Kupambana na Uonevu na Ukosefu wa Maelewano

Uislam Kupambana dhidi ya Udhalimu na Uonevu

Sheria za Kiislam zinasema kwamba usidhulumu na wala usiwe chini ya dhulma. Neno *Inzlam* lina maana kuwa chini ya mzigoto wa kudhulumiwa na kukandamizwa. *Inzlam* ni kujidhulumu mwenyewe, kudhulumu taifa moja. Dhulma pia ni kiunzi. Kila شیوه ni Haramu katika Uislam. Wewe huna haki ya kumdhulumu mtu, na mtu hana haki ya kukuvutia kwenye dhulma.

Sisi tunachotaka kwa watu wote, Waislam na wasio Waislam, wote kwa pamoja, kuwa na amani na utulivu. Lakini, hatuna maana kwamba iwapo mtu mmoja akavamia nyumba ya mwingine na kufanya kosa basi sisi tutasema kuwa ni amani na kuwapa toni ya uonevu, hapana. Kama vile ilivyokuwa dhulma ni Haram, basi usijidhulumu.

Taifa la Kiislamu fuaneni dini ambayo ratiba yake inakuwa ni mukhtasari wa maneno mawili:

لَا تَظْلِمُونَ وَ لَا تُنْظَلُمُنَّ

“Usidhulumu na wala usikubali kudhulumiwa”

Sisi na mataifa ya kidhalim, iwe wametufanyia sisi dhulma au iwe wamewadhulumu ndugu zetu Waislam, basi tutakuwa na uadui nao.

Mantiki ya Uislam ni hii kwamba, utawala haupaswi uwe juu yako, na wala haupaswi wewe uwe chini ya mtawala.

Kupambana na uonevu (dhulma) ni kazi ya ki-Ungu

Wakoloni wamekuwa na kazi ya kuingiza siasa zao na kuingiza mifumo ya dhulma kwenye masuala ya kiuchumi na kuleta athari ya migawanyiko ya watu katika sehemu kuu mbili:

1. Dhalim na
2. Anayedhulumiwa

Upande mmoja, kuna sauti za milioni ya Waislam wenyewe njaa, walionyimwa afya na utamaduni, na upande mwingine watu wachache kati ya watu ni matajiri na wanamiliki nguvu za kisiasa na wapo katika duru la ujisadi.

Wenye njaa na wakosefu wa afya wanajitahidi wenyewe ili wajinasue kutoka katika dhulma za watawala wanyang'anyi, wapate maisha yaliyo bora na juhud hizi ni za kuendelea na za kudumu. Lakini, wanapata pingamizi kubwa. Ni jukumu letu sisi tuwaokoe watu waliodhulumiwa.

Sisi tunalo jukumu la kuwasaidia wanaodhulumiwa na kuwa na uadui na madhalim. Jukumu hili ndilo ambalo Amirul Muuminiina (a.s) alisema katika wosia wake kuwaambia watoto wake wawili, kwa kusema:

وَكُونَا لِلظَّالِمِ خَصْمًا، وَلِلْمَظْلُومِ عَوْنًا.

“Na kuweni mahasimu kwa madhalimu na wasaidizi kwa mwenye kudhulumiwa.” (Nahjul-Balaghah, uk. 977, barua ya 47.)

Maulamaa na wasomi wa dini mnao wajibu wa kupambana na matumizi Haramu na aina yoyote ya dhulma. Msiache idadi kubwa ya watu wenye njaa wawe karibu na watesi wao na wanyang'anyi ili wapate baraka (neema) kutoka kwa walao Haram.

Amirul Muuminiin (a.s) anasema kuwa:

"Mimi utawala nimeukubali kwa sababu hizi, kwamba Allah Mtukufu amechukua ahadi kutoka kwa maulamaa wa Kiislam amewalaz-

imu katika kukabiliana na ulafi, ukandamizaji na kutokukaa kimya dhidi ya dhuluma na unyang'anyi."

Ni muhimu kwamba sisi tutekeleze majukumu yetu ambayo ni kukabiliana, kupambana na kuwa na upinzani kwa kila aina ya dhulma. Iwapo tutafanikiwa kuitokomeza hali hii, itakuwa ni bora zaidi. Na ikiwa tutashindwa, basi ni wajibu wetu kuyatekeleza majukumu yetu haya kwa vitendo. Tusiwe na khofu kulifanya hili. Lazima tujue kwamba, kwanza, hatutashindwa, kwani Allah (s.w.t) yupo nasi. Pili, tuchukulie kwamba tutashindwa kihali, basi hatutashindwa kimaadili, yaani kiroho. Na ushindi wa kiroho ni wa Uislam na Waislam.

KUKEMEA UKIMYA DHIDI YA UKANDAMIZAJI

Ukimya wa Wasomi wa Kiislam

Shauku ya wasomi wa Kiislam ni kupenda nchi na sheria za Kiislam. Tumeamrishwa na Allah Mtukufu kuhifadhi nchi ya Kiislam na kutafuta uhuru wake. Hivyo, kuacha kutoa nasaha au kukaa kimya katika kukabiliana na hatari zinazojitokeza mbele yetu kwa ajili ya Uislam na nchi ni dhambi kubwa mno. Hii ni kukaribisha kifo cheusi.

Kiongozi wetu mkuu, Hazrat Amirul Muuminiin (a.s), haku-ruhusu kukaa kimya katika kukabiliana na dhulma. Sisi pia ni lazima tulifahamu hilo. Wajibu wetu ni kuongoza umma, taifa, na jamii kwa ujumla na kamwe hatuwezi kujizuia kufanya hivi kwani ndivyo alivyotaka Allah (s.w.t). Katika zama hizi, kukaa kimya katika kukabiliana na dhulma ni kuidhamini dhulma.

Allah (s.w.t) anasema ndani ya Qur'ani Tukufu, Suratul Al – Maida, aya ya 63 kuwa:

اَذْ يَقُولُ لَوْ لَا يَنْهَا هُمُ الرَّبّانِيُّونَ وَالْأَحْبَارُ عَنْ
 قَوْلِهِمُ الْاثْمِ وَأَكْلِهِمُ السُّحْتَ، لَبِئْسَ مَا كَانُوا
 يَصْنَعُونَ

**“Mbona watawa (wao) na wanazuoni (wao) hawawakatazi maneno
 yao ya dhambi na ulaji wao wa Haramu? Bila shaka wayatendyo ni
 mabaya kabisa.”(5:63)**

Allah Mtukufu katika aya hii (الرَّبّانِيُّونَ وَالْأَحْبَارُ) anakusudia kutoa lawama na kukosoa kwamba, kwa nini wale waliokuwa na maulamaa na wasomi wa dini ya Kiyahudi walisema kudhulumu ni dhambi kubwa zaidi ya kuzua uongo, tuhma, kupotosha ukweli na mfano wa haya kama vile kula haram, lakini hawakuhamisha wala hawakukataza. Mbaya zaidi ni kuwa, hawakuwalaumu wala kuwallaani Mayahudi wenyewe wala maulamaa wao.

Na hii si kwa ajili ya Maulamaa wa Kiyahudi tu, bali pia ulimwengu wa Kiislam wote ukiwajumuisha wanazuoni wote wa dini ulimwenguni wanaofuata sera, siasa, na taratibu za Allah (s.w.t) ziwe za kujitegemea au za kizazi kilichopita. Kwani, hukumu ni moja, haina kusema kuwa ni ya kizazi kilichopita au kijacho. Yote haya tunajifunza kutoka katika Qur’ani Tukufu na ndivyo walivyotufunza maulamaa wetu wa kidini.

Iwapo itatokea *bida ’a* katika Uislam na maulamaa wa dini na wakuu wa madhehebu wakanyamaza, watasababisha ugoigoi katika Uislam na kudhoofisha imani za Waislam. Kwa hivyo basi, ni wajibu juu yao kwa njia yoyote ile inayowezekana wafanye kazi. Kazi yenye iwe ni kukanusha na kutokezeza ufisadi, na iwe ni kazi inayoleta athari au la mradi tu ujumbe ufikishwe.

Jihadi ni Hatua ya Mwisho Kupambana na Dhulma

Uislam na dini nyinginezo ilikuwa ni kichocheo cha kuwaamsha watu. Mafundisho ya mitume yaliwaamsha watu, yaliwahamasisha watu dhidi ya wakoloni na dhidi ya washirikina. Tunaweza kusema kwamba Qur'an ni Kitabu kama cha vita ya uadilifu dhidi ya dhulma. Ni Kitabu chenye kuhamasisha watu kupigania haki na uadilifu. Katika hali kama hii, yote ni kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watu. Lakini Allah (s.w.t) anawaambia kuwa:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ
رُحْمَاءُ بَيْنَهُمْ

“Muhammad Mtume wa Allah na walio pamoja naye ni (wenye nyoyo) imara mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao.” (*Suuratul Fat-hi*, Aya ya 29)

وَقَاتَلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقَاتِلُونَكُمْ كَافَّةً

“Na nyote piganeni na washirikina kama wao wote wanavyopigana nanyi....” (*Surat Tawba* 9:36)

Hivyo, Qur'an imekuja ili kuwaonya na kuwaasa watu, kuwatia moyo kuwa malaika wapo nasi. Pia na Malaika walikuwa pamoja nao, wakiwa wachache au wakiwa wengi walikuwa hawajali. Hata wakiwashindwa zaidi, walikuwa na nguvu ya imani ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Qur'an ndiyo ili wajenga.

Basi, Qur'an ni kitabu cha Allah (s.w.t), ni meza iliyo pana ambayo inatumika kwa kila kitu. Lakini, kila mtu anatumia kwa sura na

mtazamo kuwa ni Kitabu cha Allah (s.w.t) na Mtume wake Mtukufu (s.a.w.w.) kwa ajili ya kueneza maarifa ikiwa pamoja na shughuli mbalimbali ambazo zinapatikana katika Kitabu hiki.

Hii ina maana kwamba kwa ujuzi wa Allah (s.w.t) ni kutoa maana halisi ya maendeleo na vita ilikuwa ni kwa ajili ya hili. Sulhu ilikuwa ni kwa ajili ya uadilifu wa kijamii na haikuwa na maana ya kutaka dunia iwe chini yao na kutaka kuifanya marekebisho tu. Wote wahnahitaji marekebisho.

Hii si dini ya kutengeneza vita, haya ni makosa kabisa ikiwa ni hivyo, mimi pia nafikiria kuwa Hazrat Isa (Yesu) kama wangempa fursa angefanya utaratibu huu huu ambao Hazrat Musa (a.s) ali-fanya na kama ambavyo Hazrat Nuuh (a.s) alifanya kwa ajili ya makafiri.

Watu hawa wanafikiria kuwa Hazrat Isa (a.s) hakuwa na kazi kama hii hata kidogo na alikuwa ni mponyaji tu. Watu hawa walilingiza uharibifu katika Utume wa Hazrat Isa (a.s) na kama ilikuwa ni hivyo, basi alikuwa ni mmoja wa wahadhiri na hakuwa ni Nabii. *Muhadhiri* bila Utume.

Nabii alikuwa na kila kitu: alikuwa na upanga, alikuwa na vita. Nabii alikuwa na sulhu, yaani, vita si kimbilio lake bali ilikuwa ni kwa ajili ya kuleta marekebisho ya maendeleo katika dunia. Wali-kuwa wakipigana vita kwa ajili ya kuwakomboa watu na kwa ajili ya kujikinga na shari mbalimbali.

Mapambano na Upinzani Dhidi ya Uonevu na Dhulma

Mapambano ya Mitume na Uonevu

Salaam zisizo na ukomo ziwe juu ya Mitume *ulul adhim* kwa saba-bu Ibrahim mvunja masanamu, Musa alimwangamiza dhalim, Isa Masihi laiti angepata fursa angekuwa kama wenziwe na Muhammad

aliyeyamaliza masanamu yote na kujitenga kutokana na ushirikina na dhulma.

Na salaam ziwe juu ya Ibrahim, rafiki wa Allah (s.w.t) ambaye alibakiza sanamu moja tu katika masanamu yote ili iwe ni jibu kwa wanaoabudu masanamu na aliyeokoka kutokana na moto, na Musa aliyeongea na Allah (s.w.t) ambaye kwa fimbo ya kuchungia aliweza kuyasitisha maisha ya Firauni.

Na swala na salaamu ziwe juu ya Muhammad, kipenzi cha Allah (s.w.t) aliyesimama peke yake mpaka dakika za mwisho wa mai-sha yake akipambana na dhulma na makafiri kwa kusimamisha vita akiwa na idadi ndogo tu ya watu.

Dini nyingi za Mitume wakubwa waliopita pamoja na dini ya Uislam ni dini kubwa mno zikiwa zina vitabu vyta mbinguni kwa ajili ya uwongofu wa wanadamu, kwa upande mwengine, Ibrahim (a.s) rafiki wa Allah (s.w.t) akiwa amekamata *suhfi* mkononi mwake na mkono mwengine akiwa na shoka kwa ajili ya kuvunja masanamu.

Musa (a.s) alizungumza na Allah (s.w.t), akiwa na *Taurat* mkononi mwake na mkono mwengine ana fimbo, fimbo ambayo ilimuangamiza Firauni na wenzie, fimbo ambayo ilikuwa ni joka, fimbo ambayo iliondosha hiyana.

Mtume wa Uislam, alikuwa ameshikilia Qur'ani mkono mmoja na mkono mwengine ameshikilia upanga, upanga ambao ulikuwa ni kwa ajili ya kuzuia khiyana na Qur'ani kwa ajili ya uongofu, na upanga ulikuwa ni kwa ajili ya kukata vichwa vyta wote waliokuwa wakifanya njama dhidi ya Uislam.

Sababu hizi mbili zilikuwepo toka mwanzoni mwa uumbwaji mpaka sasa, sababu ya kujitolea katika Uislam na kusimama katika kukabiliana na dhulma, uonevu, udikteta, na nguvu za kishetani.

Tangu wakati ule wahyi ulipokuwa ukija kwa Mitume, mojawapo kati ya masuala yake ilikuwa ni ya kiroho, wakati ambapo kulikuwa na upinzani mkubwa toka kwa watu madhalimu, waonevu, wamwaga damu na kila mmoja katika hao alikuwa na njia yake ya kufanya upinzani dhidi ya Mitume. Na sifkirii hata kidogo kuwa pangekuwepo na Mtume yeote yule ambaye alikaa nyumbani kwake tu akisoma dua au akisema hukumu alizokuja nazo, la hasha, haikuwa hivi, bali walizisema hukumu zao na walikuwa wakizifua-tilia na kuzieneza.

Njia ya Maimam ilikuwa ni kushughulikia na kupambana na dhulma

Sayyidush Shuhadaa Imam Husein bin Ali bin Abi Twalib (a.s) ametufundisha kwamba ni lazima tupambane katika kukabiliana na dhulma, uonevu, na utawala wa kijahilia. Tokea pale alipotambua kuwa anatakiwa ashike njia kwa ajili ya shughuli hii, aliona ni muhimu yeye kutoka akiwa pamoja na maswahaba zake, na familia yake akaifidia kama sadaka kwa ajili ya Uislam ingawa alijua fika nini kitamtokea.

Kama harakati hii isingekuwapo, Imam Hussein (a.s) angemkubali Yazid bin Muawiya bin Abu Sufian, ambaye hakuwa na chembe ya imani katika Uislam, hasidi na fasiki, basi Uislam ungeangamia. Imam Husein (a.s) alijitoa muhanga ingawa wenyewe waliona kuwa ameshindwa na wengine kuuwawa, lakini watu walikuja kutambua kuwa ni uhaini kiasi gani na msiba ulioje uliosababishwa na Bani Umaiyyah, zaidi ya hapo, umeendelea kubaki katika historia na imekuwa ni njia ya kupata mafunzo.

Usihofu na idadi, idadi haisaidii kazi kutofanyika, ubora wa idadi, kikubwa ni ubora wa jihadi katika makabiliano, hii ndiyo inayo-

fanya kazi ifanyike. Yawezekana watu wakawa wengi sana, lakini kukawa na mapungufu katika ubora wa kazi au ikawa ovyo kabisa. Na pia yawezekana watu wakawa wachache lakini ubora na uwezo ukapatikana.

Maimam watoharifu (a.s) walipambana ingawa walikuwa ni idadi ndogo ya watu, hadi waliuawa. Maimam (a.s) walisimamisha faradhi, kila mmoja ukimuona hakupambana kwa silaha, walikaa majumbani mwao huku wakifanya tabligh. Huu ndio utaratibu ulio-kuwepo tangu mwanzoni mwa Uislam.

Maimam wetu walitumia umri wao wote kwa kufanya tabligh, kuutangaza Uislam na walikuwa na uwezo wa kufanya jambo lolote lile kwa ajili ya dunia, lakini walikuwa wakijitolea kwa ajili ya Uislam na hawakuweza kupatana na madhalimu.

Ushia ni madhehebu ya mapambano

Tunajivunia kuwa na taifa tukufu lenye kushikamana na Uislam na Qur'ani. Ni fakhari kwamba, tunafuata madhehebu am-bayo yanataka ukweli wa Qur'ani, ambayo kwa kuititia Qur'ani tumekuwa tukihimiza umoja baina ya Waislam na ubinaadamu. Ushia umeokoa makaburi na mabustani kwa kuititia aya tukufu, umeweza kuwaokoa watu kutokana na masharti yaliyokuwa yameteka miguu, mikono, nyoyo na akili zao zikavurugika na watu kuelekea upande wake ili ufungamane na utumwa na wawe watumwa wa shetani.

Na ni fakhari yetu kwamba sisi tunayaafuata madhehebu yaliyoasisiwa na Mtume wa Allah (s.a.w.w) kwa amri ya Allah Mtukufu (s.w.t), na Amirul Muuminiina Ali bin abi Twalib (a.s) aliwaokoa waja katika masharti yote na kuwatoa watu kuondokana na makali yote ya utumwa na majivuno.

Mashekhe ni Washika Bendera wa Mapambano dhidi ya dhulma

Katika kila harakati na mapinduzi katika njia ya Allah (s.w.t), maulamaa wa Kiislam walikuwa ni watu wa kwanza kabisa kuyatoa maisha yao, kumwaga damu zao na kufa wakiwa mashahidi.

Ni mapinduzi yapi ambayo Waislam walitafutwa kutoka katika Hawza (chuo kikuu cha kidini) kwa kengele (bila ya wao wenye we kutoka katika majumba yao) kabla ya kupita mlangoni ili wakajitolee maisha yao matukufu hadi wawe mashahidi?

Kitu kama hiki katika maisha ya mashekhe hakina ukweli woweote. Kuelewana na kujisalimisha katika ukafiri na ushirikina hata kama mja huyo atatenganishwa mifupa yake au vichwa vyetu vifungwe juu ya mlango, au kutumbukizwa ndani ya moto hali ya kuwa ni hai, au mke na watoto wetu kutekwa na kuwekwa kifungoni, hata siku moja hatutaweza kusaini barua ya amani kutoka kwa makafiri na washirikina.

Maana halisi ya kushinda na kushindwa

Sisi ni walinzi wa Uislam na tunaulinda Uislam kwa hali na mali zetu na kamwe hatutakaa. Iwe tushindwe katika masuala ya kidunia au kutufanya tushinde, ushindi uwe nasi, Mtume wa Waislam katika baadhi ya vita alishindwa uwjanjani lakini ushindi ulikuwa ni wake kimalengo. Maadui wa mawalii wa Kiislam pia walikuwa wakwashinda katika baadhi ya vita, lakini ushindi (wa malengo) ulikuwa ni wao. Ushindi upo pamoja na haki, batili ni yenye kutoweka.

Rejea Sura ya Isra aya 81; Allah (s.w.t) anasema:

اَنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقاً

“Hakika uwongo ni wenye kutoweka”

Tarehe 5 Juni ni Siku ya Kuanza Hamasa na Harakati

Tarehe 15 ya mwezi Khordad, sawa na tarehe 5 ya mwezi Juni, sawa na siku ya Ashura, yaani tarehe 10 ya mwezi wa Muharram, ilikuwa ni siku ya huzuni kwa taifa zima linalodhulumiwa, ndiyo siku ya hamasa na ndiyo siku uliyozaliwa Uislam na Waislam upya.

Kila ifikapo siku hii taifa kubwa la Iran huwa kwake ni siku ya Allah (s.w.t), siku yenye kuadhimishwa, ndiyo fakhari kwa taifa kwani ni siku ambayo damu tukufu za watu zilimwagika wakati wakikabiliana na dhulma za Shah Pahlavi.

Katika siku hii, vijana, wakiwamo wanaume kwa wanawake walikuwa kishahidi walipokuwa wakiandamana na kupambana dhidi ya shetani dhalimu Shah na watu wake. Zilimwagika damu zisizokuwa na hatia, na ikulu za dhaalim pia ziliharibiwa. Hii ni ishara kuwa taifa kubwa la Iran lilisimamishwa na watoto wake wapendwa, kupambana ilikuwa njia ya kupatikana amani na furaha kwa ajili ya kizazi chao kijacho.

Sababu ya Uislam kuwa Hai ni Mapinduzi ya Kiislam

Sababu zilizotufanya Iran tusimame ni kutokana na uwezo na matumaini juu ya Allah Mtukufu, kutaka Waislam duniani wawe chini ya bendera ya *tawhiid*, kushikamana na hukumu za Kiislam, kukata mikono ya mabepari kutoka katika nchi za Kiislam, kurejea katika Uislam, kujikomboa, kuwatoa madhalimu katika nchi za Waislam na kuwa huru.

Uislam ulikuwa umeangamizwa. Qur'ani ilikuwa chini ya nyayo zao, ikiharibiwa. Kupambana kwenu vijana wa Iran, kusimama kwenu taifa la Iran kwa ajili ya Allah (s.w.t) ilikuwa ni kuibakiza hai Qur'ani na kuupa uhai mpya Uislam.

Mapinduzi makubwa ya Iran yalikuwa na asili ya kipekee, yali-kuwa na thamani kubwa kiasi kwamba yameleta ukubwa wa hali ya juu katika Uislam na itikadi kwa ujumla. Ni matumaini yetu kwamba Mapinduzi haya yatakuwa ni cheche za Allah (s.w.t) ambazo tunataraji zitakuwa ni mlipuko mkubwa kwa raia wanaokandamizwa na kuchomoza kwa Mapinduzi Matukufu ya Hazrat *Baqiyati llah* (Imam Zaman (a.s)).

Hivyo ni lazima kwa taifa tukufu kama hili na mapinduzi makubwa kama haya, kuendelea kwake na kuwapo kwake kunahitaji bidii zaidi na zaidi ili kusimamisha uadilifu wa Allah (s.w.t).

Mapinduzi ya Kiislam ni matokeo ya kupambana na dhulma

Harakati zenu tukufu katika Uislam, japokuwa kwa damu tukufu za mashahidi na misiba ya waliokuwa wamejitolea nafsi zao, lakini ili-kuwa ni kudai uhuru wenu. Msingi ni kumtoa nje adui wenu na haini mkubwa katika nchi yenu na kumzika katika bustani la historia.

Kupambana kwenu na msimamo wenu kwa nchi zilizodohoofishwa ni kuleta maslahi na kutotoa nafasi kwa mashetani hao katika kukabiliana nao kwa ajili ya kulinda imani yenu na haki zenu ili kuonesha kwamba taifa liko makini kwa ajili ya kusimamisha uhuru.

Ni fahari ilioye kwa wanawake wetu watukufu katika kukabiliana na serikali ya kidhalimu, na baada ya kuipindua katika kukabiliana na wakoloni, washirika wake na kusimama safu ya kwanza kuonesha nafasi waliyokuwa nayo kwamba katika zama hizi hakuna nafasi kama hii na ushujaa kama huu haujawahi kutokea.

Ukuaji wa siasa kwa wakufunzi wa kale na wa sasa kutokana na propaganda za miaka mia moja za njama za wakoloni upo nyuma ya pazia na kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na serikali dhal-

imu, kusimama kidete kwa ajili ya kulitetea bila ya kuwa na hofu kwa taifa linalodhulumiwa kutokana na adhabu na kifungo.

Sisi tunachotaka ni kujisimamia wenyewe, sio ubalozi wa Marekani wala ubalozi wa Urusi. Sisi tunataka nchi yetu ijitarawale wenyewe na isitawaliwe na Mayahudi wala Isralili. Sisi tunataka nchi yetu iwe huru, kusiwe na unyongaji katika nchi yetu. Sisi tunataka jeshi liwe huru, lisimiliwiwe na Isralili na Marekani

Mapinduzi ya Kiislam ni kama mapinduzi tuliyokwishajifunza katika historia ya Mitume ambayo hayakutegemea kazi bali yalitegemea na kitu kimoja tu, nacho ni chanzo cha *wahyi* na kumtegemea Allah (s.w.t).

Ewe Allah! Iwapo hakuna mtu mwenye kujua basi ni Wewe mwenyewe tu, Ndiye unayejua kwamba sisi tumepambana kwa ajili ya kui-nua bendera ya dini Yako na kwa ajili ya kusimamisha uadilifu na kum-fuata Mtume Wako katika kukabiliana dhidi ya mashariki na magharibi na katika kushikamana na njia hii kamwe hatutapoteza muda.

Mapinduzi ya Kiislam ni kigezo cha wenyе kudhoofishwa

Sisi tunatangaza kuwa Jamuhuri ya Kiislam ya Iran, siku zote itakuwa ni watetezi na wasaidizi wa uhuru wa Waislam duniani. Iran itakuwa ni mfano wa jeshi (ngome) na sababu ya kuwa na jeshi la Kiislam ni kwa ajili ya kusimamia itikadi (imani) na malezi ya Kiislam na pia kuwa na kanuni na mbinu za kupambana dhidi ya mifumo yote ya kikafiri na kishirikina.

Mataifa ya Kiislam ni lazima yaige na kuchukua mfano kutokana na kujitolea kwa mujahidina wetu katika njia ya uhuru na malengo ya kuendeleza Uislam, kushikamana pamoja kujitoa katika bwawa la ukoloni na unyonyaji na kusonga mbele katika wema, ukarimu na kuyaende maisha ya kiubinaadamu.

Kushindwa kwa mapinduzi ya Kiislam ya Iran Ni kushindwa kwa Uislam

Wote mnaodhoofishwa duniani ambao mpo chini ya utawala wa kikoloni na kishetani ni lazima mtambue na mzingatie kuwa kipengele cha myeyuko wa upinzani ni lazima muuhifadhi. Kama Allah (s.w.t) hakutaka kipengele hiki ambacho tayari tumeshaanza nacho, upinzani dhidi ya wakoloni wote na mashetani wote duniani, na ukapatikana unyonge wowote ule, au sisi tukashindwa, basi watashindwa wale wanaodhoofishwa duniani pamoja na Waislam wote duniani, na hapo ndio kushindwa kwa uislam na nchi zote za Kiislam.

Moja ya mapambano ambayo sisi tumeyafanya hivi sasa katika kukabililiana na makafiri ni kuhusiana na hali ngumu na ya mashaka iliyokithiri duniani ambayo nyinyi ndio wenyewe athari katika hilo. Msifikirie kwamba Iran ikishindwa basi itakuwa imeshindwa Iran pekee, ndipo itakuwa Mashariki yote imeshindwa, ikishindwa Iran ndiyo kushindwa kwa wanaodhoofishwa, hivyo ni lazima wote kwa pamoja tuwe na umoja, wote kwa pamoja tupambane ili tuweze kuitokomeza fisadi hili katika ulimwengu wa historia

Hivi ni kwa nini Waislam washindwe, hawaangalii kwamba Jamhuri ya Kiislam ya Iran kama hii iwapo itashindwa Uislam utashindwa? Kwa nini hamuoni kuwa ukoloni unauogopa Uislam na unaipinga Iran kuhusiana na jambo hili, wanauogopa Uislam na katika ukuaji wa miji mingine, maana yake ni hii kwamba imeshajitokeza nchini Iran basi na sehemu nyingine pia itakuwa.

Kuyaeneza Mapinduzi

Uislam si mali ya taifa maalum. Uislam umekuja kwa ajili ya watu na sio kwa ajili ya Waislam na wala si kwa ajili ya Wairan. Mitume

wametumwa kwa wanadamu na Mtume wa Uislam ametumwa kwa ajili ya wanadamu, wito kwa wanadamu:

يَا إِيَّاهَا النَّاسُ

“Enyi watu”

Na sisi tumefanya harakati hizi kwa ajili ya Uislam.

Jamhuri, ni Jamhuri ya Kiislam. Harakati kwa ajili ya Uislam haitoweza kuingia katika mtego wa nchi moja na kamwe haitoweza kudanganya hata katika nchi za Kiislam. Harakati kwa ajili ya Uislam ni zile ambazo zilifanywa na Mitume, na harakati za Mitume hazikuwa za mahali pamoja tu. Ukimwangalia Mtume Mtukufu (s.a.w.w) utaona ya kuwa yeye alikuwa ni mzaliwa wa Uarabuni, lakini wito wake haukuwa ni kwa ajili ya Waarabu, kwani wito wake haukuwa mtego kwa Uarabuni, wito wake ulikuwa ni kwa ulimwengu wote.

Uzoefu tuliokuwa nao tunautoa duniani na hatimaye mapambano na ulinzi kutokana na madhaalimu bila udogo wa jisho uliokuwa nao, na mapambano tunayahamishia kwenye njia ya haki na Waislam ni waanzilishi wa uzoefu huu, bila ya maua ya ushindi, uhuru, na utekelezaji wa hukumu za Kiislam kwa ajili ya mataifa, basi haitokuwa kitengo,

Kwa matakwa ya Allah (s.w.t) tunataka kuvunja uchokozi na ukandamizaji wa madhalimu wote katika nchi za Kiislam na kuyaeneza mapinduzi yetu katika haki ya kuyaeneza mapinduzi ya kweli, kubainisha hukumu za Muhammad (s.a.w.w), kuhitimisha utawala wa kisultani na wa kidhulma na kwa msaada wa Allah (s.w.t), tunonyesha njia kwa ajili ya kuibua mwokozi na Imam wa zama, Allah (s.w.t) amuhifadhi.

Leo hii sisi tunaeneza matarajio ya Allah (s.w.t) katika ulimwengu wa wanaodhoofishwa, wanaodhulumiwa na tunashuhudia harakati zake zilivyoanza hatua kwa hatua, zipo katika hali ya kuendelea kuelekea upande wa wanaodhoofishwa na wanaodhulumiwa duniani dhidi ya madhalimu na wana harakati.

Ni dhahiri kwamba wenye imani wanaamini kuwa ahadi za Allah (s.w.t) ziko karibu sana kama dunia itakuwa tayari, kwa ajili ya kuchomoza mionzi ya uongozi, ikichomoza kutokea Makka Tukufu na kutangazwa uongozi wa wanaodhoofishwa mbele ya Kaaba.

Hongera siku hiyo ambayo mataifa yote ya Kiislam yatakuwa ni taifa moja na wote kuwa na sauti moja, kusudio moja na Uislam ukafufuliwa kila mahali na nchi zote za Kiislam zikaungana hadi pale zitakapofanikiwa kukata mikono ya mabepari.

Uvumilivu Kwenye Taabu na Matatizo katika Mapambano

Ugumu na Matatizo ya Manabii

Kama tunavyofahamu kuwa Uislam ulikuwa ukiongozwa na Mtume wa Allah (s.w.t), ni jinsi gani alivyotaabika, umri wake wote ulikuwa katika taabu na shida, baada yake pia Maimam wetu walikuwa hivyo hivyo. Hakuna hata siku moja ambayo walikuwa na maisha ya furaha ingawa kwa upande mmoja wote walikuwa wenye furaha hasa katika masuala ya utata. Hii ilikuwa ni moja ya njia ya kwanza iliyokuwa ni mapenzi ya Uislam ambayo wenyewe walikuwa kwenye njia yenye malengo yaliyowapeleka kwenye kifungo, mateso na hatimaye kuuawa.

Na hii ilikuwa ndiyo njia ya wapenzi wa Allah (s.w.t), si kwamba walikuwa katika wakati wa Uislam tu, bali hata kabla ya Uislam. Manabii na Mawalii wa Allah (s.w.t) walikuwa kwenye njia hiyo hiyo, hawakuwa wanajistawisha na mambo ya kidunia.

Wakati ukiyazingatia maisha ya Mitume utaona ya kwamba historia ya Mitume zama hadi zama walikuwa ni Mitume wenyewe sifa ya ujihadina, wenyewe shida na taabu, wenyewe waliyafurahia maisha yao, lakini walikuwa katika malengo yao.

Kuuhifadhi Uislam ni jambo la lazima ambapo Mitume wakubwa tangu Nabii Adam (a.s) hadi kufikia kwa Mtume wa mwisho (s.a.w.w), walikuwa kwenye njia hiyo hiyo iliyoambatana na juhudini na kujitolea nafsi zao na hawakuwa na kizuizi chochote kile katika kutekeleza wajibu wao huu mkubwa. Pia, baada yao Maswahaba na Maimam Watukufu (a.s) walifanya juhudini za kuuhifadhi Uislam hadi pale walipojitlea kumwaga damu zao.

Maimam na Uvumilivu katika Matatizo

Uislam ni dini ya damu kwa ajili ya kuongoza dini na watu. Mawali ni wetu hawakuwa na hofu ya kumwaga damu wala hawakuhofia kuingia kwenye vita vya umwagaji damu. Amirul Muuminin (a.s) alikuwa ni kiumbe wa pekee katika wakati huo ambapo alikuwa na *Nahjul Balaghha* kwa ajili ya mwongozo na upanga kwa ajili ya wale wanaofanya njama.

Sisi tumetoa damu na mashahidi. Uislam umetoa damu na mashahidi. Sisi tuna tofauti nyingi na Ali bin Abi Twalib (a.s), Ali bin Husein (a.s) na waliowekwa vichwa vyao juu ya mkuki mfanano Bwana wa Mashahid (Imam Hussein (a.s)), Maswahaba zake na familia yake. Uislam katika zama zote ulisimamishwa kwa damu, upanga, na sulhu.

Kama asingelikuwa ni Husein Bwana wa Mashahidi, Yazid, baba yake na jamaa zake wangeupoteza Uislam na wangesambaza fikra za kidhalim. Muawiya na Yazid waliutangaza Uislam kwa kutumia njia ya kidhalimu. Na laiti asingelikuwapo Imam Hussein ((a.s), basi uta-

wala wa kidhalimu ungepata nafasi na kukua kila mahali, wangerudisha Uislam wa zama za kijahiliya. Je, mimi na wewe tungekuwa Waislam? Ungekuwa Mwislam dhalimu na sio mwenye Uislam wa Imam Husein (a.s).

Imam Husein (a.s) ameukomboa Uislam. Je, sisi tukae kimya kwa mtu ambaye ndiye aliyeuokoa Uislam? Sisi kila siku ni lazima tulie, sisi kila siku ni lazima tupande juu ya *mimbar* kwa ajili ya kuhifadhi dini hii, kwa ajili ya kuhifadhi harakati hizi. Hizi ni harakati zilizohuishwa na Imam Husein (a.s).

Watu na Kuvumilia Matatizo

Watu watukufu wa Iran na Waislam wapenda uhuru duniani kote, ni lazima wajue kwamba kama tutataka, bila ya kupinda kushoto wala kulia na tujitegemee wenyewe kutokana na kila nguvu na ukoloni na kutosimama chini ya miguu yao, basi lazima tuhakikishe kwamba thamani ya uhuru tunaitunza na kuitumia vizuri.

Mapinduzi ya Kiislam katika nchi ya Iran yamepatikana kwa damu za mashahidi, majeruhi na kuharibiwa kwa majumba, kuchomwa moto mashamba ya mitende, kuuwawa idadi ya watu, kuchukuliwa na kukamatwa mateka vijana wa mapinduzi wa Kiislam katika mikono ya dikteta wa Iraq na kupoteza maisha ya mamia kutokana na matatizo na ugumu wa uchumi.

Uhuru wa taifa la Iran umejifunza mengi kutoka katika ulimwengu wa kikafiri kama kuharibu na kuangusha nyumba hali ya kuwa watoto wamo ndani yake na hatimaye kupoteza maisha, kujitolea kwao, ujahidi wao na kusimamia mapinduzi ya nchi yao.

Usijiweke mbali na kuuawa au kuua katika njia ya kudai uhuru. Kudai uhuru kwa ajili ya Allah (s.w.t), kwa ajili ya dini Yake, kwa ajili ya kuwatetea wanaodhoofishwa na kwa ajili ya kukata matumani ya wakoloni na madhalimu.

Wasia kwa Taifa la Iran Katika Mapambano

Uislam uliokuwa katika mikono yetu leo hii ni amana. Ni amana ambayo sisi tumeichukua kutoka mikononi mwa Mtume wa Allah (s.w.t) na ni lazima kuuhifadhi na kamwe tusifanye hiyana katika hili. Wakati tukiwa kama washika amana hii, ni jukumu letu sote kwa pamoja kulitekeleza ili kupatikane usalama na nguvu kwa ajili ya kuwafikishia vizazi vijavyo.

Sisi tulikuwa na wasiwasi kwa ajili ya nini? Hali ya kuwa sisi ndiyo tunaotekeleza majukumu yetu na tunaoyafanya kazi. Tuwe na wasiwasi ili tusije kwenda kinyume na njia ya haki. Wao lazima wawe na wasiwasi kwa sababu iwapo watauawa kwa itikadi yao ni kwamba ndiyo wameangamia, na kwa itikadi yetu ni kwamba watkwenda Jahannam.

Sisi tulikuwa na wasiwasi kwa ajili ya nini? Kwamba, iwapo sisi tutauwawa basi tutakuwa mashahidi, roho zetu zitaondoka hapa duniani kuelekea uwingu wa juu na tutakuwa tumefika katika njia tukufu. Basi kwa nini tuwe na hofu? Kwani wanaume pia huwa na hofu? Kwani ushahidi pia una hofu? Rafiki zetu ambao wamekuwa mashahidi wako kwenye njia ya haki na wanapata rehma.

Ni vipi Maimamu wetu (a.s) walivyojitlea na kila walichokuwa nacho walikitoa katika njia tukufu ya Kiislam. Pia sisi ni lazima kuwafuata wao, basi tujitolee kwa kila tulichokuwa nacho kwa ajili ya Uislam. Uislam ni bora zaidi kuliko kitu chochote na kwa kuwa ina utukufu zaidi kuliko kitu chochote ndiyo maana Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Maimamu wetu Watukufu (a.s) walijitolea kwa kila walichokuwa nacho.

SEHEMU YA TATU

Uislam wa Mustadhaafin na Wanaooneewa

Maana na Ufahamu wa Kudhoofishwa na Kutawaliwa

Leo ni siku ambayo Allah Mtukufu (s.w.t), ametuhurumia, ametupa uhuru. Uhuru wetu na uhuru huu kwetu sisi ni mtihani. Rahma hii tuliyopewa ya uhuru tuangalie ni nini cha kufanya. Tumekuwa huru na Allah (s.w.t) ametupa rehma hii ili tuangalie nini cha kufanya. Je, nasi pia tuwe kama wanaodhulumiwa au wanaodhoofishwa? Kila mtu atakuwa anayedhulumiwa na anayedhoofishwa.

Iwapo mimi nikiwa chini ya mikono yangu mwenyewe, kuna walau kwa watu wanenye, basi lazima nitakuwa nimewaingilia na kuwadharau. nikimdhara mja wa Allah (s.w.t) basi mimi ni dhaalim, nitakuwa nimemdhooofisha, na hiyo yote kwa pamoja ndiyo maana ya waliodhoofishwa na waliooneewa.

Ikiwa wewe utakuwa umewaweka chini ya mikono yako, utakuwa umewadhoofisha, utakuwa umewatawala, basi na wewe pia utakuwa ni dhalimu na utakuwa chini ya mikono ya waliodhoofishwa.

Sisi sote tumedhoofishwa, yaani tulikuwa ni watu tuliodhoofishwa na wakoloni na hatukujua chochote. Hivyo, sasa tunachotaka ni kujitoe kabisa katika mfumo huu.

Uislam safi ni Kuwahami Wanaodhoofishwa

Uislam ni kwa ajili ya watu wote. Uislam umetokana na umoja na umefanya kazi kwa ajili ya umoja huo. Uislam haukupatikana kwa tabaka la juu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alitoka katika jamii ya watu

wenye tabaka la chini na kutokana na jamii hiyo hiyo, alisimama kwa ajili ya mapambano.

Maswahaba zake pia walitokana na tabaka hilo hilo la chini. Kutokana na hali hiyo, alikuwa akipata pingamizi na kuhitilafiana na watu waliokuwa kwenye tabaka la juu na ndiyo ikawa sababu ya kutokea mapambano baina yao.

Allah Mtukufu (s.w.t) haangalii mtu yuko katika tabaka gani au cheo gani, bali anachoangalia Yeye ni mchamungu kama alivyosema kuwa:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ اتِّقَاكُمْ

“Hakika mbora kwenu mbele ya Allah ni mwenye taqwa (mwenye kumcha Allah)” (*Suuratul Hujurat*, Aya ya 13)

Katika Uislam hakuna ubora. *Taqwa* ndiyo bora. Kila mwenye *taqwa* zaidi basi mbele ya Allah (s.w.t) ana ubora na utukufu wa hali ya juu.

M pangilio wa Uislam tangu zama za kushuka wahyi hadi sasa unakwenda sambamba na shahada. Kuuliwa katika njia ya Allah (s.w.t) na katika njia ya wanaodhoofishwa ni moja ya kazi na mipangilio ya Uislam.

وَ مَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَ الْسَّتَّضَعَفُونَ
مِنَ الرِّجَالِي وَ النِّسَاءِ وَ الْوِلَدَانِ

“Na mna nini hampigani katika njia ya Allah na ya wale wanaoone-wa katika wanawake na wanaume na watoto....”
(*Suratun Nisaa*, aya ya 75)

Uislam tangu mwanzo uliamrisha kusimama na kupambana kwa ajili ya kukabiliana na kukaa mbali na watu wabaya, madhalimu. Uislam unatuamrisha tuwasaidie wote wanaodhoofishwa hadi pale watakapojisimamia wenyewe.

Ushindi wa Wanaodhoofishwa dhidi ya Madhalimu

**وَنُرِيدُ أَن نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتَضْعَفُوا فِي الْأَرْضِ
وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ**

“Na tunataka kuwafanya hisani wale waliodhoofishwa katika ardhi na kuwafanya viongozi na kuwafanya warithi.” (Suratul Qasas, aya ya 5)

Hii ni amri ya Allah Mtukufu kwa taifa tukufu, wakifuatiwa mashekhe na viongozi wa dini kuleta vikwazo katika utawala wa kidhaalimu ili kuwakomboa wote wanaodhoofishwa waweze kujisimamia wenyewe katika mambo mbalimbali yanayohusu jamii yao.

Enyi ambao mmedhoofishwa duniani! Enyi nchi za Kiislam na Waislam duniani! Simameni! Ichukueni haki hata kwa vita na kwa meno. Wala msitishike na vitisho vyao. Hukumu zao za kihalifu kwenu zitajisalimisha katika utukufu wa Uislam na kurejea kwenye nchi zao na hatimaye muungane pamoja na kuwa chini ya bendera ya Uislam ili muweze kujilinda na maadui wa Uislam na kuunda serikali moja ya Kiislam ya Jamhuri, iliyo huru, isiyofungamana na hali yoyote ile.

Inshaallah, kwa Baraka za Kiongozi wa Zama, Allah (s.w.t) amhifadhi, juhud hizi na dharba za kiutu zitaelekea kwenye ukombozi. Na wale wote waliodhoofishwa duniani waweze kuwa huru dhidi ya udhalimu. Ni matumani yangu kwamba utawala uliokuwa mkubwa,

mmoja, wa Mtukufu huyu (Imam Zaman (a.j.f.s) utakuwa wa haraka ili uweze kuleta nuru Tukufu na kutuangazia kwenye macho yetu na Waislam wote duniani.

Mashekhe wa Kiislam ni Tegemeo la Wanyonge

Ni kwa mamia ya miaka sasa ambapo mashekhe wa Kiislam wamekuwa tegemeo kuu la wanyonge. Siku zote wanaodhoofishwa wanakata kiu chao kutokana na maarifa na elimu ya mafaqihi wakubwa. Kutokana na jithada, elimu na utamaduni wao, kwa haki ya kufuzu na kupita katika njia bora iliyotokana na damu ya mashahidi.

Hawa wako kila zama. Tangu zama za kutetea dini tukufu, ardhi yao, kuvumilia mashaka, taabu, kuhamishwa, kufungwa, adhabu, kujeruhiwa na hata kupata daraja la ushahidi. Enyi masheikh watukufu! Lazima muangalie kwa makini jambo hili na kujivunia historia iliyokuwepo zaidi ya miaka elfu iliyopita. Kwamba, kimbilio la wanyonge ni kwenu. Ninyi mkiwa kama viongozi wa watu, basi wahifadhini. Wote kwa pamoja muwe chini ya bendera ya Uislam na mjilinde dhidi ya maadui wa Uislam.

Kitu ambacho ninyi masheikh mnatakiwa mjiepushe nacho ni upotoshaji. Hampaswi kuingia na kukimbilia kwenye mchakato wa aina yoyote mwengine wa matangazo (usiokuwa wa kiislam), bali, mnachotakiwa kufanya, ni kusaidia wanyonge wasio na kitu. Kwani, kila atakayefanya upotoshaji, basi atakuwa amepotosha uadilifu wa jamii katika Uislam. Sisi lazima tuwe chini ya masharti. Tujue kwamba, haya ni moja ya majukumu makubwa. Kwa hakika, kama tutafanya mapungufu yoyote, basi tutakuwa tumeufanyia hiyana Uislam na Waislam kwa ujumla.

Kudumisha misingi sahihi ya kutetea waliodhoofishwa

Tufanye juhudini zote hadi ifikie mahali kwamba upo uwezekano wa kulinda na kuwatetea waliodhoofishwa. Viongozi wa Iran na mapinduzi kwa ujumla, lazima mjue kwamba waja wa Allah (s.w.t) wako kimya kwa kutaka kuyaharibu mapinduzi. Kila anayetaka, afanye kazi kwa ajili ya kuwasaidia mafukara, maskini na kusimama katika njia ya Uislam na mapinduzi. Kateni mizizi ya ukomunisti na wala msiogope katika hili. Lazima mumshirikishe Allah (s.w.t). Juhudi zote mzifanyazo ziwe ni kwa ridhaa ya Allah (s.w.t). Kamwe mstishike na kuogopa tuhuma katika kusimamia kazi na kuwasaidia mafukara.

Lazima tuijandae, tuwe tayari kushirikiana pamoja kukabiliana dhidi ya mashariki na magharibi, kwa kushikamana na jeshi lenye nguvu la Uislam, ubinaadamu, kwa jina hilo hilo, kwa nembo ya Uislam na Mapinduzi kwa ujumla.

Nafasi ya Wanyonge Katika Ushindi wa Mapinduzi ya Kiislam

Dini zote tukufu zimesimama pamoja kuwasaidia wanaodhoofishwa dhidi ya dhuulma. Wote wanaodhoofishwa, kila Zama, walikuwa wamesimama kuwasaidia Mitume wa Allah (s.w.t). Katika Uislam, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisimama akiwa na wanyonge, aliwasaidia, na alifanikiwa na akashinda.

Wanaodhoofishwa wa dini zote wanahitaji haki. Wanaodhoofishwa wana haki katika Uislam. Hii ni kwa sababu, katika historia ya miaka 1400 iliyopita, jamii hii ilitoa msaada mkubwa kwa Uislam.

Uongozi wa Kifalme na wa kidhalimu ulishikamana na dhuulma. Na siku zote, njia yao ilikuwa si ya Kiislam. Walipambana na Uislam na waliendelea na mfumo wao wa kijahilia. Ilikuwa ni wanyonge ndiyo waliowafuata mitume, mawalii na maulamaa.

Mapambano yetu yanasonga mbele daima pamoja na wanyonge wanaodhoofishwa. Lakini, madhalimu walikuwa wanakimbia au kuka majumbani mwao. Hivi sasa wanataka kutumia neema iliyopo na kukaa meza moja. Walikuwa wapi siku zile pale wanyonge walipomwaga damu zao? Au waliposhambuliwa kwa silaha? Au walipotolewa nje ya nchi? Wanyonge hawa hawa ndiyo waliosaidia mapambano yetu yasonge mbele, hawa hawa ndiyo waliomwaga damu zao.

Vijana wasomi wa vyuoni, madrassa, sokoni, wasoma mashairi, hili lilikuwa ni tabaka ambalo lilisimama na kupambana na uongozi wa kidhalimu na walifanikiwa kurudisha nyuma nguvu zao na kukata mikono ya kidhalimu.

Kuwahudumia wanyonge na wasiojiweza

Moja ya jambo kubwa, muhimu na la kiroho ni kuwahudumia vi-umbe wa Allah (s.w.t). Kuwahudumia wanyonge. Jambo hili linafaa sana, linabakia milele hapa duniani na kesho akhera. Kulimbikiza mali hakutomfaa mtu yejote, bali kifaacho ni kuzitoa zitumiwe kwa manufaa ya wanadamu.

Leo hii, kuwahudumia wanyonge na maskini ni neema ilijoje mbele ya Allah (s.w.t). Hakuna msaada ulio mdogo, bali una fadhilaa kubwa mbele ya Allah (s.w.t).

Viongozi, wahudumu, wakuu na masheikh wote mnatakiwa kuwa waadilifu katika tawala zenu, kuwa na mahusiano ya karibu na mafakiri, maskini na wasiojiweza. Ili kuwa makini, lazima muwe karibu na watu hawa na mjue matatizo yao. Ni fahari ilijoje kwa mawalii na maulamaa ambao wamekuwa wanaiendeleza na kuifanya kazi fikra hii muhimu.

Tabaka la umaskini ni asili ya viongozi.

Zingatieni kwamba, rais wa Jamhuri na Spika wa bunge la Jamhuri awe ni mtu aliyetoka katika tabaka la wanyonge katika jamii na kuonja ladha yake, au mwenye fikra ya watu hao. Kamwe asi-toke katika jamii ya matajiri, au aliyezama katika ladha na matakwa ya kidunia ambaye hatakuwa na hisia za machungu ya unyonge na taabu ya njaa na umasikini kwa ujumla.

Ni matumaini yangu kuwa mtakuwa wahudumu na wahifadhi wa viumbe hawa wa Allah (s.w.t) ambao ni madhlum na wale walio-kuwa wamedhulumiwa, hii ndiyo sifa ya wahudumu. Na *Alhamdulillah*, ninyi pia mnatoka katika tabaka hilo hilo, hamtoki katika tabaka la juu, yaani ninyi nyote mnatoka kwenye tabaka la chini. Ninyi mnatoka katika tabaka safi, wale ambao uongozi ulikuwa wao, kwa ajili ya wanaowaongoza na hili ni tabaka lisilokuwa na kitu. Allah (s.w.t) awape taufiki siku zote muwe mnatoa huduma.

Umaskini kipengele muhimu katika uchumi wa kiislam

Kwa ujumla, zipo sheria za Kiislam katika masuala ya uchumi. Wakati ukiangalia takwimu za Kiislam ndipo utapata picha kwamba Uislam ni moja ya dini inayotilia mkazo katika kila jambo la mai-sha ikiwemo kutatua matatizo ya ufukara na kuuona ujisadi kuwa ni njia ya kujikusanya utajiri. Uislam unazuia ujisadi, unailinda jamii dhidi ya ujisadi, unapinga kukua kwa ubwana, ukoloni na ubora na ubwana baina ya watu.

Uchumi wa Kiislam unawalenga kuwasaidia Waislam maskini kutoka katika kila kona ya nchi yetu kuwaelekea mafukara na kuwatetea wanyonge. Matumaini ni kuwa, kwa utaratibu huu, ubepari utakatika, utukufu utapatikana na kukua katika kila kona ya ulim-wengu wa Kiislaam.

Moja ya jambo la msingi ambalo lazima litiliwe mkazo ni kwamba Uislamu si mwekezaji wa kibepari, muonevu na anayedhulumu raia, bali Uislam ulivyo ni makini kwa kufuata hukumu za Kitabu Kitukufu na Sunna ya Bwana Mtume (s.a.w.w) na kuwaonya wapingga haki za jamii.

Kujitegemea kokote kule ni kule ambako mwanadamu mwenyewe anatakiwa awe nao. Kujitegemea kunapatikana kwa mwanaadamu mwenyewe. Wakati mwanadamu anapokuwa anajitegemea, hata nafsi yake pia itakuwa tegemeo kwa dunia ambayo ni mali yake, nafsi yake na hali yake.

Endapo mwanadamu atakuwa amezinduka na kuondokana na utegemezi huu, basi atakuwa huru katika hili. Huu utakuwa ni uhuru mwingine. Hatokuwa anamwogopa mtu tena hata kama ulimwengu wote ukashirikiana pamoja kumpinga, ye ye hatoogopa.

SEHEMU YA NNE

UISLAM NA MAISHA YA KAWAIDA

Maisha rahisi, ya kawaida ndio thamani ya viongozi wa dini ya Allah (s.w.t)

Nukta iliyopo hapa ambayo inastahiki kutolewa shukurani kutoka kwa maulamaa, mashekhe, watumishi wa nchi na wanyonge ambayo ni lazima nisisitize na kuonya, kwamba ni lazima kuishi maisha ya kawaida na kujinyima.

Maulamaa na mashekhe mlioshikamana na Uislam ni kama baba wa wa watoto wote ambao Allah (s.w.t) amewapa kazi ya kuongoza nchi kubwa na kufikisha ujumbe wa Mitume. Kama mlivyoambi-wa kuwa; kamwe msitoke katika mstari wenu kwani ninyi ni kama cheche na mfano mwema katika dunia hii kwa ajili ya kuendeleza mfumo wa Jamhuri ya Kiislam ya Iran. Hivyo, kuweni wema na hata siku moja kamwe isitokee hatari kwa ajili ya mashekhe na kwa ajili ya dunia na akhera yenu.

Zingatieni mwenendo wenu usiwe ni wa kidunia, kwani alhamdulillah, mashekhe mmeshikamana na Uislam na mmepewa mtihani wa kujinyima wenyewe.

Nyinyi ambao mmekuwa mabalozi na mna wadhifa wa kisheria. Na kwa kila kilichokuwa rahisi katika balozi zenu, maisha yenu kwa ujumla lazima yawe ya kawaida. Watu mnaowafanyia kazi huko mliko watakuwa chini ya mikono yenu. Muwe ndugu kwao. Katika hali kama hii ni lazima mkubalike kwao. Mkubali hali za watu wa huko, wekeni mazingira ya Kiislam na kila mtu atakapofika hapo auone Uislam wenu kwa vitendo.

Kila tunapopaza sauti kuwa sisi ni Waislam na ni Jamhuri ya Kiislam lakini **wakati** wakituangalia matendo yetu ni tofauti na Uislam, kamwe hawatakuwa na imani na sisi. Mahali wanapoweza kutuamini ni kuanzia pale tunapotamka kwamba sisi ni Jamhuri ya Kiislam. Maulamaa wetu ni hivyo hivyo. Wasifanye matendo ya kishetani. Kauli ziwe za Kiislam, matendo na mwenendo wetu uwe wa Kiislam. Kuzungumza kwetu kuwe Kiislam na mapinduzi haya tuyaneze katika nchi zote.

Umuhimu wa kuwahifadhi wanazuoni wa kidini

Mafanikio mengi na ushawishi wa mashekhe katika jamii ya Kiislam naufahamu hasa katika thamani ya vitendo na kujinyima (kukinai). Hivi sasa thamani hii si kwamba isahaulike tu bali lazima izidishwe zaidi kuliko hapo nyuma. Hakuna kibaya zaidi kwa mashekhe kama kupenda dunia.

Pia, hakuna kitu kibaya na kibaya zaidi kama kuungana na dunia, mashekhe kuchafuliwa labda kwa kuwa na marafiki wajinga, maadui wajinga, na moyo wa huruma uliokosa njia ya kujinyima katika mai-sha yao, mashekhe kutetea ubepari, kuwa upande wa kibepari na kuwa na tuhuma za uwekezaji.

Katika mazingira haya, hatima ya maamuzi nyeti na muhimu ambayo mashekhe wanatakiwa kuwa nayo katika kujenga na kusimamia nchi ni hatari kufikiria kudhulamu wengine kwa hadhi ya ushekhe wao. Wanapaswa kuwa makini katika mwenendo wao, iwe watu kutoka katika mashirika, vyama, mashirika ya kisiasa na zaidi ya hayo ambayo yana muonekano wa Kiislam kwa asilimia mia moja yaye yana sifa ya kujenga uaminifu kati yao.

Ingawa tunajua kwamba *marjaa* wetu, maulamaa na wasomi wakubwa wamefungamana na baraka nyingi, na ni makini kwa

maamrisho haya, lakini khofu yangu bado ipo pale pale. Kwamba, pindi utukufu utakapofananishwa na cheche kitakachopatikana hapo ni maisha ya kawaida na ya kimaada ambayo athari yake itaendelea hadi kizazi kijacho na Allah (s.w.t) asijaalie hayo, na kile ambacho mimi nakiogopea, ni haya yasije kutokea katika *hauza* zetu (vyuo vikuu vya kidini).

Ni muhimu sana, hususan kwa viongozi ambao mtakuwa mk-iendesha na kuongoza mambo haya, ni lazima mzingatie kuzuia ukatili na hali ya mashaka na kila mkifanyacho katika kuhudumia *Hauza* hizo iwe ni kwa ajili ya kuuhudumia Uislam na elimu ya Kiislam kwa ujumla, mrekebishe vitendo vyenu na mjiepushe na matendo maovu.

SEHEMU YA TANO

SURA YA KWANZA

SIFA ZA UISLAM WA KIMAREKANI

KUTENGANISHA DINI NA SIASA

Uislam wa Kimarekani ni kutojihusisha katika siasa

Suala la kutenganisha siasa katika dini siyo kitu kigeni. Ni mpanago uliokuwepo tangu zama za Bani Umayyah na ulipata nguvu na kuimarika katika zama za Bani Abbas. Katika zama za hivi karibuni, ambapo mikono ya nchi za kigeni imefunguliwa na kuyavalia njuga mambo haya kiasi kwamba hata baadhi ya watu wa dini na mashekhe nao pia wameweza kuwaamini na kufungamana nayo na kiongozi yejote wa kidini atakayeingia katika masuala ya kisiasa basi ataadhibiwa. Hii ni moja ya mipango mikubwa ya wakoloni ambayo baadhi yao wameiamini.

Kiburi cha wakati huu ambacho kinatokana na uharibifu halisi wa mashekhe na vyuo vikuu vya kidini waliopotea kwa ajili ya mgommo na mashambulizi unaweza kuchagua njia mbili;

1. Ni njia ya vitisho na nguvu,
2. Ni njia ya udanganyifu, ushawishi,

Njia za ushawishi zimeimarika maradufu. Ya kwanza na muhimu ni kutambulishwa na kusonga mbele kwa kauli mbiu ya kutenganisha dini na siasa. Kwa bahati mbaya, mbinu hii imeingia katika vyuo

vya kidini na katika nyoyo za wanazuoni kwa kiasi kikubwa. Mbali na kujihusisha katika siasa kwa kisingizio cha utegemezi, bila shaka wanazuoni na mujahidina ndiyo waliojeruhiwa na ushawishi huu zaidi.

Uislam kwa upande mwingine unatuonyesha kwamba hii ilikuwa ni njia ambayo pamoja na mipango, ilifanyiwa kazi. Sisi wenyewe pia ilifika muda tuliweza kuamini na kujiuliza maulamaa katika siasa ni akina nani na wanafanya nini? Haya ni maneno ya kikoloni. Yaani, maulamaa wana nini katika siasa?

Katika dua ya Jami'a, neno **سَاسَةُ الْعِبَادِ** lina maana ya: "**kutoa mafunzo na ufundi**"

Vipi sera ya Imam katika siasa? Ndiyo, lakini sheikh si siasa?

Hadhrat Amirul Mu'uminiin (a.s) aliendesha nchi, katika utawala wake alikuwa mwanasiasa. Basi sera ya sheikh katika siasa ni nini? Mambo haya ni kwamba sera ya wakoloni ilikuwa ni kuwaondoa na kuwatenganisha masheikh katika serikali na taifa. Walitaka kuwatumia, mara wakawaamini. Masheikh nao wakaanza kupingana na sisi kuwa je, na nyinyi mna sera gani katika siasa! Usheikh huu ni siasa! Mambo haya ndiyo yaliyotufanya sisi kubaki nyuma, yanarudisha nyuma. Usheikh ni sampuli ya Uislam.

Wakati mwingine shetani ni mjanja na mdanganyifu. Kwa hivyo, kwa upande alitetea utukufu wa Uislam ili Uislam na dini nyingine za Allah (s.w.t) zisimamie kazi za kiroho, kusafisha nafsi za watu, kuzuia uongofu, kuwaondoa katika mamlaka ya kidunia, kuwahimiza watu kuiacha dunia, washughulike zaidi katika masuala ya ibada, dhikri na dua. Kwamba, watu wanatakiwa wawe karibu na Mtukufu Allah (s.w.t), na kuwa mbali kabisa na dunia, uongozi na siasa.

Kusudi na lengo la upinzani hapa ni kwamba, wote hawa wali-kuwa wanataka kuifanyia marekebisho dunia. Walikuwa wanataka kuupinga Unabii - Mitume wa Allah (s.w.t) - pamoja na kwamba inasikitisha sana kwa upande wa pili, kuathirika mambo yote ya tabligh kwa baadhi ya maulamaa na wanadini waliokuwa wameghafili. Kwa Uislam kutojihusisha na hata kutojiingiza katika masuala ya uongozi na siasa, ilikuwa inaonekana kwamba kujishughulisha na masuala haya ni mfano wa kutenda dhambi na ni ufasiki. Pia, kuna wengine wanaona kwamba haya ni moja ya majanga makubwa yaliyokuwa ndani ya Uislam.

Kukataliwa na Kutengwa katika Ulimwengu wa Kisiasa

Mikono ya mabepari kwa kutumia watu na vikundi maalum walio-fanikisha kuleta migawanyiko katika mataifa ya Kiislam, kwa miaka mingi wamekuwa wakisuka mipango na cha kusikitisha ni kwamba wamefanikiwa kutoa matunda yao machafu kwa mataifa mengine.

Kujihusisha kwa maulamaa katika mambo ya kijamii imekuwa ni moja ya vikwazo vikubwa. Walipinga haki (uadilifu), nafasi ya maulamaa na hata katika mavazi yao rasmi pia yalionekana si kitu chochote. Iwapo ulamaa atavaa vazi hilo basi atatoka yuko nje ya haki.

Kujihusisha na masuala ya siasa ni hali iliyokuwa ikifasiriwa kuwa ni kinyume na dini na kwamba endapo ulamaa fulani ni mwansasa, basi tena, alionekana kuwa hapaswi kuwa ulamaa.

Propaganda hizo walizianza mapema wakati ambapo na mimi mwaka huo huo - wa kwanza na wa pili - nikarejea Qum. Wakati huo, Qum ilikuwa ikiongoza kwa maulamaa. Kulikuwa na watu wzushi waliokuwa wakisema kwamba kupatikana kwa gazeti katika nyumba ya ulamaa ilijulikana kuwa ni kosa. Ulamaa fulani kama

ni mwanasiasa humwita bidaa (ulamaa ni mwana siasa). Akiwepo mwanasiasa kwa ulamaa fulani basi ulamaa huyo alitengwa. Wali-kuwa wakimzuia na kumtenga katika masuala binafsi, kijamii na ya kisiasa. Matangazo ya mara kwa mara kama hayo walikuwa yakiwapa hofu maulamaa wakati wakitaka kuingia kwenye mambo haya.

Madhara ya Kutojihusisha Katika Siasa kwa Jamii ya Kiislam

Wakoloni walikuwa na imani hii na kawaida ya kusema kuwaambia wana dini kwamba:

“Dini inapaswa kutenganishwa na siasa na wasomi wa Kiislam wasijihuhshe na kuingilia katika masuala ya kijami na wala ya ki-siasa.”

Je, katika zama za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) siasa ilitenganishwa na dini? Je, katika kipindi hicho hakukuwa na maulamaa na wengine wakiwa wanasiasa? Je, zama za makhalifa kulikuwa na haki au hakukuwa na haki? Je, zama za ukhalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) siasa ilitenganishwa na dini? Je, Kulikuwa na makundi mawili?

Haya ni maneno ya wakoloni na hivi ndivyo walivyoyatengenza katika siasa zao ili dini isitumike kwenye masuala ya kidunia na kuuandalia mazingira ya mbali ulmwengu wa Kiislam pamoja na maulamaa wa Kiislam ili watu wasiweze kupigania uhuru wao. Kwa mtazamo huu walipata watu wengi na waliteka mali na utajiri wetu. Hili ndilo likuwa kusudio lao.

Athari za Kutojihusisha Katika Siasa kwa Vyuvo Vya Kielimu Vya Kiislam

Mikono ya mabepari kwa kutumia watu na vikundi maalum ambao walifanikisha kuleta migawanyiko kwenye mataifa ya Kiislam, kwa

miaka mingi, wamekuwa wanasuka mipango, cha kusikitisha ni kwamba wamefanikiwa kutoa matunda yao yaliyojaa uchafu kwa mataifa mengine. Ilikuwa na maana kwamba maulamaa na mashekhe ni lazima wabakie misikitini na kukaa katika kona za nyumba zao. Siku zote kazi yao ni hiyo tu, yaani, kutoka nyumbani kuelekea msikitini na kutoka msikitini hadi nyumbani. Wasiwe karibu na jamii wala kuwa na habari za kitu chochote kinachoendelea wala kutokea katika jamii hiyo.

Amri hii ilikuwa ya kuwajenga wanazuoni na kuwaburuza kwenye pembe za nyumba zao, vyumba vya madrasa na pembezoni mwa misikiti. Jambo hili lilishakuwa kwenye mpango na kukubalika na maulamaa wengi na balaa kubwa limeshawatokea watu wengi.

Ikiwa kulikuwa na sera muhimu kuhusu mambo ya kisiasa, kijamii na matatizo yote yaliyokuwa ya kisiasa, kijamii, Kiislam na nchi za Kiislam, maulamaa hawakustahiki kuyaingilia. Hizi ni sera zilizochukuliwa kutoka nchi za Ulaya, ambao nao pia waliwaburuza maulamaa wao kwenye nyumba zao. Hata wakitaka kufanya lolote kwa watu, hakuna mtu wa kusema kwa nini. Na hapa pia, katika taifa letu na miji mingine ya Kiislam, hali ilikuwa hivyo hivyo wakati ulamaa anapotaka kujihusisha katika sera moja ya kisiasa, basi ni jinsi gani watu watakavyoleta vikwazo juu yake!

Wanapaswa wawe kando ya kisiasa. Hatma ya matatizo ya Uislam na Waislamu iwe ni sera ambayo itakuwa mikononi mwa masultani na wanaowategemea tu. Hii ndiyo picha iliyochorwa kwa miaka mingi na kutumika kwa muda mrefu.

Na laiti kusingelikuwa na sera kama hii, au wasingeliyafkia malengo yao, basi nchi yetu na nchi za Kiislam ambazo maulamaa wao ni lazima wajihusishe kwenye masuala ya nchi na wanapaswa kuweka ajenda ya sera na mipango yao wenyewe, katika nchi za

Kiislam matatizo kama haya kamwe hayapatikani. Wao walishafahamu vizuri sana kwamba taifa ambalo mbele ya watu lina ushawishi, ufunguo wake ni watu.

Kinachopaswa kufanywa ni kwamba, watu hawa pia hawaruhusisiwi kuingilia mambo ya kisiasa. Na wao wenyewe pia waje kuamini kwamba hawapaswi kuingilia mambo ya kisiasa.

Hivi hivi ndivyo ambavyo wamagharibi walivyoyafanya makanisa, kanisa likajiweka kando na ndivyo ilivyokuwa kwa mataifa mengine. Hivyo basi, amri hii ndiyo iliyotufikisha sisi hapa tulipo sasa.

SURA YA PILI

UISLAMU UMELETA UONGOFU NA FURSA

Sisi tunajua kwamba, wakoloni na serikali zote zilizokuwa na mahusiano na wakoloni pamoja na Uislam wa kifalme na kiraia hauna upinzani wowote, hii haina shaka. Lakini pia inathibiti kwamba, Uislam uliosababishwa kwa njia hii ya ushetani, ujahilia na kwa mtazamo wao wa kidunia, umesambaza fikra kwamba maulamaa wa Kiislam na Waislam kwa ujumla hawapaswi kujihusisha kwenye masuala ya kisiasa na kijamii. Pia, hawapaswi kujibidiisha, kufanya juhud katika masuala ya Waislam na wapuuzie hukumu zilizo dhahiri zinazokubalika katika Qur'ani na hadithi.

مَجَارِيُ الْأَمْوَرِ بِبَدِ الْعُلَمَاءِ بِاللَّهِ

“Uwezo wa kazi upo katika mikono ya wasomi wa mambo ya kimungu.”
(Kitabu: Tuhfi al 'Uqool: uk. 271).

وَ أَمّا الْحَوَادِثُ الْوَاقِعَةُ فَارْجِعوا فِيهَا إِلَى رُوَاةِ
 أَحَادِيثِنَا

“Na kwa hakika katika matukio ya kweli rejeeni kwa wapokeaji wa hadithi zetu.” *(Kitabu: kamalud-Diin, Juz. 2, uk. 484)*

Na hadithi nyingine za msingi au zisizokuwa na sura ya udanganyifu, na zinathibitishwa kwa asilimia mia moja.

Ni vyema maulamaa na Waislam wenye mwamko waache kughafilika, wafunge sera za kishetani na wasifungue njia za uporaji

ufanywao na wenye mamlaka. Wao ambao wamekuwa wakiungwa mkono, wana nini katika Uislam? Wanaouogopa Uislam wa Ali bin Abi Twalib (a.s)?

Ikiwa wale walikuwa mashahidi **kutokana na maradhi yao ya kupenda uislam, na** walikuwa wanautambua Uislam kwa dhati; na ikiwa hao wanaodhania KUWA, Uislam ni kukaa majumbani mwao kumwabudu Allah (s.w.t) tu, hawana jambo jingine la kufanya isi-pokuwa kuelekea msikitini tu na kurudi nyumbani:laiti kama ingelikuwa hivi, basi kusingetokea vita vya Siffiin, Nahrawani wala vya Jamal, na wala Waislam wasingeuawa makundi kwa makundi vile na wakawa mashahidi.

Laiti Bwana wa Mashahidi – al-Imaam Husein (a.s) - an-gekuwa na fikra kama hizo, angekaa tu karibu na kaburi ya babu yake (Mtume (s.a.w.w) akidhikiri na kusoma dua tu, basi, tukio la Karbala lisingeweza kutokea, maswahaba zake na wapenzi wa Allah (s.w.t) wasingelikatwa vipande vipande. Waja wa Allah (s.w.t) wasingelichukuliwa mateka, na juu ya yote hayo, kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w) angelikuwa na fikra kama zao, kutokana na kazi hii ya kuhubiri na kubainisha hukumu za kiibada, basi asingeliweza kufikwa na mateso na mashaka yaliyomfika na Waislam wote wale wasingelikufa shahidi.

Tukirejea upande wa maulamaa wetu wa zama hizi, marehemu Ayatullah Mirza Muhammad Taqii Shirazi - Allah amsamehe - kwa nafasi kubwa aliyokuwa nayo katika elimu na uchamungu, pia an-gekuwa na fikra kama zao, basi kusingetokea vita baina ya Waislam nchini Iraq na wavamizi wa Kiingereza. Waislam wote hao wasingelikufa mashahidi na uhuru wa Iraq usingelipatikana.

Tawala zilizopo katika zama hizi, kwa moyo na kwa jina la Uislam, zimekuwa zinaitumikia Marekani ili ziweze kuongoza kwa maslahi yake ya kidunia.

Maulamaa ambao pia ni wajumbe katika mamlaka za kifalme hawana habari juu ya Allah (s.w.t), wanawaunga mkono wafalme hao, wanapinga utawala wa Kiislam, wanafanya juhud za kuwadhulumu Waislam, kuleta uchokozi kwenye Utume wa Mtume Muhammad (s.a.w.w). Wanauarifisha Uislam kuwa ni wa kifalme, usiokuwa na mipango, ambao una nia ya uhalifu na ukatili. Wanalamika dhidi ya dhulma za Marekani na Israili kwamba wanataka kuwatenganisha katika faradhi za Hijja. Uislam huo ni lazima uthibitishwe na Umoja wa Kisovieti, Marekani na Israili.

Mimi nina imani kwamba ikiwa mwanadamu ataishi kwa taabu na dhiki zote, akaishi kwa kutumia mali yake mwenyewe, aka-jitegemea mwenyewe maisha yake yote, akala mkate wake, hiyo ina thamani zaidi ya mamia kuliko mtu akakaa katika ghorofa kubwa (*apartment*) na akanyoosha mkono ili awasalimie wengine.

“Kwa Hakika mbele ya Allah hii ni taabu juu yao kwamba waliona dhulma, uchafu, na rushwa waziwazi lakini hawakuwa ni wenye kujataza, hii ni kwa sababu ya tamaa zao za kupata chochote, kuogopa mateso, na mashaka kutoka kwao.” (*Tuhf Aluqool*, uk. 271)

Pia Allah (s.w.t) anasema katika Qur’ani Tukufu kuwa:

“Msiwaogope watu, na niogopeni mimi.” (Surat Al maidah: 44)

Uoga wa nini? Hakuna cha zaidi isipokuwa kuwaweka jela, kuwafukuza nje ya nchi na kuwaua. Mawalii wetu walitoa maisha yao kwa ajili ya Uislam, ninyi pia ni lazima muwe tayari kwa ajili ya masuala haya.

Nafafanua kwamba, msingi wa kuwepo vikwazo na matatizo yampatayo mwanadamu tangu zama za Nabii Adamu (a.s) hadi leo na kuanzia leo hadi Siku ya Hukumu (Kiyama) - hii ni siku ambayo yote yaliyompata mwanadamu na wote walioathirika

kwa rushwa, dhulma, vita, kutawaliwa na yote hayo - yatakuwa dhahiri na wazi

Yote haya yanayojitokeza msingi wake mkuu ni kupenda nafsi, kama utaangalia vizuri, utaona kwamba matawi yake yanatokana na kutegemea upendo na kujionesha.

Kujionesha huku makao yake makuu ni kuipendelea nafsi (mata-manio ya nafsi) ambayo ndiyo yaliyompeleka mwanadamu kwenye uhari bifu na kuua. Mitume walikuja kuleta mageuzi, kurekebisha pamoja na kuleta usawa.

Kujionesha, kupenda nafsi, uongozi, nafasi, ushindani na yote haya yalikuwepo tangu mwanzo wa dunia hadi sasa na yalitumika katika tawala zao ambapo msingi wake mkuu ulikuwa ni kupenda nafsi.

Kama mataifa ya Kiislam na Waislam, badala ya kutegemea **vitalu** vya mashariki na magharibi, wangetegemea Uislam na mafundisho ya nuru ya Qur'ani na kuwa ni sehemu ya kufungama-na nayo katika maisha yao, na kuifanyia kazi, Lakini, kwa bahati mbaya leo hii tumekuwa mateka wa ugomvi (uchokozi), na mzuka wa kutisha wa Marekani, na kuhadaika na kuona kuwa Wasovieti si wabaya kwao.

Kuwa mbali na Qur'ani Tukufu kwa mataifa ya Kiislam ndiko kuli yofanya weusi na taabu ya Waislam na nchi za Kiislam kwa ujumla na kwa kupitia matumizi na marekebisho ya sera za kisiasa ndiko kulikotuweka kushoto na kulia.

Viongozi Ndio Kilele cha Uislam

Sisi na wewe, angalau katika miaka mia moja mingine, taratibu tu-jaribu kufungua miguu ya mamlaka zote kubwa zenye nguvu za Ki-

islam na nchi nyingine changa. Kwani, tumekuwa tunashuhudia wenyewe, au kama tulivyosimuliwa katika historia zenyе usahihi ndani yake kuwa, hakuna hata nchi moja kati ya hizi zikawa na uhuru wa kifkra na ustawi katika mataifa yao kutokana na tawala za serikali hizi.

Bali, takriban wengi wao wameangukia kwenye ukatili, ukandamizaji wa watu wao na kila walichokifanya kilikuwa ni kwa ajili ya maslahi binafsi, au kikundi, au kwa ajili ya kuwastawisha matajiri, kuwa katika matabaka ya wote walioonewa, kupata vikwazo na kuzaa hata maji, mkate, uzima na nguvu.

Ni huzuni iliyojе kwa maskini hawa, wamekuwa wanafanya kazi ya kunufaisha maslahi ya maisha ya matajiri. Au kwamba, nguvu zilizotumika zilikuwa ni za kuwaweka na kuwafanya wawe tegemezi kwa nchi na watu fulani kwamba, kila kinachopatikana kilikuwa kinatumiwa na nchi mbalimbali kwa ujanja na hila tofauti, kuwafanya soko la mashariki na magharibi kwa maslahi yao na kuyafanya mataifa haya kuwa yanatumiwa na yabaki nyuma. Hadi sasa hali hii bado inaendelea.

Tawala zote hizi waliona kuwa nguvu ya Uislam ina madhara. Baadhi yao wanasema wazi kwamba, nguvu ya Uislam ina madhara, na baadhi yao wanasema ulimwengu wa Kiislam tuliookwa nao sisi ni kinyume. Wao wanataka mfano wa Uislam wa Saudia.

Ukimya na maelewano na Israeli

Ewe Allah! Tawala hizi zisizoelimika pamoja na uwezo wote walio nao kuwashinda wakoloni, uhalifu wa Marekani na Israeli unatumiwa kuwa ni msingi wa kuimarisha kufuru zao usiku na mchana, lakini wenyewe hawaelewi.

Ewe Allah! Waislam na wanaoonewa waokoe kutokana na dhulma hizi. Lakini ni nini sasa tunapaswa kufanya? Je, maandamano na

kupaza sauti kunatosheleza kuutoa Uislam kutoka mikononi mwa maadui? Je hii ndiyo njia ifaayo, Au hakuna lengo?

Ingawa serikali **hizi bado zinaendesha vitendo vyao vya ukandamizaji**, pia wamekuwa hawavumulii vilio hivi, muwe na uhakika kwamba vilio vya wanaaoonewa na waathirika wa haki iliyosahaulika wamekuwa wakinyongwa. Na wale ambao hadi wakati sasa wanaalia kutowana na dhulma, ambao mara moja kila mwaka, huzunguka Kaaba wakiwa wanatarajia kupaza sauti zao wanapokuwa kwenye mikutano ambayo misingi yake ni ya kisiasa, juu ya mambo kisiasa yaliyoasisiwa, wamekuwa wakipata upinzani.

Uislam na Mtukufu Mtume, Mkuu wa Daraja (s.a.w.w) na shujaa na shahid wa mihraab, ambaye aliuawa na damu yake ikamwagika ardhini katika usiku Mtukufu wa Lailatul Qadr, utukufu huu umezikwa wapi ambapo viongozi wa miji ya Kiislam wanasema ingeni kwenye maumivu na mateso, wala msilie na kuweni chini ya mateso na uchafu wa Marekani na Israeli.

SEHEMU YA SITA

Kuulinda Uislam Safi dhidi ya Uislam wa Kimarekani

Utangulizi Mfupi Juu ya Watetezi Wawili wa Kiislam

Kitu pekee ambacho mnapaswa kufikiria na kukithibitisha ni misingi imara ya Uislam Safi wa Muhammad (s.a.w.w). Uislam ambao washika bendera wake ni maskini. Wanaodhulumiwa na mafakiri duniani. Adui zake ni makafiri na wawekezaji wa kibepari wanaoabudu pesa.

Uislam una wafuasi halisi siku zote. Unajinyima mali na uongozi. Maadui zake halisi na wa kweli ni wadanganyifu (wajanja), watawala wa kimabavu na kinafiki.

Mamlaka kuu za kinyang'anyi mionganoni mwa jamii ya watu huwa na mitazamo bandia, fikra tofauti za kitaifa, kiroho na kuon-ekana kwamba wana nafasi ya kufaa **kutengwa**. Zote zimejaa hatari na zinaleta madhara. Kumbuka kwamba, wakati mwingine kwa mia-ka thelathini, arobaini, pamoja na sera ya Uislam, utukufu au uzalendo, kutumia ujanja mwingine pamoja na kuishi kwa uvumilivu na kuvumiliana baina ya mataifa wanakuwa wanatekeleza majukumu yao katika wakati mwafaka.

Mapambano makubwa katika Uislam wetu yamekuwa ni cheche katika suala hili. Lakini hadi sasa, vyuo vya kidini vimefikiria kujichanganya katika maeneo yote mawili. Ni lazima wawe makini katika wazo la kutenganisha dini na siasa, na masuala haya haya-paswi kuambukizwa kuanzia chimbuko la wanafikra hadi kwa vijana wasomi.

SURA YA KWANZA

Watetezi wa Uislamu Safi

Wanaoonewa na wanaodhulumiwa

Maskini na mafakiri walio vijijini wamekuwa mstari wa mbele katika jamii. Hawa wakaao vichakani, mijini na wale waliodhulumiwa ndiyo hao ambao wametufikisha kwenye matunda haya ya mapinduzi. Hawa walikuwa watu waliojitelea kila kitu chao kwenye njia ya Uislam na sasa ni wote wanaoshughulika. Hawa hawa, hivi sasa ndiyo wapo mstari wa mbele wakijitelea na vijana wao ndio wanashughulika nchini kote, ndani na nje ya nchi wakiueneza Uislam.

Taifa tukufu la Iran lina idadi kubwa ya vijana na familia kubwa. Kwamba vijana hawa, ndio waliokabidhiwa jamii na walimtegemea Allah (s.w.t) kwa kila kitu na ikhilaswi ilikuwa ni mwongozo wao. Kama wasingelikuwepo, jamii hii iliyokuwa katika uonevu na iliyofungamana na dunia ingeendelea na hali iliyokuwa nayo. Kama utetezi huu usingelikuwepo, utetezi wa wanyonge, utetezi wa wanaoshi vijijini, utetezi wa kusini mwa miji, vyote hivi visingelikuwepo. Basi, kusingelikuwa na mapambano dhidi ya dhulma wala sisi tusingeliweza kukabiliana na matatizo wala kusimama imara dhidi ya matatizo.

Mustadhaafin ndio Wasaidizi wa Harakati za Mitume

Dini zote zilifanikiwa kuuangusha uovu kutokana na msaada wa mustadhaafin ambao walisimama kidete dhidi ya uvamizi wa mabepari. Historia inatueleza kwamba mustadhaafin walisimama kidete kuwasaidia Mitume wa Allah (s.w.t) kupambana na dhulma. Katika

Uislam, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisimama akiwa mionganini mwa mustadhaafin, akawapa msaada mustadhaafin, alikuwa makini na akawashinda mabepari wa zama zake.

Mabepari (wawekezaji), matajiri, waishio kwenye mahekalu hawana nafasi katika Mapinduzi

Wale waliokuwa nje ya nchi walikuja ili wachume matunda. Ndiyo wale waliokaa juu tangu hapo mwanzo, wakiangalia hali ya hewa (mazingira), au wakitoa msaada ili kudhulumu, sasa wamekuja kwa sura ya kimapinduzi. Hamjawakubali na wala hatujawakubali. Ndio wale waliochukua kalamu ya sumu na wakaandika vibaya dhidi ya Uislam.

Hadi sasa wamekuwa wanashughulishwa na mtu mwenye cheo na nafasi. Yaani, vyeo vyote viko chini yao. Au kwa wale matajiri, napenda kuwabainishia kwamba hakuna wawekezaji hata mmoja mpaka sasa aliywahi kuuliwa. Kila aliyeuawa, basi huyo ni muuza mkaa, muuza majani na mkulima. Hii ni nini!

Hili ni taifa ambalo ninyi ndiyo mliowaokoa na kuwaacha huru watumwa. Leo hii hakuna kikwazo wala utumwa katika nchi yoyote ile. Hakuna kujitoa kwa wengine. Leo, nchi isiyofungana na upande wowote ni Iran, huwezi kupata nchi nyingine kwa maana ya kweli na hii ni kutokana na baraka za watu waishio vichakani. Hili lilikuwa ni **darasa (gome)** la unyanyasaji. Hili ni darasa la unyanyasaji kwa vijana wote tulitotoa. Waje kuwahesabu, ni watu wangapi kati ya hao ni matajiri, ni wangapi kati yao sasa wamekaa na wanaisema vibaya Jamhuri ya Kiislam, Kati yao ni wangapi walienda vitani? Wametoa mashahidi wangapi? Kama mtampata mmoja basi huyo mmoja wao ni mwadilifu, inawezekana. Inawezekana kuwa mmoja wao katika nyumba yake atakuwa amejawa na

jazba kwa ajili mapenzi ya Allah (s.w.t) na akatoka. Lakini haya ni kidogo.

Viongozi Wanao Wajibu Mkubwa Kuwatumikia Mustadhaafin

Napenda kulisua Bunge, Serikali na wahusika wake wakuu kwamba; wanapaswa kutambua ukubwa wa taifa hili katika kutoa huduma hususan kwa walioonewa na waliodhulumiwa. Jueni kwamba, hawa ni nuru ya macho yetu na Mawalii wote ni neema ya Jamhuri ya Kiislam. Imewaletea njia wao na kujitolea kwao wametafuta kuutambua ukweli na maisha yake ikiwa ni pamoja na wajibu wa kuahudumia. Kamwe msiiachie na mtambue kwamba wao wametokana na watu na wale wametokana na wao.

Ni kweli, ulikuwa ni wakati ambapo maskini, wanavijiji na tabaka la kipato cha chini katika jamii yetu walikuwa wamejaribiwa kwa kiasi kikubwa, **na kutoa vijana na wapenzi wao** kadhaa waliokuwapo katika kila eneo la maisha, na Inshaallah, watakuwepo. Mnajitolea katika njia ya Allah (s.w.t), basi ni kwa nini tusiwhudumie watu hawa wenye ikhlaas ya kweli. Hebu tujivunie na ubinadamu huu wa heshima ya hali juu uliojaa ushujaa wa kihistoria.

Maulamaa halisi waliochukua ahadi

Maulamaa na wasomi wa dini wapo kifua mbele kupambana na kila risasi yenye sumu itakayoelekezwa upande wa Uislam kwa mapenzi waliyokuwa nayo juu ya Uislam, basi, wao wapo tayari kuchinjwa ili kuutetea Uislam.

Ahadi ya kwanza iliyokuwa muhimu sana ilikuwa katika kipindi cha mapambano ya umwagaji damu siku ya Ashura sawa na tarehe 15, Khordad. Ni kielelezo kamili. Siku hiyo ya Khordad 15, watu 42 walipambana kwa bunduki na risasi dhidi ya jeshi la Shah na

kwamba, kama wasingelikuwepo hao tu, basi ingelikuwa si rahisi kupambana.

Katika kipindi hicho, hakuna hata siku moja iliyopita bila ya kutokea tukio lolote, kwa kificho na kwa dhahiri. Marekani na Shah walikuwa wakifanya uchochezi, kashfa na **kuleta** fitna, hata kwa wasioswali, wazungu, na Wakomunisti **ili wapambane na** watu wote walikuwa wakiwajibika katika kuendesha kampeni ya uongofu.

Kwa kweli maulamaa halisi na wenye ikhlaas peke yao ndiyo waliokuwa wakilia. Kwamba, ni viyi Marekani na kibaraka wake Pahlavi wanataka kuondosha mizizi ya imani na Uislam wakati baadhi ya maulamaa watukufu hawana habari, au wametawaliwa na michezo ya kidunia, na baadhi yao wamekuwa wana matumaini na nyuso zao zimeng'ara mara baada ya ushindi.

Taifa la Kiislam mnapaswa kutambua kwamba huduma ambazo zinatolewa na maulamaa wa dini kwa nchi za Kiislam katika historia nzima imekuwa si ya kuhesabika. Katika zama za hivi karibuni, wamekuwa na kazi ya kuokoa nchi kutokana na kuanguka kwa baadhi ya marja'a (viongozi wa dini) waliobeba majukumu na juhud walizokuwa nazo maulamaa.

Vyuo vikuu vya kidini na maulamaa wakubwa siku zote wamekuwa wanahifadhi, wanalinda uhuru na uadilifu wa nchi za Kiislam. Wanatoa huduma, wanatumikia na wanaleta msukumo kwa ajili ya amani katika Uislam. Walikuwa na jukumu la kulinda na kudumisha nidhamu (sheria) za nchi na vikosi vya usalama, ingawa hakuna yeyote aliyekuwa na tatizo la kutojua bajeti ya nchi. Kwa MTAZAMO WANGU, mahaini hawa ni lazima wasambaratishwe!.

Wao wanao usoefu wa muda mrefu sana na wenyewe wanatambua kwamba maulamaa wakubwa wa Kiislam na wahadhiri watukufu, pamoja na jitihada zao endelevu kwa Mataifa na kwa manufaa

ya Uislam na Qur'ani, kamwe hawatatishika kwa vitisho na hongo kwa manufaa ya mifumo ya hila na unyang'anyi, **bali wataendelea kuwa na nguvu ya kulinda misikiti na jamii** kwa kutoa huduma za kiroho na Uislam.

Iwapo baadhi ya maamuma, wasio na hadhi, walioghafilika katika neema za Allah (s.w.t), watachukua hatua kwa manufaa ya mfumo wa hila, basi hii itakuwa ndiyo sababu ya vyuo vya kielimu na jamii za Kiislam kujitia hatarini hadi pale watakapokata ndoto zao hizi za udanganyifu. na itakuwa ni jukumu kwa maulamaa wakubwa na mubalighina (walinganiaji) na kuupeleka Uislam kwa vitendo na kuifanyia kazi misingi ya imani na kuwafikisha katika kusudio lake ambalo ni kuuondoa ukoloni na KUZIMA moto ulioshika katika nchi zote na kuzishughulikia nchi za Kiislam ambazo bado ziko nyuma.

Mataifa ya Kiislam lazima watakuwa wameipokea dalili na sababu ya kweli, kwamba, kwa nini nchi ya Iran wanao akina **Mutwahhari**, akina **Behesti**, **Mashahidi madhabahu** (mihrabu) na maulamaa wengine? Na nchini Iraq wapo akina **Sadr**, na akina **Hakimi** na Lebanon kuna akina **Raghib Harb** na akina **Karimi**. Pakistani utawaona kina **Arif Huseini** na maulamaa kutoka katika nchi zote za Kiislam ambao wana uchungu na Uislam Safi wa Muhammad (s.a.w.w), wanafikia kwenye lengo na hatimaye wa-nauawa?

Maulamaa na Kupinga Mawakala wa Ukoloni

Uislam na madhehebu tukufu ya Ja'far ni kikwazo kwa ukoloni na ndio madhehebu pekee inayokabiliana na ukoloni. Iwe kushoto ama iwe kulia, ni maulamaa ambao ndiyo wanakihifadhi kikwazo hicho. Na kwa juhudi hizo, kamwe mkoloni hawezi kwa vyovyyote atakavyo, kuishi katika nchi za Kiislam hususan kwa nchi kama Iran.

Kwa karne sasa, wamekuwa wakijitahidi kuuharibu utaratibu huu kwa hila mbalimbali.

Mimi nina yakini na ninashuhudia kwamba, kama tungewatanguliza mbele watu ambao si maulamaa kwenye harakati hizi za mapinduzi na wangkuwa na maamuzi juu ya jambo hili, basi leo hii kusingelikuwa na chochote kile isipokuwa aibu, unyanyapaa na maumivu (madhara) kutoka Marekani na washirika wake na kisingelibaki chochote kile, bali ni upotoshwaji wa imani ya Kiislam na mapinduzi yenywewe.

SURA YA PILI

KUUTETEA NA KUUHAMU UISLAMU WA KIMAREKANI

Mnaweza kuona kwamba, mojawapo ya makundi ni hili ambalo kwa sasa linaudhihirisha Uislam. Wengi wenu kati yenu ninyi pia mmekuwa mnaudhihirisha Uislam. Kwamba, idadi hii ya watu waliokuwamo katika Uislam, ikiwa wao pia watautaka, basi si ule Uislam alioutangaza Mtukufu Mtume (s.a.w.w), bali ni kitu kingine. Ufunuo (aya) wake wautakao ni kuufanya uwe na mtazamo mwininge, Jeshi lote liwe kinyume na kuwa chini ya mafanikio na matakwa yao. Miongoni mwa watu hawa ni wengi sana, kati yao wapo wanadolitamka jina la Uislam. Pia, wengi mno huwa wanaujali na kuwa na uchungu na uislam, hata kama watakuwa na uchungu nao basi ni kwa ajili ya huo uislam wao na si kwa ajili ya uislam wetu wa kuuonea huruma uislam. iwapo wataona huruma hiyo ni kwa ajili ya Uislam, lakini wao wenyewe hawapo kwa ajili ya Uislamu wetu.

Kuna baadhi yao pia hawana kabisa imani na Uislam. Hata kama hawatakuwa na imani na mapinduzi haya, lakini, kwa asilimia mia moja, wamekuwa Waislam na wanamapinduzi. Je, hivi sasa unaweza kumpata mtu mmoja ambaye atawaambieni kuwa Mimi si mwanamapinduzi? Wote pia watasema kuwa sisi tulikuwemo tangu mwanzo. Wote ambao sasa hivi wanakuja watasema kuwa sisi pia tulikwenda kifungoni. Nini tumefanya katika zama za ujahilia? Tuli-fanya upinzani. Lakini, haya yote hayapo kwenye nafsi zao.

Hawa sasa wanauhofia Uislam. Tena, wana wakati mgumu sana wa kuuogopa hali ya kuwa Uislam ni mwema kwa ajili ya wote. La-

kini, hofu yao ni ya vitendo vyao vya khiyana, ndiyo maana wanaouna Uislam sio mzuri. Hakuna dini yoyote ya tawhiid itakayosema Uislam si mzuri. Uislam unapingana na mahaini. Kinyume chake ni kwamba, vijana wetu wameondoa uharibifu kwa jina la Uislam. Kupanda kwa jina na ubora wa nchi yetu, kwa jina la utamaduni, wote hawa pia wanaseema Uislam. Kama ustaarabu mkubwa; ni uthibitisho kwamba jina la ustaarabu mkubwa ndiyo ulioifikisha nchi yetu hapa tulipo, ambao kwamba, hivi sasa wote umejikusanya na kamwe hawawezi kuufanyia marekebisho.

Pia, hawa wanataka jina la Uislam litumike katika kila eneo la maisha ya kila siku, hata kwa mambo ya kimaada (kidunia), basi yafikishwe kwa jina la Uislam.

Watawala ni Watetezi wa Uislam wa Kimarekani

Ukweli ni kwamba, katika kipindi cha ukoloni wa mashariki na maghari, hususan serikali ya Marekani na umoja wa Kisovieti, dunia waliigawanya sehemu mbili: Huru na Karantini ya kisiasa.

Katika sehemu ya ulimwengu huru, wakoloni hawa walikuwa ni watu wasiotambua chochote kuhusu mpaka wa kisheria na wakiukaji wa maslahi ya watu wengine na unyonyaji, utumwa, na ukoloni kwa mataifa kuwa ni agizo muhimu, ukamilifu wa haki, na busara inayoendana na kanuni zote na viwango. Umoja wa mataifa unatambua.

Lakini, sehemu ya karantini ya kisiasa, kwa bahati mbaya wengi wao ni mataifa maskini, hususan ulimwengu wa Kiislam. Katika hao wapo waliokamatwa na kuwekwa jela, hawakuwa na haki ya maisha wala kudhihirisha maoni yao, sheria, kanuni na fomula zote ni zile zilizokuwa tayari zimekwishaandikwa kwa matakwa yao na mifumo waitakayo na ni ile yenye manufaa ya kikoloni.

Kwa bahati mbaya, watendaji wengi wa sehemu hii ni watawala wale wale wasiojua au wale wote wanaofuata mistari ya kikoloni ambayo, hata kama utapiga mayowe kutokana na maumivu, licha ya hivyo, pia iwapo utapatikana na hatia au uhalifu wowote, huwa ni dhambi isiyo na msamaha na hatimaye kufungwa, kuwa ndani ya minyororo na kuuawa, hakuna mtu yejote atakayekuwa ana haki ya kusema neno.

Tangu hapo awali, ulimwengu wa Kiislam ndio umekuwa sababu ya kukandamizwa, kufungwa, kunyongwa na kutokuwa na uwezo wa kubainisha na kusema majanga yatokanayo na tawala zilizokuwapo katika nchi zao. Wanapaswa wawe na uwezo wa kupata huruma na amani ya Allah (s.w.t). Pamoja na kupata uhuru kamili, kuwa na uhu-ru wa kujielezea majanga na machungu wayapatayo na hata Waislam wengine pia wapate njia kwa ajili ya kupata ushauri na fikra zaidi.

Hivyo basi, kutokana na mambo haya, tunapenda kusisitiza na kuwaendeleza Waislamu kwamba angalau wangeitumia nyumba Tu-kufu na yenye wingi wa amani ya Allah (s.w.t) ili wawewe kuondoa vikwazo, utumwa, na dhulma. Jambo kubwa la msingi kwetu ni ku-tangaza kujitoa na kwa njia yoyote ile, nyumba hii (Kaaba Tukufu) itumike kwa ajili ya kujikomboa.

Viongozi na wanaoongoza makundi ambao wanataka kuongoza Waislam kwa jina la Uislam ili wadhoofishe misingi ya Uislam na vijana, wao wamewekwa kama mtego. Hawana habari yoyote ile inayohusu Uislam wala hawajui shabaha ya kanuni zake (Uislamu). Kwa kusoma aya chache kutoka katika Kitabu cha Allah (s.w.t), iba-ra fupi kutoka katika *Nahjul Balaghah* na tafsiri za kijahilia na zenyе makosa haitakufanya uujuue Uislam.

Kazi yao ni kugeuza Aya Tukufu na ufafanuzi wake. Aya na sen-tensi zinazoelezea wazi, zilizo na upinzani dhidi ya itikadi yao huzi-

kanusha. Kwa kweli hutegemea Qur'ani na *Nahjul Balaghah* kwa kuuponda Uislam na Qur'ani, wafungue njia kwa ajili ya viongozi wao wa kimagharibi na mashariki. Nyinyi vijana wapenzi na rasili-mali za nchi, muhamasike kwa ajili ya maslahi ya nchi yenu.

Wote mnapaswa kuwausia vijana ambao tayari wameshadang-anyika na mambo ya kinafiki na mfano wao huu, muwaite, muwarud-ishe kwenye haki, na lazima muwafahamishe kwamba kuwa kwao dhidi ya Jamuhuri ya Kiislam ni sawa na kupambana na Uislam. Wao kupambana kwa jina la Uislam ni kuusambaratisha Uislam.

Kuendeleza Dhulma na Dhambi ni Kuharakisha

Kutokeza Imam wa Zama (A.J.F.S)

Kundi moja linasema kuwa; sawa! Ni lazima ulimwengu uwe ume-jaa maasi hadi Imam wa Zama (a.j.f.s) aje. Tusikataze maovu wala kuamrisha mema ili kila mtu afanye atakalo. Madhambi yatakapozi-di ndipo faraja itakapokuwa karibu.

Na kundi jingine, ambalo lilikuwa ni la juu zaidi, nalo linase-ma; anatakiwa kuchangia dhambi, waite watu kwenye dhambi ili ulimwengu wote ujae jeuri na dhulma ndipo Mtukufu Imam (a.j.f.s) atakapokuja. Hili pia lilikuwa ni kundi ambalo ingawa mionganoni mwao mlikuwa na wahalifu, mlikuwa na watu wenye nyoyo nyepe-si, na pia kulikuwa na watu waliokuwa na madhumuni ya kuchangia katika jambo hili zima la maasi.

Hii ina maana ya kwamba, tufanye maasi ili Imam Mtukufu wa Zama (a.j.f.s) aje, na ikitokea kwamba Imam amekuja, anakuja kwa ajili ya nini? Anakuja kwa ajili ya kueneza uadilifu, kwa ajili ya kui-marisha serikali (utawala), kwa ajili ya kuondosha ufisadi. Sisi tupo dhidi ya aya tukufu ya Qur'ani na tumeacha kazi ya kukataza mao-

vu, na tumeacha kuamrisha mema, tuusie na tuyaondoe madhambi ili Imam aweze kuja. Imam akija, anakuja kufanya nini? Anakuja ili afanye kazi hiyo hiyo. Je, sasa hivi sisi tena hatuna wajibu wowote? Je, watu tena hawana wajibu wowote? Bali, wajibu wake ni huu kwamba kuwaita watu kwenyadi.

Kundi jingine lilikuwa likisema kwamba; linasubiri faraja, na hii ni kwamba sisi tusiwe na kazi yoyote ile, kwamba; nini kinapita katika ulimwengu huu, nini kinatokea katika mataifa, sisi tusifanye chochote kile, tutekeleze wajibu wetu wenyewe, na Imam mwenyewe ndiye atakayezuia na kurekebisha kila kitu. Hivyo, sisi hatuna jukumu lolote lile. Wajibu wetu ni kukaa, kusoma dua, kuomba yeye aje na sisi tusijishughulishe na lolote linalotokea katika ulimwengu au katika nchi yetu. Hili nalo lilikuwa ni moja ya kundi ambalo watu wake walikuwa ni wema. **“Kama Imam (a.s) mwenyewe anajua fika, kwamba inambidi aje.”**

Mmoja kati ya maulamaa (Allah amrehemu) anasema hivi:

“Mimi moyo wangu wala hauungui kabisa kwa Uislam na Mtukufu Imam wa zama (a.j.f.s) vyema yeye anaona hili, yeye mwenyewe anakuja, basi kwa nini mimi nifanye?”

Hizi ni mantiki za watu ambao wanataka kupita chini ya mbawa wakimbie. Haya yote Uislam hauyakubali, hauhesabu chochote katika haya. Hawa wanataka kukimbia kupertia chini ya mbawa. Wanataka kufanya jambo moja; riwaya mbili wachukue moja kutoka upande huu na nyingine upande ule, kwamba hakuna:

**“Kwa mfano, wekeni uhusiano mzuri pamoja na wafalme,
waombeeni dua wafalme.”**

Huku ni kwenda kinyume na Qur’ani. Hawa hawajaisoma Qur’ani. Iwapo wataleta aya mia moja kama hizi zitupieni ukuta-

ni, ni tofauti na Qur'ani, ni tofauti na sira ya Mitume. Pamoja na kwamba hii si riwaya, ninyi wakati mnapotafakari riwaya hizi zote kwamba, iwapo mtu atakuwa na haja ya kufanya haya, ni riwaya ambayo atakuwa na nia ya kuishi kwamba, huyu ni sultan, wewe utakuwa upo pamoja naye.

Ikiwa Waislam watakuwa na nia wawe na maisha mamoja na kufanya dhulma, kuua mtu, kuwa na mahusiano na mtu ambaye ni muuaji wa watu, ambaye ulimwengu mzima anaua, ni kiasi gani maulamaa wetu wakubwa hadi sasa wameshauawa? Ni wangapi wamefungwa? Ni wangapi wamefukuzwa? Watoto, Uislam ndiyo huu! Huyu ndiye Muislam. Muislam kama hutotaka kujibidiisha na masuala ya Waislam, basi si Muislam.

**لِيْسْ بِمُسْلِمٍ "مَنْ أَصْبَحَ وَلَمْ يَهْتَمْ بِأَمْرِ الْمُسْلِمِينَ
فَلِيْسْ بِمُسْلِمٍ"**

**"Syo Muislam ambaye ataamka bila ya kutilia umuhimu mambo ya Waislam, basi huyo si Muislam." Hata kama atatamka shahada,
yaani: لا إله إلا الله.**

Nafasi na Mitazamo Tukufu ya

Mtume (s.a.w.w) na Maimam (a.s)

Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), anasema kwamba;

"Mataifa (makabila) mawili yamenivunja kiuno changu (yanausam-baratisha Uislam) maulamaa ambao ni mafasiki na jahili (mjinga) ambaye haujui ujahili wake."

Na sijui Uislam utaumia zaidi kutoka katika taifa lipi? Je, kutoka kwa ulamaa fasiki au jahili asiyejijua? Hata hivyo, yote mawili yanauumiza Uislam. Na haya yote yapo, yatakuwepo baadaye na yatakuja hata katika kipindi cha kudhihiri kiongozi wa Zama, Mtu-kufu Imam Mahdi (a.j.f.s)

Waislam Kutengwa

Leo hii, Iran inawatenga baadhi ya maulamaa wafuasi wa kiongozi wa nchi na Waislam wa Iran. Hawautambui Uislam kwa kuwa wao na Marekani wanakhilitafiana, na ni uhalifu gani zaidi ya huu na ni kitu gani ambacho mtu kitamtoa katika Uislam zaidi kuliko hili? Ni kwa yejote kuwa na ujasiri dhidi ya Marekani na Israel! Hiki ni kikwazo chenu Waislam.

Hadi sasa, kitu ambacho ni maeneo ambayo hayajazingatiwa au kufanyiwa uchambuzi wa kina na yanayoabisha ni falsafa ya Hijja iliyochorwa. Kwamba, Hijja ni moja ya ibada ya pamoja, ni moja ya safari ya kiziara na ya kitalii. Katika Hijja ni namna gani unapaswa kuishi, vipi unapaswa kupambana na kwa namna gani utakabiliana na mabepari wa dunia na Ukomunisti uliosimama!

Katika Hijja ni jinsi gani haki ya Waislam na wanyonge inapaswa kusimamiwa kutoka kwa madhalim! Kile kilichokuwa lazima katika Hijja ni shinikizo la kimwili na kisaikolojia kwa Waislam ili kupata ufumbuzi mbadala wa kufikiri!

Kilichokuwa lazima katika Hijja ni kuona kwamba Waislam ni nguvu kubwa na yenyewe uwezo katika ulimwengu wa tatu inayotakiwa kulimdwa!

Katika Hijja, Waislam wanatakiwa wawe dhidi ya serikali tege-mezi zinazojiosha. Lakini pia ni jambo la kushangaza kuwa Hijja hiyo hiyo imekuwa ni safari ya kutembelea na kuona Kibla na Madina tu.

Allah (s.w.t) na Mtukufu wa daraja Mtume (s.a.w.w) katika siku kubwa ya Hijja waliita na kupaza sauti kubwa kwamba wao, Allah (s.w.t) na Mtume (s.a.w.w) wamejitenga na washirikina;

وَ اذْنٌ مِّنَ اللَّهِ وَ رَسُولِهِ إِلَى النَّاسِ يَوْمَ الْحَجَّ
الاَكْبَرِ أَنَّ اللَّهَ بَرِّي مِنَ الْمُشْرِكِينَ وَ رَسُولُهُ

**“Na ni tangazo litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake,
kwa watu siku ya hija kubwa kwamba Mwenyezi Mungu (yu mbali
nao).” Suratul Tawba: 3.**

Siku hiyo itumike kuwaondoa Marekani na maulamaa ambao ni maofisa wa baraza la Mfalme wa nchi, kwamba wao wanasaidia kumnufaisha Shetani Mkubwa, wanatoa fatwa (Allah (s.w.t) ae-pushie mbali) kuwa Allah (s.w.t) na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) wako kinyume na mila za Hijja na wameamuru kuwa mbali na masuala haya.

Siku ambayo Walii wa Allah (s.w.t) na Imam wa Zama (a.j.f.s) atadhishiri katika Kaaba Tukufu, atatoa wito, tena wa uadilifu na kutoa ukelele wa kupinga dhulma na ukafiri. Maulamaa wale wale am-bao walitengwa watamuunga mkono na kutoa msaada wa kupingana na dhulma.

SEHEMU YA SABA

UADUI DHIDI YA UISLAMU SAFI

SURA YA KWANZA

Sababu ya Mapambano na Uadui

Migogoro ya Waislamu ni kwa Ajili ya Maslahi ya Ukoloni

Uislam na madhehebu Tukufu ya Ja'fari ni kizuizi, hushika mikono ya mabepari, iwe kushoto ama kulia na maulamaa ambaao ni walinzi wa kizuizi. Kwa jitihada zao, mabepari wameshindwa kufanya watakalo katika nchi za Kiislam hususan Iran.

Takriban ni karne sasa wamekuwa wakiweka mitego tofauti tofauti ya kuondoa kizuizi hiki. Wakati mwingine walitumia njia ya kuingiza vitendo vyao vichafu kwenye nchi za Kiislam na mara nyiningine kwa njia ya kuunda na kutengeneza dini na madhehebu batiili kama Bahai, Uwahabi na pia kwa njia ya kuanzisha vyama vyaa uchochezi.

Maulamaa wa Kiislam ni Kizuizi Kinachozuia Unyang'anyi

Ulaya kwa muda mwingi walichukua hatua hii kuwashawishi maulamaa na wenye msimamo mkali wa dini. Si rahisi kuzivuta nchi za Kiislam kwa wepesi. Waibe rasilimali za utajiri zinazopatikana bila ya kuulizwa ili watimize malengo yao ya ukoloni (ubepari) na unyonyaji na wayafanyie kazi. Ndipo walipogundua kwamba mizizi ya mapenzi ya dini ipo na inatokana na tabligh na kazi za maulamaa

wa Kiislam. Mapenzi waliyokuwa nayo katika dini yao kamwe hai-towezekana kabisa kuyachukua kutoka kwao.

Kama tutasoma historia hii kwa miaka mia moja na miaka mingine mia, basi tutaweza kuona ni kwa nini makundi kwa makundi toka ndani na nje wanafanya njama toka ndani na nje, kuwapinga, kuwanyang'anya kalamu, kupinga maneno yao na kuwaandika katika magazeti yao. Asili yake hii ni nini?

Katika miaka mia moja iliyopita waliona kuwa mzee katika kijiji kimoja nchini Iraq (Samarrah), wakati alipoona Iran ipo kwenye shinikizo la kigeni la mkataba wa aibu uliofungwa, mzee huyo aliyejewa kando ya kijiji kimoja hicho, akaandika mstari mmoja, mstari ambao uliweza kukabiliana na Vikosi vyote vya ndani na nje na vilishindwa kupigana na mstari huu mmoja.

Alikuwa ni marehemu Mirzai (Allah amrehemu) ambaye alii-haramisha tumbaku katika kijiji cha Samarra. Hii ni kwa sababu Iran ilikuwa imekaribia kifungoni kuititia mkataba huu wa tumbaku. Yeye aliandika kuwa, "**Tumbaku ni Haram.**"

Hata kwa jamaa zake pia taratibu iliweza kutoa natija kutokana na fatwa hii na wavutaji wakashindwa. Katika zile sehemu ambazo tumbaku ilikuwa na soko sana wakazimwaga barabarani, wakazichoma moto. Mwishowe wakavunja mkataba kabisa. Kuvunjika kwa mkataba huu ndipo wakaona kwamba kitu kama hiki ambacho ulamaa mzee kama huyu aliyejewa katika kona ya kijiji kati ya vijiji vya Iraq, anaandika neno moja tu na taifa zima linasimama kidete!

Hivi ndivyo ilivyokuwa kwetu sisi kwa Shah na rafiki zake (Waingereza). Hivi ndivyo inavyotakiwa kwa maulamaa kuwa na nguvu moja ya kupinga kitu.

Hofu ya Uislam Kuingia katika Nchi Nyingine

Kama hivi muonavyo, hizi ndiyo propaganda za watu hawa, za kumpambana dhidi ya Iran. Vikundi kwa vikundi vyombo vya habari, mara kwa mara, hutumiwa dhidi yetu kuupinga Uislam. Sisi tunataka kustawisha utamaduni wa Kiislam kila mahali, wao wanaogopa iwapo Uislam utafika katika nchi zao kitakachobakia ni kutokuwa na nafasi sehemu yoyote ile.

Mapinduzi ya Kiislam yanatokana na muundo wa kwanza kabisa uliokuwepo tangu mwanzo wa Uislam. Siyo hivi kwamba mtu mmoja, tuseme alikuwa mwathirika wa magharibi au mashariki, akafanya mapinduzi, akawaita watu kwenye mapinduzi aliyoafanya, yakaweza kuwa ni mapinduzi. Ni masuala yasiyokuwa mapinduzi. Ni suala la taifa moja kusimama kidete kukata mkono wa dhulma ndani na nje.

Kusimama kwa taifa moja ni kukabiliana na mamlaka zote zenye nguvu. Ni lazima wote wawe tayari kwa kuwa mamlaka zote zimevamia na hatuna matumaini yoyote kuwa Marekani au Urusi watakuwa na maslahi na sisi. Wote hawa wanaona iwapo mapinduzi haya yatafanikiwa nchini Iran *Inshaallah!* wataifiki kwa malengo. Hivi ndivyo ambavyo Uislam unataka kupata utafiti. Kulazimisha mapinduzi haya yafike nje wala pia haihitaji mtu kwenda kufanya kazi hii. Lakini ni wajibu kuyatangaza kila mahali.

Lakini, kama watu wa dunia watayatambua mapinduzi haya kama ambavyo wanayatambua sasa, wenye nguvu (wababe) nao pia watayatambua, watahisni hatari. Madhalim pia watatambua kwamba huenda hii ikawa ni njia ya uokovu. Mapinduzi haya kama yatafiki malengo yake na Uislam ukawa na serikali, hapa basi kusingelikuwa na chochote chenye hadhi zaidi kuliko Uislam.

Hili ni tishio kwa mamlaka zote kubwa zenye nguvu pamoja na washirika wao na ni njia ya matumaini kwa walioonewa duniani, kwa maana kwamba, Mitume wote tangu kuumbwa kwa ulimwengu wa kwanza hadi sasa walikuwa wakiyatufuta.

SURA YA PILI

Mbinu za Mapambano na Uadui

Udanganyifu na Udhahilishaji wa Mataifa

Katika historia, karne iliyopita, juhud zimekuwa zikifanyika kwa mataifa ya dunia ya tatu wawe wamelala, wameghafili na wasiwe wanatambua shakhsiya (tabia) zao wenyewe. Hali hii il-iendelea kwa muda mrefu sana na daima ilikuwa ikikua mara kwa mara hadi mwisho huu ulifikia ukuaji kwa kiasi kikubwa.

Kuondoa Athari za Imani ya Dini

Wasaliti - mabepari - waliitaka mashariki, hususan miji ya Kiislam, washughulike kwa ajili ya maslahi yao wenyewe. Kutokana na utafiti walioufanya katika miji hii na miji mingine yote, walipata kuishi watu wa kiroho makundi kwa makundi.

Walifanya utafiti wakafikia hapo walipofikia kwamba wasiwaache Waislam washikamane na Qur'ani Tukufu kwa sababu waliona kwamba Qur'ani ndiyo kikwazo chao kikubwa. Endapo Waislam wote watashikamana na Qur'ani, basi hakutakuwa na nafasi itakayobaki kwa ajili yao. Hivyo, kilichobakia ni kuwatenganisha watu na Qur'ani na Uislam na kutenganisha mataifa na Uislam.

Nukta muhimu ambayo sisi sote tunatakiwa tuizingatie hasa ni kanuni na sera zao pamoja na ugeni wanaojiwekea. Hii ni kwamba, kwa maadui zetu na mabepari, mpaka lini na mpaka wapi sisi tunaweza kuwavumilia na kwa mipaka ipi watakubaliana na uhuru wetu. Kwa hakika, mipaka yao hawa si chochote isipokuwa ni kue-

puka utambulisho na maadili ya kiroho na kutomtambua Allah wetu Mtukufu.

Kwa mujibu wa Qur’ani Tukufu, kamwe hawataacha kuwaua na kugombana na ninyi hadi pale watakapowatoeni kutoka kwenye dini yenu. Tutake tusitake, Mazayuni, Marekani na Urusi wataendelea kutia doa utambulisho wa dini yetu na utukufu (hadhi) uliokuwamo ndani ya dini yetu

Baadhi ya watu wetu wenye fikra na mitazamo wamekuwa na chuki na uovu kwenye mambo ya siasa katika jamii. Walivyoileza ni kwamba, yanayoshutumiwa na kutupiwa lawama wanasema kuwa ni: “Mapinduzi ya Kiislam ndiyo chanzo cha adui, yamekuwa yanatupiwa jicho toka Mashariki na Magharibi.”

Vizuri, swalii hili linaweza kujibisha kwamba, mataifa ya dunia ya tatu na Waislam hususan taifa la Iran, ni katika zama zipi wali-kuwa karibu na watu wa Magharibi na Mashariki, ambapo hadi leo wakakosa kuheshimiana na kuhusiana!

Kupinga Maendeleo ya Kuutangaza Uislamu

Njama muhimu katika karne iliyopita hasa katika miongo ya sasa baada ya ushindi wa mapinduzi imekuwa kutupiwa macho na propaganda za kila aina ili kupoteza na kukatisha tamaa mataifa hususan taifa linalojitolea la Kiislam la Iran.

Wakati mwengine walitoa sababu na hoja ya kwamba hukumu ya dini ya Kiislam ni ile ya miaka 4000 iliyopita, ambayo haiwezi kuongoza nchi katika zama hizi, au Uislam ni dini inayopinga maendeleo, inapingana na kila ustaarabu na kamwe haiwezi kulinganishwa na ustaarabu na tamaduni za kidunia za zama hizi na mfano wa propaganda za kijinga zinazofikishwa katika ulimwengu wa Kiislam.

Moja katika harakati zinazofanywa na wakoloni katika nchi za Kiislam ni kuutangaza Uislam kuwa umepitwa na wakati. Viongozi wa makabila wanasema kwamba ni ibada iliyopitwa na wakati na ya kizamani, inayopingana vikali na maendeleo. Hivi ndivyo wanavy-outangaza Uislam.

Asili ya mawazo haya ni ujisadi wa kibanaadamu ambao kwa njia yoyote ile lazima uondolewe aidha kwa kijeshi, kiuchumi, kima-hakama na kisha ya kiutamaduni.

Utamaduni wa kifisadi wa mashariki na magharibi unajinadi kuwa wanamiliki vifaa adhimu, kila wakati wanatunga uongo na tuhuma dhidi ya utamaduni wa Allah (s.w.t), Uislam na kwa kila na-fasi wanayoipata wanaponda na kuharibu kanuni ya sheria za Allah (s.w.t), asili ya Uislamu na Jamhuri ya Kiislam.

Wenye kushirikiana nao wanadai kwamba ibada ya kizamani haina siasa, hawajui kuwa sheria ya Uislam inatosheleza kwa wakati huu, kwa kisingizio kuwa ni sheria ya miaka 1400 iliyopita, haina uwezo wa kiutawala. Kwamba, dunia ni mpya ambayo ndani yake haina wakati. Baadhi ya watu wanadai Uislam ni somo lenye kujirudia.

Matangazo mbalimbali na adhimu yanayoonekana dhahiri dhidi ya Iran na ukweli dhidi ya Uislam, kwamba mapinduzi haya ya Iran kamwe hayawezi kuendesha nchi yetu. Au, dola ya Iran ipo katika hali ya kuanguka kwa sababu hakuna uchumi salama, hakuna utamaduni sahihi, hakuna jeshi wala silaha za kijeshi zilizo tayari tayari. Matangazo haya yanaenezwa na kutangazwa na vikundi vya wanahabari wa Marekani na washirika wake. Wanachochea maadui wa Iran na Uislam. Ukweli ni kuwa, propaganda wanazozifanya dhidi ya Uislam wanajifanya wanadai kwamba Uislam katika zama hizi hauna nguvu ya kuongoza nchi.

Hawa wanaotuombea mabaya wanasema nini? Uislam umetawala na kuongoza dunia kwa zaidi ya nusu karne na kutawaliwa na tawala za kikafiri na madhalimu kwa chini ya nusu karne. Ni vipi hivi sasa kuwe na ajizi katika kuongoza nchi?

Leo, taifa letu linasaidia kupanga na kuongoza nchi kwa kuzipa uhai shughuli mbalimbali na mashirika yake. Maadui wa Uislam ni kutokana na nguvu ya Uislam kwa kuuvunja vunja ukandamizaji na kuanzisha idara za nchi kwa kuzingatia kughafilika kwa uadilifu.

Maadui wa Uislam wengi wao ni marafiki wa Waislam. Waislam ambao pia wana nguvu na uwezo wa kuongoza, na hawana habari juu ya hukumu za kisiasa, kijamii na Kiislam

Kupinga na Kupambana na Watetezi wa Uislam Safi

Wote wanatambua kwamba leo tunauona uhalifu wa wazi kutoka kwa walowezi na mabepari, eti kuulinda Uislam na kuuchukua rasmi utawala wa Jamuhuri ya Kiislam kutoka mikononi mwa wanaowaita madhalim na mwa Kifalme. Uhalifu na dhambi zetu ni kuzipa uhai Sunna za Mtukufu Mtume wetu (s.a.w.w), kutekeleza kwa vitendo maamrisho ya Qur'ani Tukufu, kutangaza Umoja baina ya Waislam hususan Shia na Sunni kwa ajili ya kukabiliana na njama za makafiri wa dunia, kutetea taifa linaloonewa la Palestina, Afghaniastani, Lebanon, kufunga ubalozi wa Israili nchini Iran, kutangaza vita dhidi ya Uzayuni, kupambana dhidi ya ubaguzi, kuwatetea watu wanaoone-wa wa Afrika, kupinga mikataba ya kitumwa na kuutangaza uchafu na uonevu wa Marekani.

Je, kuwa karibu na walowezi, kuwa nyapara wao asiyekuwa na idara na kuwa karibu na wanaouzungumzia Uislam na utawala wake, ipi ni dhambi kubwa kuliko? Kwa hadhi ya Waislam wali-yokuwa nayo na kwa uhuru, wamesimama na kukualika kukabiliana na waonevu warukao mipaka.

SEHEMU YA NANE

Utaratibu wa Kutoa Utawala kwa Uislam wa Kimarekani

SURA YA KWANZA

Maadui Wakuu wa Uislam Safi

Suala lililo muhimu sana linaloleta maumivu makali ni kwa mataifa ya Kiislam, nchi zisizokuwa za Kiislam na zile tawala zilizo chini ya uangalizi wao ni mada kuhusu Marekani. Serikali ya Marekani ina nguvu zaidi ya nchi zote duniani na inayoongoza kwa kumeza, kutawala nyenzo na hifadhi za nchi nyingine, na hakuna jaribio lolote iliyoshindwa kulifanya.

Marekani ni adui namba moja kwa watu wanaoonewa na wale wanaodhoofishwa duniani. Marekani ipo kwa ajili ya kutawala mamlaka zote kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijeshi. Vyote hivi inataka kuviangalia viwe chini ya himaya yake. Hakuna ye yote anayeweza kuepuka uhalifu wake.

Marekani imekuwa ikisambaza matangazo kwamba ina mapenzi kwa watu wanaodhulumiwa duniani, lakini ni mnyonyaji wa kimataifa kwa kushirikiana na Mazayuni.

Kwa njia yake ya utata, vitendo vyake vya khiyana na namna alivyokuwa akimwaga damu za watu wasio na hatia hujiona kwamba zaidi yake na wanaoandamana naye, hakuna mtu mwenye haki ya kuishi.

Asili ya Marekani na Urusi ni chuki na uadui dhidi ya Uislam Safi wa Muhammad (s.a.w.w). Wamekuwa ni wenye kupiga wimbi juu ya hilo. Chombo hiki (Umoja wa Mataifa) ni mafanikio kwa wakoloni ambacho kina nia ya kuwapora watu wanyonge duniani na hii ndio sababu ya kuwa na upinzani mkubwa na ninyi.

Ewe Allah (s.w.t)! Leo hii nguvu zote na mamlaka zote zimekuwa sumu ili waweze kukata mizizi ya Uislam Safi wa Mtukufu wetu (s.a.w.w) Ee Mola! Leo sauti zetu pamoja na chuki walijokuwa nayo katika dini yako, wameungana kwa pamoja duniani ili waweze kuzima sauti ya Uislam wa Muhammad (s.a.w.w).

Waislamu mliokuwa tayari kutoka kila taifa na madhehebu mbalimbali, lazima mtambue vizuri kuwa adui yetu wa asili wa Uislam, Qur'ani, na Mtukufu Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w) hasa ni Marekani na mtoto wake fisadi Israili, ambaye ana jicho la tamaa katika nchi za Kiislam kwa ajili ya kupora rasilimali zilizopo ardhini na juu ya ardhi. Kamwe hawawezi kuuacha uhalifu wao na njama zao katika nchi hizi kwa kupidisha njama za kishetani, kwa kila linaloweze-kana ni lazima liwe kwa kuleta mgawanyiko baina ya Waislam.

Katika msimu wa Hijja, inawezekana kuwa watu kama vile maulamaa wanaweza kuungana na nguvu hiyo, wakatumika kwa ajili ya kutengeneza tofauti baina ya Shia na Sunni. Mbaya zaidi, jambo hili limegeuka, limeweza kuaminiwa kirahisi na baadhi ya watu na limeweza kusababisha ufisadi wa hali ya juu.

Ndugu zangu kina kaka na kina dada wa kila madhehebu! Mnapaswa kuwa makini kujua kwamba vitendo hivi ni kwa lengo la kuliaibisha jina la Uislamu, Qur'ani na Sunna ya Mtume (s.a.w.w). Wanachotaka ni kuuharibu Uislam, Qur'ani na sunna au angalau kuwapotosha Waislam.

Kina kaka na kina dada! Mnapaswa kujua kwamba Marekani na Israeli ni maadui wa Uislam. Kwa kuwa Uislamu, Kitabu na Sunna ni njia yao ya kuchochea na, kuwahamasisha. Ili kuzuia unyang'anyi wao, wanajua kwamba Iran wanafuata Kitabu hiki na Sunna, walismama katika kukabiliana nao, hatimaye wamekuwa wanamapinduzi na walishinda.

SURA YA PILI

Pigo kwa Uislam kwa Kutumia Jina la Uislam

Dini za Allah - *tauhidi* - zilikuwa ni za kwanza kuwepo kwa wanaadamu. Lakini kwa masikitiko, zimepitia kwa wakiukaji kiasi kwamba hazikupaswa kuenea hususan kwa madhehebu ya Mtukufu Nabii Isa (a.s) ambayo liliangukia katika mikono ya kabile moja, ukatokea upotoshaji, kunakili mambo yasiyostahili kwa Nabii Isa (a.s) na mbaya zaidi, yule sultani aliyejinasibisha na madhehebu haya hakuwa Masihi (Yesu), alikataza mafunzo ya Hadhrat Isa (a.s) yasitolewe ili ukweli usije kugundulika.

Iwapo mafunzo ya Hadhrat Isa (a.s) kwa Wakristo, Hadhrat Musa (a.s) kwa Wayahudi na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa Waislam yangeachwa huru kwa kila mtu anayetaka kufanya uchambuzi ili ukweli ujulikane, basi leo hii kusingelikuwa na matatizo haya yaliyokuwapo mionganoni mwa watu.

Ninyi wenye kazi kubwa zilizofanyika, wanafanya uhalifu duniani kiasi kwamba nchi kubwa kwa jina la Ukristo inajinasibisha kwa jina la Hadhrat Isa (a.s)? Hali kadhalika, ni uhalifu gani waufanyao viongozi wa nchi za Kiislam kwa jina la Uislam? Licha ya kwamba wao pia ni Waislam.

Kuuficha Ukubwa na uhalisia wa Uislam

Moja ya kazi kubwa zilizofanyika - na ninafikiri kuwa haya yamefanywa na mashetani hawa - ni kuwa, Qur'ani na Uislam vibakie hivyo hivyo vilivyo tu na hawakutaka Waislam wavielewe. Wamefanya ushawishi na propaganda hii hadi kwenye vyuo vikuu vyatikidi vya Najaf (Iraq) na Qum.

Hii ina maana kwamba, kwa upande mmoja iwe ni thamani ya Uislam, kwa upande mwengine iwe ni thamani inayohesabiwa baina ya wasomi wa Kiislam na thamani ya Uislam nyingine ibakie chini yake, ijifiche.

Hawakutaka sisi tuufahamu Uislam hivi jinsi ulivyo kwani, moja ya hatari walizoziona wao ni kuwa, endapo Uislam utafahamika jinsi ulivyo, basi watu wote watatoka kwenye dini zao na kufuata. Haitobaki nafasi tena kwa ajili yao. Hawakutaka kuongoka ingawa walinyaona mafunzo ya Uislam. Wakati Waingereza walipokwenda Iraq, mmoja wao alisikia sauti ya adhana, akauliza, "Ni nini hicho?" Wakamjibu kuwa hiyo ni adhana. Akauliza, "Je, hii ina hasara kwa dola ya Uingereza?" Wakamjibu, "Hapana." Akasema, "Kila una-chotaka basi sema adhaan."

Yaliyopo katika mjadala huu ni kwamba sisi tunajadili kuhusiana na himaya ya Uingereza na Jamhuri ya Amerika – sijui - kama hakuna madhara katika Jamhuri ya Kisovieti, hawa wanaangalia sana upepo unakoelekea ili waweze kurefusha mjadala zaidi na iwapo itapelekea hasara kwao basi watafanya kila njia suala hilo lisifanikiwe. Kama akiishauona upepo anarudi na kufanya majadiliano yote kwa kirefu. kile kilicho onekana kina hasara kwao basi hawakiachii kifanyike.

SURA YA TATU

Kuleta mgawanyiko katika mataifa na kuzua tofauti baina ya Waislam

Serikali za kikoloni, serikali ambazo kwamba wanataka kuchukua rasilimali za Waislam na vifaa mbalimbali, kwa hila na udang-anyifu wa kila aina katika dola za kiislam, kuwadanganya wakuu wa majimbo ya Kiislam, wakati mwingine huleta tofauti kwa jina la Sunni na Shi'ah. Hata kwa wale ambao wako katika Mashariki na ambao si Waislam wamekuwa wanadanganyika.

Inasemekana kwamba nchini India katika siku za Idi al Adha, idadi kubwa ya ng'ombe watukufu huletwa kwa waabudia ng'ombe. Kisha huuzwa kwa Waislam kwa bei rahisi. Hulazimisha hao ng'ombe walio karibu kwa utukufu kwa taifa wachinjwe. Baada ya kuwachinja husema, Waislam wamewachinja ng'ombe wenu watukufu.

Mhemko huu hutokea katika mataifa ya Wahindi, baina ya Wahindu na Waislam. Pia katika nchi za Kiislam, huzua na kueneza mambo baina ya mataifa kwa jina la Uislam, kwa jina la madhehebu, tabligh inayofanywa na Waislamu na mwishowe huangukia katika kuuana, pia hupatikana hitilafu baina ya Sunni na Shia, wao wanapata mwanya wa kuchukua rasilimali walizokwu nazo Waislam, wakati Waislam wanashindwa kufanya shughuli zozote zile.

SEHEMU YA TISA

Wadhifa wa watu kuutambua Uislam Safi

SURA YA KWANZA

Jukumu la mataifa na watu

Kuubaini, Kuutambua na Kuufikisha Uislam

Sisi tuna wadhifa mkubwa mno, siyo sisi tu, bali waislam wote, si wewe tu, bali pia sehemu yote nchini Iran na nje ya Iran na wote ambao mmechukua ahadi katika Uislam, tunayo fursa kubwa ambayo hivyo ndivyo ilivyo katika Uislam. hivyo ndivyo Allah (s.w.t) alivyotuamrisha, hivyo ndivyo zilivyokuja riwaya zetu na Kitabu chetu Qur'ani tukufu, hivyo ndivyo ulivyyowasilishwa kwa watu, katika dunia na wenyewe pia unaweza kuwa na ufanisi **kwa maelfu ya mipira** na zaidi ya **matanki**.

Uongofu unaweza kupatikana, kwa kurudisha nyoyo za watu na kazi hii hasa inatokana na sanaa iliyokuja katika hukumu ya Kiislam, kamwe haitofanya kazi kwa mpira mmoja wala tanki na ninyi wenyewe mnaona ya kwamba licha ya nguvu walizokuwa nazo na kumiliki nyenzo mbalimbali duniani lakini kila siku ni wenyе kushindwa.

Mnapaswa kufahamu kuwa Uislam, tangu kuasisiwa kwake hadi sasa umehifadhiwa na mafaqih (maulamaa). Baadhi ya masuala yаликуwa na nguvu na yalitekelezwa, na masuala mengi yaliyokuwa katika Qu'rani, vitabu na habari za mafaqih ni kamili na hayajaharibiwa.

Mfahamu ya kwamba hadi pale mtu anapoonekana dhahiri yupo sahihi, hakuwa na ufahamu katika Uislam, na mara moja akaelewa kuwa amekwenda kinyume na njia ya haki, ni lazima uhakikishe kuwa Uislam wako usijitenge na maulamaa. Na kwa wale ambao Uislam wao unapingana na maulamaa, basi ni lazima mpingane nao.

Kuunda Umoja wa Waislam

Ni lazima tupate mafunzo ya Uislam vile vile ambavyo Uislam ul-ivyo tuamrisha, kwamba, muumini na waumini wote, popote pale walipo ni ndugu. Uislam umetuamrisha kwamba, wote kwa pamoja tushikamane na kamba ya Allah na kamwe tusifarikiane. Pia tu-meamrishwa kuwa tusipambane na kupigana wenyewe kwa wenyewe, ama sivyo tutashindwa.

Wakati Waislam wenyewe watakapoweza kuondoa hila za wakoloni na hila za mamlaka za kifisadi na kuafikiana katika amri za Allah tangu mwanzo wa Uislam hadi mwisho, basi tutaweza kuafikiana katika wito huu wa Allah (s.w.t).

Udugu wetu tunautangaza kwa ndugu zetu Masunni, maadui zetu wa Uislam wanataka tuhitilafiane na ndugu zetu. Maadui zetu na wale waliodanganywa na hao, kuanzia sasa wanatangaza kuhitifiana kwetu baina ya makundi haya mawili. Tunasema kwamba, umoja ni neno la Waislam.

Iwapo Waislam watashikamana na neno umoja, kamwe watu hawa hawatapata mwanya wa kutuwatawala. Mfarakano huu uliopo baina ya Waislam ndiyo sababu ya hawa watu kupata fursa ya kututawala. Isitoshe, mfarakano huu uliopo baina ya Waislam umegunduliwa na mtu mmoja jahili na sasa tumekuwa watu wa shida.

Ni wajibu wetu kwa kila Muislam tuwe pamoja. Muda huu ni muhimu sana. Kwa hakika tupo katika usambazaji baina ya uhai na

mauti. Hivi sasa nchi yetu, aidha sisi tunapaswa kuwa chini ya nira ya ukoloni na udikteta milele au tunapaswa kujinasua kutoka katika nira hii. Iwapo hatutahifadhi neno hili la umoja, basi mpaka mwisho ni lazima tutaathirika.

SURA YA PILI

Nafasi ya Hawza na Vyuvo Vikuu

Ulezima wa Kubaini, Kuutambua na Kuufikisha Uislam

Vijana wasomao dini na wasomao vyuoni mnapaswa kutumia muda wenu kuzitambua kanuni za msingi wa Uislam. Uislam msingi wake mkuu upo katika *tawhiid*, uadilifu na kuwatambua Mitume ambao ndio waliokeleza hukumu hii ya Uadilifu na uhuru kuanzia kwa Ibrahim, kipenzi cha Allah hadi kwa Mtume wa mwisho, Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w). Na katika kuelewa hatua za fikra zao, kuanzia kwenye nukta ya mbali, yenyе kina cha kiroho na *tawhiid* hadi pale kwenye hatua ya kuitengeneza jamii.

Jitahidini muweze kuueneza Uislam kwa watu. Asasi hizi za Kislam zifanyе juhudи, kwani jambo hili ambalo sisi tunalo hakuna mtu mwingine aliye nalo, Qur'ani hii ambayo sisi tunayo wengine hawana, sunna hizi ambazo sisi tunazo watu wengine duniani hawana, hivyo ni lazima muelimishe.

Kuulinda Uislam na Kutambua Hukumu za Mafaqih – Maulamaa

Kutekeleza kazi ya Allah (s.w.t) kwanza ni kuulinda Uislam. Sisi sote, mataifa yote, maulamaa wote na wote ambao mnajitambua kuwa mnao wajibu huu, mtambue kuwa hii ni zawadi ya Allah (s.w.t) na inabidi muihifadhi, kwani sasa Uislam umekabidhiwa mikononi mwetu.

Laiti kama tungelikuwa na udhuru tangu mwanzo, wenye nguvu -wenye mamlaka - wasingelituachia tuweze kufanya chochote. Wa-

likuwepo kama hao waliokuwa wapinzani, maulamaa walizuiliwa kutekeleza majukumu yao. Leo hii tena, sisi hatuna udhuru kama huo. Maulamaa, popote pale walipo, wanaweza **kuwakumbusha watu** masuala mbalimbali, **kutatua** matatizo yao na matatizo ya watu. Wameweza kuyasikiliza na wameweza kuwaonya na kuwaongoza watu kama ambavyo taifa hili linavyoongoza na kusimamia watu.

كلم راع و كلم مسئول

“Kila mmoja wenu ni mchunga, na kila mmoja ataulizwa alichokichunga”

Na huu uchungaji ndio unaostahili kwa ajili ya maulamaa. Hivyo, sisi sote ni wenye kuwajibika na tunayo *mas’uliya*. Hata kama watatuua wote, wale watakaokuja baada yetu ni lazima wa-chukue nafasi hii.

Huu ndio Uislam, Uislam unatulazimu sisi sote tujitoe muhanga, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alijitoa muhanga kwa ajili ya Uislam. Bwana wa mashahidi, Imam Husein (a.s) alijitoa muhanga. Uislam ni jambo kubwa sana ambalo Allah (s.w.t) amekabidhi kama amana kwa wanadamu. Ni lazima tuihuishe azma yetu na tuwe mashujaa katika njia hii na tuwe wasomi zaidi.

Somo na mjadala huu ni juu ya kuuhifadhi Uislam. Siku ambayo Uislam utahitaji hifadhi hiyo, basi maulamaa nao pia wanatakiwa wajitokeze kwenye uwanja wa vita, ni lazima waende. Siku ambayo Uislam utahitaji hifadhi hiyo, basi pia vyuo vikuu vya kidini (*Hawza*) viwe na mapumziko na washughulike na kazi moja tu, ya kuulinda na kuuhifadhi Uislam.

Kwa kufupisha maneno, sisi tunapaswa kuzingatia kusudio la kutambua vitendo vya maulamaa wa Kiislam ili kufanikisha kuitawala

dunia, bila kujali hila za magharibi na uchokozi wa mashariki na bila kujali udiplomasia. Kwa muda mrefu, fiqhi imebakia katika vitabu na imekuwa ni siri vifuani mwa maulamaa. Mabepari hawastahiki, hata kama maulamaa wote wasishiriki kufanya juhudini kutatua matatizo na masuala mbalimbali, kamwe mabepari hawawezi kuelewa kwamba, mlango wa ijtihad unatosha kuongoza jamii.

Vyuo vikuu nya kidini (*Hawza*) na maulamaa wanapaswa kufikiria kwa makini mahitaji ya jamii ijayo, na siku zote iwe chini ya himaya yao pamoja na kupiga hatua mbele kutohaka na matukio na kuwa tayari kupata jibu sahihi na lenye kustahiki. Labda kwa miaka ijayo waweze kubadilisha mbinu za kuongoza jamii ya watu na kwa ajili ya kutatua matatizo yao kwa kutafuta masuala mapya yenye kuhitajika. Hivyo maulamaa wakubwa wa Kiislam kuanzia sasa mnapaswa kufikiria na kuitafakari kwa kina mada hii.

Na tunapata natija kwamba iwapo maulamaa watachelewa kuteetea na kuushabikia **Uislam Safi** na mapinduzi basi mamlaka zenye nguvu na vibaraka wao watayamaliza masuala haya kwa maslahi yao wenyewe. Jamii ya waalimu mnapaswa kuwajua wasomi wa dini watukufu, wanamapinduzi waliofanya bidii kwa taabu zote, waliopigwa na kushiriki katika vita kwa ajili ya dini tukufu na mapinduzi ya Kiislam.

Ni lazima mfanye vikao pamoja na wao, mpange mipango, wekeni mikakati, pokeeni mawazo yao na heshimianeni nao. Kwani, kuwaheshimu wao na kukabiliana na taifa lisilokuwa na mpangilio maalum ndipo hapo wasomi hupata fursa ya kuwa kitu kimoja. Pia, wao wawetayari kujitoa muhangna na kuwa mashujaa ili kuwaongoza watu.

Sasa katika jamii ya watu wasomi wa dini, sisi tulivyokuwa tunafikiria zamani ni kwamba wengi wa maulamaa watakuwa kweli ni watu watendao haki, waaminifu na watiifu kama ilivyokuwa katika zama za Maasumin (a.s).

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzu Ya Kwanza Mpaka Thelathini
2. Uharamisho Wa Riba
3. Uharamisho Wa Uwongo Juzu Ya Kwanza
4. Uharamisho Wa Uwongo Juzu Ya Pili
5. Hekaya Za Bahlul
6. Muhang'a Wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo Iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab Vazi Bora
9. Ukweli Wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu Imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini Katika Swalaa
16. Misingi Ya Maarifa
17. Kanuni Za Ndoa Na Maadili Ya Familia
18. Bilal Wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi Wa Historia Ya Uislamu Na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an Na Hadithi
24. Elimu Ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu Ya Shia
26. Ukusanyaji Na Uhifadhi Wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo Kutoka Katika Qur'an
29. Uislamu Mfumo Kamili Wa Maisha Ya Kijamii
30. Mashukio Ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu Kwa Mujibu Wa Kitabu Na Sunna.
34. Haki Za Wanawake Katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu Na Sifa Zake
36. Kumswalia Mtume (S)
37. Nafasi Za Ahlul Bayt (A.S)
38. Adhana

39. Upendo Katika Ukristo Na Uislamu
40. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
41. Maana Ya Laana Na Kutukana Katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka Juu Ya Khofu
43. Kukusanya Swala Mbili
44. Bismillah Ni Sehemu Ya Qur'ani Na Husomwa Kwa Jahara
45. Kuwaongoza Vijana Wa Kizazi Kipyta
46. Kusujudu Juu Ya Udongo
47. Kusheherekeea Maulidi Ya Mtume (S)
48. Tarawehie
49. Malumbano Baina Ya Sunni Na Shia
50. Kupunguza Swala Safarini
51. Kufungua Safarini
52. Umaasumu Wa Manabii
53. Qur'an Inatoa Changamoto
54. As-Salaatu Khayrun Mina - 'N Nawm
55. Uadilifu Wa Masahaba
56. Dua E Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu Wa Binadamu
58. Umaasumu Wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu Wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu Wa Mitume - Umaasumu Wa Mtume Muhammad (S)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu Ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu Ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala Ni Nguzo Ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora Wa Imam 'Ali Juu Ya Maswahaba Na Ushia Ndio Njia Iliyonyooka
75. Hukumu Za Kifikihi Zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-U-Llaah
77. Muhammad (S) Mtume Wa Allah
78. Amani Na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani Na Mtume Muhammad (S)

81. Mitala Na Ndoa Za Mtume Muhammad (S)
82. Urejeo (Al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (Al - Badau)
85. Hukumu Ya Kujenga Juu Ya Makaburi
86. Swala Ya Maiti Na Kumilia Maiti
87. Uislamu Na Uwingi Wa Dini
88. Mtoto Mwema
89. Adabu Za Sokoni
90. Johari Za Hekima Kwa Vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi Katika Usunni Na Ushia
96. Hukumu Za Mgonjwa
97. Sadaka Yenye Kuendelea
98. Msahafu Wa Imam Ali
99. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma Sura Zenye Sijda Ya Wajibu
102. Hukumu Zinazomuhusu Mkuu Wa Kazi Na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru

123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzuniqa na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukumu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swalaya Jamaa na Msikitii.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu

165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'an
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi

206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Mahali na Mali za Umma
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA

KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH

FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique